

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 16 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa 03:00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Rais – T AMISEMI, Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Shangazi!

Na. 399

**Kuanzisha Shule za Kidato cha 5 na 6 – Segerea**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y MHE. BONNAH M. KALUWA)** aliuliza:-

Katika Jimbo la Segerea zipo shule kumi na moja za sekondari za Serikali ambapo wanafunzi wa shule hizo wanafaulu vizuri kwa kupata daraja la I, II na III na kuwa na sifa ya kujiunga kidato cha tano. Kwa mfano mwaka 2015 wanafunzi zaidi ya 400 walifaulu kwenda kidato cha tano,

lakini katika Jimbo la Segerea hakuna hata shule moja ya kidato cha tano licha ya kuwa na maeneo ya kujenga ya kutosha katika shule za sekondari za Kinyerezi, Magoza na Ilala.

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuanzisha shule za kidato cha tano na sita katika maeneo ya shule zilizotajwa ili kuwapunguzia wanafunzi hao adha ya usafiri wanayopata kwa kufuata shule mbali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ina jumla ya shule za sekondari za Serikali 49 zikiwemo shule sita kongwe. Kati ya shule hizo, saba ni za kidato cha tano na sita. Halmashauri inaendelea kuboresha miundombinu ya shule ya sekondari Juhudi ili iwe na Kidato cha tano na sita. Aidha, katika mpango wa muda mrefu Halmashauri imepanga kuanzisha shule sita za kidato cha tano na sita kuanzia mwaka 2017 hadi 2022. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha shule hizo zinakuwepo katika kila tarafa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za kidato cha tano na sita ni za kitaifa ambapo zinachukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini, ndiyo maana wanafunzi 400 kutoka Jimbo la Segerea wamechaguliwa kwenda shule mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuna maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kama tunavyofahamu Jiji la Dar es Salaam linazidi kupanuka na maeneo ya pembezoni zipo sekondari nyingi ambazo mwisho wake ni kidato cha nne; na kwa kuwa katika Jimbo la Segerea hasa katika eneo la Kinyerezi na Kipawa, bado hakuna Sekondari za kidato cha tano na sita. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati sahihi sasa wakupeleka hizi shule za kidato cha tano na sita katika maeneo ya pembezoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa swali hili linafanana kabisa na kule Lushoto, hasa Jimbo la Mlalo. Tunazo Tarafa tano katika Halmashauri yetu ya Lushoto, lakini ni Tarafa nne pekee ndio zenye sekondari ya kidato cha tano. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka Tarafa ya Umba na Mlola nazo zipate sekondari za kidato cha tano? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Jiji la Dar es Salaam linapanuka, na shule nyingi nyingine zimejengwa pembeni mwa Jiji la Dar es Salaam *especial* maeneo ya kule Mbondole, Zingiziwa na maeneo mengine. Kwa hiyo nimesema kama ni ile mikakati wa Kiserikali, kwa sababu Halmashauri wenyewe wana mkakati wa kujenga takribani shule sita mpya za sekondari. Sisi Serikali katika hilo tutawaunga mkono shule hizi, na mara baada ya kukamilishwa kwake tutaweza kuzisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa vijana wetu ambao wanapata nafasi baada ya kumaliza kidato cha nne waweze kupata nafasi ya kidato cha tano na sita. Kuhusu suala la shule za kule Mlalo, Mheshimiwa Shangazi kama mtakuwa mmeianzisha hii mipango kule Mlalo katika Halmashauri yenu ya Lushoto, naomba nikuhakikishie kwamba Serikali haitosita kushirikiana nanyi. Kwa sababu hata nilipokuwa ziarani kule mlinipeleka shule moja ya

sekondari ambayo mmeniambia kwamba watoto wanafaulu kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo Serikali itaungana na ninyi, lakini ni mara tu baada ya kuanza michakato hii mliyoianza ya ujenzi wa sekondari za kidato cha tano na sita. Serikali tutaungana na hilo ili kuwafanikisha wananchi wa Mlalo na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla ili waweze kupata fursa hii ya elimu ya kidato cha tano na cha sita. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia halafu Mheshimiwa Amina.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Lengo la Nne la Maendeleo Endelevu ya Dunia linasema elimu bora sawa shirikishi kwa wote ifikapo mwaka 2020/2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wanafunzi wamefaulu wengi sana ambao wanatakiwa waende kidato cha tano na hasa Shule za Sayansi; lakini kuna tatizo kubwa la wanafunzi wanakwenda kwenye shule hizo hakuna maabara kabisa. Serikali Awamu ya Nne ilianza hili suala la maabara.

Je, nini jukumu la Serikali kwa haraka iwezekanavyo kuhakikisha shule zote za Sayansi zinakuwa na maabara za kisasa ili tujenge Tanzania yenye uwezo wa sayansi na teknolojia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wanafunzi wamefaulu wengi sana mwaka huu, ni kama takribani asilimia 27 ya waliofanya mtihani. Na malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilikuwa kwamba tuwe tunapeleka wanaofaulu hawa wafike asilimia 20, isipungue asilimia 20. Kwa hiyo, utaona kazi nzuri imefanywa na Serikali, lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza sana walimu wa nchi hii kwa kazi waliofanya na kusababisha ufaulu huu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushughulikia kiasi cha wanafunzi 93,018 ambao wamefaulu kwenda kidato cha tano, tumejipanga vizuri tumepeleka kiasi cha shilingi 22,000,000,000 ili kuhakikisha kwamba tunajenga maabara. Fedha hizi zimekwenda toka kama miezi mitatu iliyopita. Ujenzi unaendelea katika shule zote za *A-level* na hasa zitakazochukua wanafunzi wa *combination* za sayansi. Ujenzi huo tunahakika kabla shule hizi hazijaanza kupokea wanafunzi utakuwa umekamilika. Kwa sasa hivi tumetawanya watu kutoka ofisini pale Idara ya Elimu, karibu kila Mkoa tumepeleka maafisa wawili kwenda kuhakikisha kwamba wanasimamia kwa haraka ili shule hizi ziweze kukamilika. Kila shule ambayo tutakuwa tunapeleka wanafunzi zitakuwa na maabara zote zinazostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumeshachukua hatua, tumepeleka fedha hizo na nipende kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kama kuna shule ambayo ipo katika eneo lako basi mtusaidie Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu fedha zimepelekwa na ziwe kwenye Halmashauri zetu, tusimamie tuwe karibu tuhakikishe kwamba shule zile zinakamilika kabla ya tarehe moja mwezi wa saba. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Aah! Mheshimiwa Waziri wa Elimu, nilikuwa sijakuona uko mwisho huku, samahani.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Sambamba na majibu mazuri kabisa yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, ningependa pia kumpa taarifa Mheshimiwa James Mbatia kwamba Serikali pia imeshanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule hizo, kwa hiyo ujenzi utakapokamilika vifaa vipo na wanafunzi watapata vifaa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Tumalize na Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali za kusambaza vifaa saidizi kwa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inajenga shule moja ya mfano ambayo itawajumuisha watoto wenye ulemavu pamoja na watoto wengine ambao hawana mahitaji maalum, ili basi shule hiyo iweze kuwasaidia kwa kiwango kikubwa watoto wenye mahitaji maalum?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakamilisha mapitio ya michoro kwa ajili ya shule maalum ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kujenga shule ya Kisasa ambayo itakuwa ni ya bweni, shule ya msingi na sekondari kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo shule hiyo itajengwa kwenye maeneo ya Chuo cha Ualimu cha Patandi ambacho ni chuo mahususi kwa ajili ya kufundisha walimu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huo utaanza mara moja mara baada ya kukamilisha mishoro kwa sababu fedha kwa ajili ya ujenzi zipo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 400

## **Matumizi Mabaya ya Sheria ya Tawala za Mikoa**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Sheria ya Tawala za Mikoa Sura ya 97 inawapa mamlaka ya kipolisi Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwatia nguvuni watu wa muda wa saa 48, lakini sheria hiyo imekuwa ikitumiwa vibaya na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kutoa amri za kukamata Wabunge, Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na hata watumishi wa umma wakiwemo madaktari.

(a) Je, Serikali inawachukulia hatua gani Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanaotumia vibaya madaraka na sheria hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itaifanyia marekebisho sheria hiyo ili kuwaondolea Wakuu wa Mikoa na Wilaya mamlaka ya kuwaweka watu ndani kwa kuwa ni kandamizi, inakiuka haki za binadamu na inatumika vibaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais –TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kisheria ni wasimamizi wa shughuli zote za Serikali katika maeneo yao ya utawala. Hivyo, ni jukumu lao kuchukua hatua pale sheria za nchi zinapokiukwa ili kuhakikisha kunakuwepo amani na usalama kwa ustawi wa wananchi na Taifa kwa jumla. Hata hivyo, wapo baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao wanatumia vibaya mamlaka yao, tayari Serikali imetoa maelekezo mahususi kuzingatia mipaka yao ya kazi katika kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Wakuu wa Mkoa na Wilaya wamepeva madaraka ya kuwa mlinzi wa amani na usalama (*peace and security*). Kifungu cha 7 na 15 vya Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura, 97 Vinawapa Mamlaka viongozi hao kumweka ndani mtu yeyote kwa muda wa saa 48 ikiwa itathibitika kuna hatari ya uvunjifu wa amani na usalama au mtu huyo ametenda kosa la jinai. Tumetoa maelekezo yanayofafanua matumizi mazuri ya sheria hii kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote pamoja na mafunzo kuhusu mipaka na majukumu ya kazi zao, hivyo kwa sasa sheria inajitosheleza, ila tutaendelea kusisitiza matumizi sahihi ya sheria husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa kuwa Serikali inakiri kwamba kuna baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamekuwa wakiitumia sheria hii vibaya.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuleta mabadiliko ya Sheria hii hapa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamewasimamisha baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ambao wamechaguliwa kihalali kwa muda mrefu na kukaimisha nafasi hizo kwa watu wengine, jambo ambalo linakwenda kinyume kabisa na sheria, kanuni na taratibu bora za uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Je, Serikali inatoa kauli gani dhidi ya jambo hili? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama

nilivyosema awali, hivi sasa sheria hii inajitosheleza. Changamoto kubwa ni matumizi ya ile sheria. Ndiyo maana tumesema kwamba ofisi yetu na kupitia Waziri wangu hapa, alitisha kikao maalum cha kupeana maelekezo ya jinsi ya kutekeleza vizuri sheria hii. Lengo kubwa ni kwamba makusudio ya sheria hii yaweze kufikiwa kama vilivyo.

Kwa hiyo ukiangalia, muktadha wa sheria yenyewe haina matatizo isipokuwa katika *implementation* ya sheria. Ndiyo maana tumesema kwamba maelekezo maalum yametolewa na sasa hivi hatutarajii kwamba kama kutakuwa na mapungufu yoyote mara baada ya maelekezo hayo ambapo ofisi yetu imefanya kazi kubwa sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Wenyeviti wa Vijiji kusimamishwa na baadhi ya Wakuu wa Wilaya, naomba ikiwezekana tupate taarifa ya eneo *specific*, liko wapi, halafu tuangalie kesi gani ambayo imejitokeza katika eneo husika tuweze kuangalia tatizo gani limesababisha kusimamishwa. Hata hivyo tuna imani kwamba Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya jukumu lao kubwa ni kuhakikisha kwamba utaratibu wote unasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakati mwingine inawezekana baadhi ya vijiji kuna baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji huenda wameuza ardhi ya kijiji au kufanya jambo lingine ambalo lilikuwa tofauti na utaratibu, ndiyo maana utakuta Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anafanya taratibu za kisheria. Lakini kama kuna jambo ambalo limekiukwa basi naomba ofisi yetu tupate taarifa hizo tuweze kulifanyia kazi kwa misingi ya kisheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud na ...Aah! Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Waziri anazungumza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Sheria hii ya Mikoa inatoa mamlaka kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuweza kumkamata mtu katika mazingira ambayo wanaamini kwamba mtu huyo ama anatenda kosa la jinai, ama kwa ufahamu wao ametenda kosa la jina, ama anafanya kitendo chochote kinachovunja amani na utulivu, ama anaona mtu huyu anatarajia kutenda au kuhatarisha amani, hivyo ndio tafsiri ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hili wamepewa hawa kwa sababu ya ku-*maintain law and order*. Utaiona leo hii inapokuwa ipo kinyume na wewe kama mbaya, lakini ikiwa inakusaidi katika wakati ambapo amani yako, haki yako au jinai dhidi yako inataka kutokea, mkuu huyu anapochukua zile hatua ndipo utakapoonna msingi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama, mamlaka haya yanatokana na nguvu kubwa waliyonayo katika msingi wa Katiba. Halikadhalika, mtu yoyote anayo haki ya kuomba mtu mwingine ambae anaweza kutenda kosa la jinai dhidi ya mtu fulani au ya watu fulani kuomba wakamatwe.

Kwa hiyo haki hii sio tu wamepewa hawa peke yao, ukisoma vizuri sheria nyingine tulizonazo pia zinakupa wewe nguvu ya kusema wewe hapana, Simbachawene mimi naona huyu anatarajia au anahatarisha amani au anataka kutenda kosa, akakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa cha msingi ni pale tu ambapo inapaswa kutumika kwa kuzingatia sheria. Mtu huyo awe ana mtarajio ya kupelekwa mahakamani *immediately* baada ya kukamatwa na baada ya muda ule kupita. Isikamatwe kwa ajili ya *show off* tu, asikamatwe mtu kwa ajili ya ku-*show*, asikamatwe kwa ajili tu ya kuonesha kwamba wewe una madaraka. Lazima akamatwe mtu huyo kama kweli kitendo chake kinahatarisha amani na utulivu. Hapa ndipo ninapotaka nisisitize kwamba Wakuu wetu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kutumia sheria hii, wawe

makini na kuhakikisha kwamba wanaitumia kama vile sheria inavyotaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa maelezo hayo inatosha Mheshimiwa Masoud au kuna la ziada?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna la ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa Wakuu wa Wilaya wanatumia madaraka vibaya ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini ambapo amemsimamisha kazi Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) wa Mtaa wa Mlimwa Kusini, kwa hila na ujanja na mpango wa kutengeneza. Jambo ambalo inapelekea kunakuwa na malalamiko makubwa miongoni mwa wananchi wa Mtaa wa Mlimwa Kusini ambapo ni Kiongozi wao wamemchagua na wanampenda. Je, tabia hii mbaya ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, ni lini ataacha kusimamisha watu kiholela? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *scenario* anayoizungumzia *is a very specific scenario* na pengine tungeweza kuisikiliza chanzo chake, imekuwaje, ilitokeaje. Si rahisi kwa muda huu kuweza kufanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote humu Wabunge tunafahamu, namna ambavyo Wenyevidi wetu wa Vijiji na Mitaa wanavyouza maeneo, wanavyoharibu mali za umma, wanavyochezea mali za umma. Kwa hiyo, kuna mambo mengi yanayotokea huko; na sisi kama nchi tumewapa madaraka hawa watu wawakilishe mamlaka ili kuhakikisha kwamba maslahi ya umma inalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kutekeleza majukumu haya, mazingira hayawezi yakafanana, yanatofautiana kutoka sehemu moja na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tunayosimamia, Utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, tupo tayari kupokea jambo lolote mahsusi na kulishughulikia namna ilivyo. Lakini si kweli kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawa wanafanya mambo ya ovyo. Wanafanya mambo ambayo yanasababisha tunakuwa na amani katika nchi hii na tunawapongeza wanafanya mambo haya katika mazingira ambayo ni tata, kwa sababu pia kuna siasa ndani, kuna mambo mengi; tuwasaidie lakini pia tulete mambo ambayo yamekwenda sio sawa ili tuweze kuyashughulikia kulingana na yalivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Ali Mangungu swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Jamal Kassim.

Na. 401

### **Kuajiri Walimu Waliohitimu Mwaka 2015**

**MHE. JAMAL KASSIM ALI (K.n.y MHE. ISSA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

Serikali ilitoa mafunzo kwa walimu ambao walihitimu mwaka 2015 lakini walimu hao hawajaweza kuajiriwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri walimu hao walioachwa ingawa kiuhalisi bado kuna uhaba mkubwa wa walimu katika shule za sekondari hasa vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais –TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017 Serikali imeajiri walimu 3,081 wa masomo ya sayansi na hisabati ambao wameshapangwa na kuripoti katika shule walizopangiwa nchi nzima. Ajira hizo zimetolewa kwa walimu waliohitimu mafunzo mwaka 2015 na mwaka 2016. Mpango wa Serikali ulikuwa ni kuajiri walimu 4,129. Hata hivyo, walimu 1,048 wa masomo hayo ya sayansi na hisabati hawakupatikana katika soko wakati wa uhakiki wa vyeti uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kuajiri watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo walimu katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jamal swali la nyongeza.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Issa Mangungu na wananchi wa Mbagala nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali katika mwaka unaokuja 2017/2018 wamepanga kutoa ajira za walimu. Je, ni walimu kiasi gani ambao wamepangwa kwenda kuajiriwa katika Wilaya ya Temeke hususan katika jimbo la Mbagala, katika shule za sekondari za Kingugi, Mbande, Charambe, Toangoma na Mbagala Kuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali katika mwaka huu imeajiri walimu wengi wapya, je, ni lini sasa Serikali itawapatia stahiki zao walimu hawa wapya na pia kuwapatia makazi ili kuwawesha kufanya kazi yao kwa ufanisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali kwamba tuna mpango wa kuajiri walimu, lakini katika hili sasa hivi tunafaya vile vile na tathmini

ya idadi ya walimu ambao wametoka katika *system* ya kiserikali mara baada ya vyeti *fake*. Kwa hiyo, tutaleta taarifa rasmi hapa baadaye kwamba idadi ya walimu ambao wamekutana na vyeti *fake* ambapo hivi sasa kuna *deficit* ambayo itakuwepo, lakini na idadi ya walimu wapya. Kwa hiyo, tutaleta taarifa rasmi ya idadi ya walimu. Hata hivyo naomba nikuhakikishe Mheshimiwa Jamal kwamba kwa Mkoa wa Dar es salaam maeneo ya Temeke na mimi nafahamu sana Temeke ilivyogawanyika mpaka kwenda kule ndani maeneo ya Toangoma tutaangalia ni jinsi gani tutafanya ili maeneo hayo kama ambavyo umeainisha tuweze kuwapeleka walimu wa kutosha ili vijana wetu wanaokwenda kujiunga, waweze kupata elimu hiyo inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa pili wa swali lako nadhani Mheshimiwa Jamal, nimesahau kidogo kipengele cha pili.

**MWENYEKITI:** Haina shida hiyo imeshaeleweka Mheshimiwa kwa hapo, mwenyewe aliyeuliza swali ameshaelewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo, Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na swali la msingi kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema watoto wote wasome bure, katika jimbo la Kaliua shule ya msingi Ushokola walimu wanafundishia nje na walimu hawatoshi. Ni lini Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itaona hili tatizo la Kaliua kuongeza walimu wa shule za msingi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante; Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Bulembo, *Senior MP*, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bwana Bulembo bahati nzuri siku nne zilizopita nilikuwa na viongozi kutoka katika Wilaya ya Kaliua, walifika ofisini kwangu pale lakini ili kujadili ajenda za kimaendeleo. Ninasema *Senior MP* kwa sababu mwanzo alikuwepo na hivi sasa mnajua kazi zake kubwa anazozifanya katika nchi hii na juzi alikuwepo kule Mkoa wa Tabora nadhani ndio maana ameweza kufanya *verification* ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kikubwa zaidi nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge; nilikubaliana na viongozi waliotoka Kaliua kwamba nitafika Kaliua. Naomba nikuhakikishie kwamba nitatembelea shule ile ili kubaini mahitaji halisi. Hata hivyo Serikali tutaweka mpango, namna ya kufanya ili tuweze kujenga miundombinu na kuwapatia walimu ili vile vile wananchi wa eneo lile wapate fursa ya kusema tulitembelewa na mjumbe wa Kamati Kuu ambaye anasimamia suala zima la utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Vicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka, halafu Mheshimiwa Ulega.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa vile swali langu ni sawa sawa na hali halisi iliyoko Mbagala, ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba jimbo la Same Mashariki limekuwa na shida sana ya walimu, tuna kata moja ya Bwambo, shule ya Changuruwe imekuwa na walimu wawili tangu darasa la kwanza mpaka la saba kwa muda mrefu sana na kilio hiki hakijaweza kusikilizwa na kufanyiwa kazi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia ni lini atanipa walimu tuongeze hii shule ambayo wanabidii sana lakini kwa walimu wawili hata ungefanya nini hawawezi kutosheleza kusaidia wanafunzi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge nikupe pole katika hilo. Nilivyofika katika Mkoa wa Kilimanjaro, miongoni mwa Mikoa ambayo ina walimu wengi ni Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, nitumie fursa hii sasa kumuagiza Afisa Elimu wa Mkoa, haiwezekani walimu wote wakajazana Moshi Mjini, wakati wananchi wa Same hawana walimu. Nimuagize Afisa Elimu wa Mkoa wa Kilimanjaro, shule zinapofunguliwa ahakikishe shule ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha katika Halmashauri ya Same amepoleka walimu wa kutosha, la sivyo tutamuona kwamba hatoshi kusimamia eneo hilo la elimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, Mheshimiwa Ulega swali fupi kabisa la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kupata fursa hii. Kama ilivyoshida ya walimu katika jimbo la ndugu zangu wa Mbagala na sisi watu wa Mkuranga tunashida kubwa ya upungufu wa walimu. Serikali inanipa ahadi gani ya kuhakikisha kwamba upungufu ule wa walimu unapungua? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri naona ametoka huko tunaenda Mkuranga sasa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimuhakikishe Mheshimiwa Ulega, kama alivyokuwa makini kusimamia shughuli za maendeleo katika jimbo lake, naomba nimuhakikishe kwamba katika mchakato huu wa sasa wa kuelekea kuajiri walimu Mkuranga tutaipa kipaumbele, na nikijua kwamba jimbo lako lile limetawanyika sana, tutakupa kipaumbele ili elimu kwa wananchi wa Mkuranga iweze kupanda na hatimaye waweze kupata mafanikio mazuri ya Serikali yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda niongezee sehemu kidogo tu. Waheshimiwa Wabunge ni karibu maeneo mengi yana upungufu wa walimu na hasa kwenye shule zetu za msingi. Pamoja na jitihada za Serikali kuwapeleka walimu ambao wanaonekana wamezidi katika baadhi ya maeneo lakini baadhi ya shule bado walimu hao ni wachache, kwa sababu ya changamoto za miundombinu zilizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea mipango ya Halmashauri na vipaumbele vyao inasikitisha kuona wakati mwingine mipango hiyo, na kwa sababu utawala wa nchi hii unatoka chini kwenda juu na si juu kwenda chini na ndio maana bajeti inaanza kupangwa kutoka chini baadaye juu tunakuja kumaliza, tungelitegemea vipaumbele viwe nyumba za walimu na miundombinu kama hiyo inayotegemea kujenga mazingira bora ya watumishi hawa kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali la msingi inaonekana ni mazingira magumu ya kule milimani ya kule Same ndiyo maana walimu hawakai, hivyo ukijiuliza hakuna nyumba na hata walimu hawa wakifika uongozi tu wenyewe kuwapokeana kujenga mazingira mazuri ni vigumu sana, hawashughuliki nao, na ndiyo maana kuna upungufu.

Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, sisi ndio tunaoshiriki kwenye vikao vya maamuzi makubwa, sisi tunashiriki kwenye vikao ambavyo vinapanga mipango na bajeti. Tupange mipango hiyo inayotatua kero za nyumba za walimu ndipo tutakapoweza kuwa-*retain* walimu hawa katika shule zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa *clarification* Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Wizara ya Katiba na

Sheria, Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 402

### **Mahakama ya Wilaya ya Kasulu**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ni ya zamani sana, ni chakavu sana na wakati mwingine huduma hazitolewi kabisa.

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeitelekeza Wilaya ya Kasulu?

(b) Je, mahakama hiyo itajengwa lini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ni chakavu. Hata hivyo, mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa ni kujenga upya jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ambapo hadi sasa mkandarasi wa ujenzi huo ameshapatikana na anategemea kuingia makubaliano ya ujenzi huo mwishoni mwa mwezi huu wa Juni, 2017. Hivyo napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mahakama itaanza utetelezaji wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kasulu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri mafupi ya

Mheshimiwa Waziri Profesa Kabudi. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Mahakama hiyo tumeisubiri kwa muda mrefu na umekiri kwamba mkandarasi amepatikana, je mkandarasi huyo anaitwa nani? Na mkandarasi huyo atajenga kwa gharama gani, kwa maana kama amepatikana atakuwa anajulikana na gharama ya ujenzi inajulikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali dogo la pili; pale pale Kasulu kilomita kama 10 hivi kuna Mahakama ya mwanzo ya Heru Juu, na bahati nzuri mimi kule Heru Juu ndiko ninakozaliwa, Mahakama ile iliangukiwa na mti mwaka 2010 na bahati nzuri Mtendaji Mkuu wa Mahakama alifika pale akaiona. Je, hiyo Mahakama ya mwanzo ya Helujuu ni lini itakarabatiwa, maana haijengwi, inakarabatiwa, ili wananchi waendeleo kupata huduma za Mahakama ya Mwanzo katika Mahakama ile? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi ambaye atajenga Mahakama ya Wilaya ya Kasulu anaitwa *Morad Tanzania Ltd.* ambaye pia ndiye amejenga Mahakama ya Kibaha. Gharama ya ujenzi wa mahakama hiyo nitamuomba Mheshimwa Mbunge baadaye nimpe ili ajue ni kiasi gani. Hata hivyo haitazidi gharama ambayo imetumika kwa ile Mahakama ya Kibaha na kama umeona kitabu cha bajeti ya mwaka huu kule nyuma Mahakama ile ya Kibaha umeiona na ndivyo itakavyokuwa Mahakama ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Mwanzo ya Heru Juu, kijiji ambacho na mimi nimewahi kufika na nimekipenda sana, napenda nikuarifu kwamba Mahakama ya Mwanzo ya Heru Juu itaanza kujengwa katika mwaka wa 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante niende kule mwisho kabisa! Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Uchakavu katika Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ni sawa na hali ilivyo katika Mahakama ya Wilaya ya Mpanda. Jengo ni la kizamani, dogo na halikidhi mahitaji ya sasa ya Wilaya na Mkoa kwa ujumla. Ni lini Serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya Wilaya ya Mpanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu la mjumbe, niwe na hakika, Mbunge ni Kapufi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Mpanda imepangiwa kujengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kama ilivyo Mahakama ya Kasulu ni chakavu, lakini Wilaya ya Liwale ni Wilaya ambayo ina umri wa miaka 42 mpaka leo haina jengo la Mahakama. Jengo linalotumiwa ni lile jengo ambalo lilikuwa Mahakama ya Mwanzo ambalo sasa hivi limechakaa limefika mahali ambapo mafaili yanafunikwa na maturubai. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuijengea Liwale Mahakama ya Wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Liwale itajengwa mwaka 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mko wengi sana malizia kule mwisho, Mheshimiwa Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Kavuu na Mkoa mzima wa Katavi, kutokana na jografia yake imekaa kama umbo la pweza. Je, Serikali inafikiria nini katika Jimbo la Kavuu, Halmashauri ya Mpingwe kuanzisha Mahakama yenye hadhi ya Wilaya kutoka kwenye hadhi ya Mahakama ya Mwanzo ili kuwanusuru wananchi kwenda katika makao makuu ya Nyonga ambayo wanapita katikati ya mbuga na kuhatarisha maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yake nimeyasikia tutayafanyia kazi, na baada ya hapa namuomba tuonane katika ukumbi wa Bunge ili tuweze kuongea na nielewe hasa nini kifanyike kwa ajili ya eneo hilo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda unakwenda natamani niwapeni wote lakini haiwezekani, kwa hiyo, tuendelee na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni sasa aulize swali lake.

Na. 403

### **Kuwaongezea Posho Askari wa Jeshi la Wananchi**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Serikali imeandaa utaratibu wa kuliwezesha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kufanya shughuli zake kwa kuwapatia posho mbalimbali ikiwemo *ration allowance*.

Je, ni lini Serikali itaongeza posho hiyo iendane na maisha yalivyo sasa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inao utaratibu wa kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kufanya shughuli zake kwa kuwapatia maafisa na askari posho za aina mbalimbali ikiwemo *ration allowance*. Serikali imekuwa ikiboresha maslahi na stahiki mbalimbali kwa maafisa na askari kwa kuzingatia hali ya maisha ya wakati husika na uwezo wa Serikali kifedha kumudu kulipa stahiki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ration allowance* inalipwa kwa maafisa na askari wote. Serikali ilipandisha kiwango cha posho ya chakula (*ration allowance*) kwa nyakati tofauti. Kwa mfano, mwaka 2011 *ration allowance* ilikuwa shilingi 7,500, mwaka 2014 *ration allowance* ilipanda kufikia shilingi 8,500 na mwaka 2015 ilipandishwa kufikia shilingi 10,000, kiasi ambacho kinaendelea kutolewa hadi hivi sasa. Kwa hivyo, Serikali itaendelea kuboresha posho ya chakula na posho nyinginezo kadiri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Khatib Kai una swali lingine?

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri katika jibu la msingi kwamba askari wa jeshi sasa hivi wanalipwa posho ya shilingi 10,000 kwa siku hela ambayo kwa maisha ya sasa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itawaongezea askari hawa posho kutoka shilingi 10,000 angalau hadi 20,000 kwa siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jeshi letu la Tanzania limekuwa likipata sifa kitaifa na kimataifa kutokana na weledi na utendaji wake wa kazi, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Jeshi hili halitoi malalamiko kwa posho wanazolipwa, hasa ukizingatia kazi wanazozifanya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, ni kwamba posho zinaongezwa kadri ya uwezo wa Serikali unavyoruhusu. Katika hili nimetoa mifano, kwamba tulianza na shilingi 5,000 ikapanda mpaka shilingi 7,500 ikapanda mpaka shilingi 8,500 sasa ni shilingi 10,000; kwa hiyo, tutaendelea kuzipandisha posho hii kwa kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la pili kuhusu malalamiko unayoyazungumzia; nataka nikueleze Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwa kiwango kikubwa posho zinazotolewa sasa kwa askari na maafisa wetu zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa. Mimi nataka nikuhakikishie kwamba wengi wanafurahia posho hizi zinazotolewa. Kama nilivyosema hakuna kinachotosha, mara zote kutakuwa kunaupungufu tu. Kwa hiyo, kwa kadri uwezo utavyoruhusu tutaendelea kuwa tunazi-*review* kila mwaka posho zote kuangalia uwezekano wa kuzipandisha kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na posho za *ration allowance* kuwa ndogo lakini pia inasemekana kuna mpango wa kuzifuta posho hizi

ili askari wasipewe *cash* wawe wanakula *ration* makambini. Je, ni kweli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga taifa majibu kwa ufupi tu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya *ration* tutambue madhumuni yake kwanza, madhumuni ya posho ya *ration* ni kumlisha askari na maafisa ili waweze kutekeleza majukumu yao. Sasa wako wale ambao wako kwenye makambi, wako wale ambao wanalazimika kula ili waweze kutekeleza majukumu yao, hao kuna wazabuni katika Makambi yote wanaopewa fedha hizo ili waweze kuwalisha, lakini wale ambao majukumu yao hayapo katika Kambi wao wanapewa fedha zao taslimu ili waweze kutumia wanavyoamua wao wenyewe.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tumalizie na Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nina swali moja tu; kwa kuwa Serikali imerejesha Kambi ya JKT Mpwapwa na kwa kuwa vijana wengi wa Wilaya ya Mpwapwa wanataka kujiunga na JKT Mpwapwa, je, ni taratibu gani watumie ili waweze kujiunga na ile kambi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba JKT ina azma ya kufungua makambi mapya katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mpwapwa, na utaratibu utakaotumika wa kujiunga ni ule ule ambao unatumia sasa kwamba wakati ukifika JKT itatoa nafasi za vijana wa kujitolea kuomba ili kuingia katika makambi haya mapya. Kwa pale Mpwapwa haitokuwa vijana wa Mpwapwa peke yao, itakuwa kwa nchi nzima, tutazigawa nafasi kama tunavyozigawa sasa kupitia Wilayani na Mikoani na hatimaye vijana watajiunga na Kambi

hiyo ya Mpwapwa itakapokuwa tayari kutoa mafunzo. Vile vile kwa siku zijazo tukiwa tayari kambi hiyo pia itatumika kwa vijana kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Mwinyi Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 404

### **Manufaa ya Mgodhi wa Kabanga Nickel kwa Wananchi**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Katika maeneo ya Bugarama, Wilaya Ngara kuna Mgodhi wa Kabanga Nickel uliodumu kwa miaka 30 sasa na kampuni mbalimbali zimekuwa zikiendesha shughuli zake kwenye mgodi huo na kuondoka tangu mwaka 1970 wakidai kuwa wanafanya utafiti huku bei ya Nickel katika soko la dunia akishuka.

Je, wananchi wa Ngara hususan maeneo ya Bugarama watanufaika na uwepo wa rasilimali hiyo iliyopo kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya Kabanga Nickel inamiliki mradi wa utafutaji madini ya Nickel katika eneo la Kabanga chini ya leseni namba moja ya mwaka 2009 iliyotolewa tarehe 02 Mei, 2009. Kampuni hiyo inaendelea kufanya utafiti wa kina ili kubaini kama mradi huo unaweza kuendelezwa kwa faida zaidi. Hivi karibuni bei ya madini ya Nickel ilishuka ghafla kutoka dola za Marekani 11 kwa *pound* mwaka 2010 hadi dola za Marekani 4 kwa *pound* kwa

mwaka 2014. Kutokana na hali hiyo, kampuni inatarajia kuendeleza shughuli za uchimbaji mara baada ya bei hiyo kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 4 Aprili, 2017 bado bei ya Nickel katika soko la Dunia ilikuwa dola 4.45 kwa *pound* ikilinganishwa na bei ya dola 11 mwaka 2009 mradi ulipokuwa ukifanyiwa upembuzi yakinifu. Mgodi unatarajiwa kutoa ajira 1,455 wakati ujenzi ukiendelea na wakati wa uzalishaji itaajiri Watanzania 800. Mradi utakapoanza kupata faida mambo yatakayofanya wananchi wanufaika ni pamoja na kulipa *service levy*, kutoa huduma za Maendeleo pamoja na ajira hapa nchini. Kadhalika tutajenga miundombinu kwa ajili ya kusaidia jamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Kabanga Nickel una mda mrefu sana, kama nilivyouliza kwenye swali langu la msingi, tangu mwaka 1970 na wachimbaji walianza tangu mwaka 1973. Wananchi wa Ngara tulikuwa tukiona ndege za wazungu zikija na kuondoka wakidai kwamba wanapeleka *sample* na hawarudi tena, isije ikawa kama makinikia. Je, huu mgodi wa Kabanga Nickel utanza lini rasmi ili wananchi wa Ngara na Serikali kwa ujumla tuweze kunufaika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Sheria na mauziano ya Makampuni inataka mnunuzi na muuzaji kulipa kodi ya Serikali. Mgodi wa Kabanga Nickel umekwisha kubadilisha wamiliki zaidi ya wanne. Je, Serikali Kuu na Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Ngara imenufaika vipi na huo umiliki wa kubadilisha wamiliki kila mara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa

Semguruka kwa jinsi anavyofuatilia maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Kagera pamoja na wananchi wa Ngara kwa ujumla wake. Nampongeza pia anavyoshirikiana na Waheshimiwa Wabunge wengine majirani wa Biharamulo, Ngara na wengine, hongera sana Mheshimiwa Semuguruka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali la kwanza. Ni kweli kabisa huu mradi umeanza tangu mwaka 2009, kwa kweli si miaka ya 1970 iliyopita. Hata hivyo niseme tu kwamba kazi inayofanyika sasa hivi ni kukamilisha upembuzi yakinifu, na natarajia kufungua mgodi mara tu baada ya bei ya nickel kuimarika. Hata hivyo tumempa muda wa mwaka asipofanya hivyo eneo hilo tutalichukua tutawamilikisha wawekezaji wengine wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa yatakayopatikana mgodi huo ukifunguliwa ni pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wengi wa Bugarama na Kanyenyi, kadhalika watalipa mafao ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na uhamishaji, Sheria za Kodi zinamtaka mmiliki yeyote akihamisha au kuuza hisa au leseni yake anatakiwa kulipa *capital gain* ya asilimia 10 na kwa upande wa Sheria ya Madini kifungu cha 9(1) cha mwaka 2010 kinataka mmiliki akianza kuhamisha analipa dola 3,000. Kwa hiyo, atakapofika hatua hiyo Mheshimiwa Semuguruka haya mafao ya Serikali yataingia. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira kule Mbeya umekuwa *static* kwa muda mrefu sana na Mgodi huu mimi naweza nikasema sasa wananchi wa

Mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani tumekuwa yatima. Nini tamko la Serikali, nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa swali fupi la Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nae kwanza Mwanjelwa hongera sana. Hata mwaka jana amehangaika sana kuhakikisha kwamba mgodi huu unafanya kazi. Nimpe taarifa tu, mwaka 2017/2018 Shirika la *STAMICO* limeanza uchimbaji, na hivi sasa limeishachimba tani 500 ya mkaa ya mawe na wataendelea na uchimbaji. Kadhalika kuna makampuni mawili yataingia ubia ili kuwezesha uchimbaji kuwa wa manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mgodi wa Kiwira umeishaanza shughuli na kufika mwaka 2018/2019 tunatarajia tani 100,000 zitakuwa zimezalishwa katika mgodi ule. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, mkiuliza kwa ufupi mnaweza kupata wengi lakini mnauliza marefu Oran Njeza na Mheshimiwa Tundu Lissu wa mwisho.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. Katika milima ya *Panda Hill* Wilaya ya Mbeya kuna madini ya *niobium* ambayo yanatarajiwa kuchimbwa hivi karibuni. Je, Serikali imechukua hatua gani na tahadhari gani ili yasije yakatokea yale yaliyotokea kwenye *Acacia* na *Barrick Gold Cooperation*?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana, Mgodi wa *Niobium* hapa Tanzania ni mgodi pekee ambao unapatikana katika eneo la Songwe. Kinachofanyika sasa ni majadiliano kati ya Magereza ambako eneo la mgodi litachukua ili kuona kama kutakuwa na *re-settlement* na majadiliano kama yakikamilika.

Kwa hiyo, nimpe taarifa tu, taratibu zinazofanyika sasa ni majadiliano kati ya Kampuni pamoja na Magereza, taratibu zikishakamilika basi uwekezaji utaendelea.

**MWENYEKITI:** Tumalizie na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na huo mgodi unaopangwa kujengwa wa Kabanga Nickel, Serikali itapata asilimia ngapi kama mrahaba kwa mujibu wa Sheria za Tanzania? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge mashuhuri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimueleza Mheshimiwa Tundu Lissu; Mrabaha unaotozwa kwa sasa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 madini yote ya ujenzi ikiwa pamoja na madini ya chumu na *iron* ambayo ni nickel ni asilimia tatu, lakini madini mengine ya dhahabu ni asilimia nne na madini mengine ni asilimia moja, madini ya almasi ni asilimia tano. Kwa hiyo, asilimia tutakazopata kutoka kwenye mgodi ni pamoja na hiyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang sasa aulize swali lake.

Na. 405

### **Kuondoa *Tariff* katika Mradi wa Maji wa Katesh**

**MHE. DKT. MARY MICHAEL NAGU** aliuliza:-

Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Maji wa Katesh,

hata hivyo mradi huo bado haujaweza kuwanufaisha wananchi kwa sababu ya gharama kubwa za umeme zinazosababisha pampu za maji kufanya kazi kwa muda mfupi tu.

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza au kuondoa kabisa *tariff* zilizopo ili gharama ya umeme iwe chini kidogo na kusaidia kusambaza maji kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mradi kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu inasambaza umeme vijijini kwa kuweka kipaumbele kwenye huduma za jamiii ikiwemo Mradi wa Maji wa Katesh. Lengo la Mradi huu ni kuwezesha huduma hiyo kupatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kuendesha mtambo wa kusukuma maji kwa kutumia umeme ziko chini ukilinganisha na gharama ya kutumia mafuta ya dizeli. Gharama ya kuzalisha *unit* moja ya umeme ni shilingi 292 wakati gharama za kufua umeme kwa kutumia mafuta shilingi 450 hadi shilingi 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, gharama ya kuunganisha umeme kupitia Mradi wa *REA* ni shilingi 27,000 tu ambayo ni *VAT* kwa ajili ya Serikali kwa sababu Serikali imegharamia kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gharama za umeme ni nafuu kuliko gharama za mafuta, tunashauri Halmashauri husika itenge pesa kwa ajili ya kuunganisha umeme katika mitambo ya maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali kwa ufupi lakini kama tunavyotegemea, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba niulize maswali mawili madogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya Mji wa Katesh yanaendeshwa kwa umeme wa *grid* lakini bado gharama ni kubwa. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie kwamba atatuma wataalam kuona kwa nini gharama ile iko juu ili watu wa Katesh waweze kupata maji kwa sababu kwa sasa hivi wanapata mara katika wiki na ni hatari kwa mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine dogo la pili ni kwamba; ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri huyu kwa kuona umuhimu wa vijiji kuwa na umeme ili wanapochimba visima waweze kusukuma maji kwa nguvu ya umeme. Hata hivyo Wilaya yetu ni moja ya Wilaya ambayo imepata vijiji vichache. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunihakikishia kwamba vijiji vyetu vingi sasa vitapata umeme wa *REA* na kwamba Mkoa wa Manyara ataanzia na Wilaya ya Hanang? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuhusiana na kutuma wataalam wakaangalie kama bei ni halisi, Mheshimiwa Mary Nagu kwanza nakupongeza sana kesho wataalam watakwenda kwenye *site* wataangalia ili wajiridhishe kama ni sahihi, nitawaagiza waende washirikiane na watu wako walioko kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijiji ambavyo ameseme Mheshimiwa Mary Nagu, kwanza nakupongeza Mheshimiwa Mary Nagu, wakati wakati wa bajeti yetu ulitupatia vijiji vyako 44 ili tuvipelekee umeme. Sasa napenda kuwahakikishia wananchi wa Hanang kwamba vijiji vyako vyote 44 ulivyotupatia ikiwepo kijiji cha Gocho, kijiji cha

Kaltaki, kijiji cha Gawindu pamoja na Kateto na vitengoji vyake vyote vitapata umeme Mheshimiwa Nagu.

**MWENYEKITI:** Ahasante sana, tunaendela na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla swali langu halijajibiwa ninaomba nifanye marekebisho madogo. Tulisema wananchi wa Jimbo la Ndanda hawako tayari kabisa kuona mfumo wa uuzaji wa korosho Stakabadhi Ghalani ukiendelea, iwapo changamoto zilizojitokeza mwaka huu hazitarekebisha kabla hatujaingia msimu ujao, ahsante.

Na. 406

### **Mfumo wa Stakabadhi Ghalani Kuondolewa**

**MHE. CECIL DAVID MWAMBE** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Ndanda hawako tayari kabisa kuona mfumo wa uuzaji korosho wa stakabadhi ghalani ukiendelea.

Je, Serikali chini ya kauli mbiu "Hapa Kazi Tu" ipo tayari kuondoa kabisa mfumo huo ambao ni kandamizi na hauendani na gharama za uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijajibu lazima niseme kwamba kama Mheshimiwa Cecil Mwambe asingerekebisha swali ningeshangaa sana kama swali la aina hiyo lingetoka kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni utaratibu ulioanzishwa kisheria wa namna ya uuzaji wa mazao kwenye maghala kwa wakulima kukusanyia mazao yao kupitia chama chake cha misingi na mazao hayo kupelekwa katika ghala kuu ambapo ubora wa zao huhakikiwa kulingana na Sheria ya Maghala na mkulima kupewa stakabadhi ambayo hutumika kama dhamana ikiwa mkulima atahitaji mkopo wakati akisubiri mazao yake kuuzwa sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu una mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na wakulima kupata uhakika wa soko, kupanda kwa bei ya zao la korosho ambapo wakulima waliuza korosho zao kwa bei ya ushindani sokoni kwa wastani wa shilingi 2,500 kwa kilo na bei ya juu kufikia hadi shilingi 4,000 kwa kilo katika msimu huu wa 2016/2017. Aidha, mfumo huu pia umewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la korosho ambapo uzalishaji uliongezeka kutoka tani 155,244.64 katika msimu wa 2015/2016 hadi kufikia tani 264,887.52 kwa msimu wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ya mfumo huu ni kwamba wakulima wa korosho kwa sasa wanapata bei za juu kutokana na wakulima kupata bei sokoni kwa utaratibu wa kuvumbua (*pride discovery*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo, Serikali haiko tayari kwa sasa kuondoa mfumo wa Stakabadhi Ghalani katika uuzaji wa zao la korosho nchini kutokana na mafanikio hayo, badala yake Serikali itaendelea kusimamia na kuboresha mfumo huu na kuwahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa korosho zenye ubora ili kujiongezea kipato chao na nchi kwa ujumla.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na nitakuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto zilizojitokeza kwenye msimu wa korosho mwaka wa jana ni

pamoja na wizi uliofanyika katika maghala ya YURAPyaliyoko Masasi kwa kushirikisha wamiliki wa ghala lakini pamoja na viongozi wa mkoa walibariki jambo hili; na sasa hivi kuna kesi zinaendelea mahakamani kwa ajili ya kuweza kupata haki ya wakulima wale. Sasa tunataka kufahamu Serikali haioni haja ya kuwalipa wakulima pesa zao, kwa sababu walikuwa wanatoa michango kwenye mfuko wa kuendeleza zao la korosho wakati ninyi mnahangaika na wale wezi wenu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sasa hivi tunaelekea kwenye msimu wa kilimo na wananchi wanaendelea kutayarisha mashamba yao kwa ajili ya msimu wa korosho ujao. Hata hivyo kumekuwa na sintofahamu kubwa sana kuhusiana na pembejeo baada ya Serikali kutangaza kwamba itapeleka pembejeo za bure. Sasa tunataka kufahamu, ni lini pembejeo zitawafikia kwa asilimia 100 ili waweze kutayarisha mashamba yao, kwa sababu wanategemea zinatolewa na Serikali tena kwa bure? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali yake ningependa kusema kwamba zao la korosho ni moja kati ya mazao ambayo yamefanikiwa sana katika miaka ya karibuni. Mwaka huu korosho ndiyo imeongoza kwa kuiingizia nchi yetu fedha za kigeni kati ya mazao yote, imeipiku tumbaku. Vilevile katika msimu huu Serikali imefanikiwa kuwapatia wananchi wa mikoa inayolima korosho shilingi bilioni 800. Kwa hiyo, tunapozungumza korosho tunazungumza mafanikio makubwa sana ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu utaratibu wa Stakabadhi Ghalani tunaelekea sasa kwenye mazao mengine hususan Kahawa, lakini vilevile na mazao ya jamii ya mikunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maswali yake, ni kweli kwamba kuna mapungufu yametokea ikiwa ni pamoja na mapunjo ya fedha za wakulima. Kama mnavyofahamu, tayari kuna watumishi wa *MAMCU* wamepelekwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka ya kuhujumu uchumi. Vilevile katika fedha ambazo zimepotea tayari Serikali imesha-*recover* shilingi bilioni 1.5 na hizo zitaenda kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tani 9,000 za *sulfur* tayari zimeishaingia nchini na *sulfur* hiyo inagaiwa bure na iko njiani kuelekea kwenye mikoa inayolima korosho ili wananchi waweze kugawiwa, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda unaenda, tunamalizia na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 407

### Mitihani ya Taifa

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Mitihani ya Taifa kidato cha nne na sita hufanyika kwa pamoja kwa wanafunzi wa Tanzania Bara na Visiwani.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia mitaala na vitabu vya aina moja ili kuwapa wanafunzi wa Zanzibar fursa ya kujisomea na kufanya vizuri katika mitihani yao?

(b) Kwa kuwa mitaala na vitabu vya elimu ya awali na ya msingi kwa upande wa Zanzibar ni tofauti na Tanzania Bara, je, kwa nini Zanzibar wasiruhusiwe kutunga mitihani ya Taifa tofauti na Bara kwa kidato cha nne na sita, na mitihani hiyo ikapata hadhi sawa na ile inayotungwa Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala na vitabu vinavyotumika kufundishia na kujifunzia kwenye ngazi ya elimu ya sekondari (kidato cha kwanza hadi cha sita) kwa Tanzania Bara na Zanzibar ni vya aina moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mitaala na vitabu vinavyotumika katika ngazi ya elimu ya sekondari kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ni vya aina moja, Sheria ya Bunge namba 21 ya mwaka 1973 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 inalipa mamlaka Baraza la Mitihani la Tanzania ya kuendesha mitihani ya Taifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa kuzingatia kuwa mitaala na vitabu vya elimu ya awali na msingi vinavyotumika kwa upande wa Zanzibar ni tofauti na vinavyotumika Tanzania Bara, mitihani ya elimu ya awali na msingi kwa upande huo huendeshwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar.

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amekiri kuwa mitaala na vitabu vya elimu ya awali na msingi vinavyotumika upande wa Zanzibar ni tofauti na vya Bara.

Je, haoni kuwa kitendo hicho kinafifisha na kudhoofisha uwezo wa wanafunzi ambao wanaanza mitaala mipya badala ya kuendeleza ile waliyokuwa nayo na kusababisha wanafunzi kutoka Zanzibar kutofaulu vizuri mitihani yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar huendesha mitihani ya elimu ya awali na msingi Zanzibar, na kwa kuwa Baraza la Mitihani Zanzibar lipo, Serikali haioni kuwa ni wakati muhimu sasa iruhusu mitihani ya kidato cha nne na cha sita ikatungwa na kusahihishwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar na kupewa hadhi sawa ya Kitaifa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, kwa kuwa vitabu katika eneo hili la mafunzo katika elimu ya awali na msingi vimekuwa vikitungwa upande wa Zanzibar, basi kwa kushirikiana imeonekana kwamba ni vyema wao wenyewe kuendelea kutunga hiyo mitihani. Hata hivyo tuelewe kwamba suala la Baraza la Mitihani ni suala ambalo lipo katika mambo ya Muungano katika jedwali la kwanza namba 16.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo pale inapotokea kwamba kuna haja ya kufanya marekebisho ina maana ni suala la Kikatiba ambalo inabidi kufuata taratibu za Kikatiba katika kupata marekebisho kama hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali la msingi linahusiana na kutokuwa na usawa katika suala la mitihani naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa na huku Bara kuna tatizo kubwa sana kwamba kuna wanafunzi wa sayansi wana maabara nzuri sana lakini wengine hawana maabara lakini mitihani inakuja sawa. Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuhakikisha kwamba shule zote zinakuwa na maabara ili

wanapotungiwa mtihani wawe sasa wana usawa katika mitihani hiyo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale inapokuwa kwamba wengine wana fursa za kujifunzia zilizo kamili tofauti na wenzao na wakapata mtihani unaofanana si jambo jema ndiyo maana marekebisho yanafanyika. Jambo hilo kwa kweli haliko katika elimu tu, na hata katika masuala ya maji nimesikia Waheshimiwa Wabunge wakisema kwamba vijijini hakuna maji, mjini kuna maji na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inatoa fursa na usawa katika maeneo yote kulingana na mahitaji ya wananchi wake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu halafu Mheshimiwa Saada Mkuya.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu ningependa pia kutoa ufafanuzi kwamba utaratibu ulioko kwa sasa kwa shule ambazo hazina maabara lakini kuna wanafunzi wanafanya masomo ya sayansi, wanakuwa na mtihani tofauti na hawalazimishwi kufanya *practical*. Kwa hiyo kuna kitu ambacho kinaitwa *alternative to practical*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango wa Serikali kama ambavyo tumekwisha eleza katika swali ambalo lilikuwa limeulizwa hapo awali ni kwamba tunataka kuhakikisha kwamba shule zote zina maabara na zinakuwa na vifaa ili hatimaye hii *alternative to practical* ambayo imekuwa ikitolewa isiendeleo kuwepo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya tumalizie.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwakatika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba hii Bodi ya Baraza la Mitihani ni suala la Muungano katika Katiba imo katika nyongeza. Sasa nataka tu kumuuliza, hivi kuna wawakilishi wangapi kutoka Zanzibar katika Bodi ya Baraza la Mitihani na kwamba kama tunaona idadi hiyo inakidhi matakwa na haja ya wanafunzi kutoka Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu ni kwamba shughuli zote zinazofanyika zinazohusu masuala ya Muungano yanashirikishwa kikamilifu kwa pande zote mbili kwa idadi ni ngapi, kwa mujibu wa taratibu za Kibunge nadhani sitaweza kumpa hiyo namba kwa sasa hivi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu wa maswali umefikia mwisho, tuna matangazo kwanza ya wageni ambao wametufikia Bungeni kwa siku hii ya leo.

Tuna wageni 55 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kilichopo Mkoani Dodoma.

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliokuja kututembelea katika Bunge. Wanafunzi 90 na walimu kutoka shule ya sekondari Kaloleni iliyoko Mkoani Arusha. Lakini pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde; ni kijana Emmanuel Mathias maarufu MC Piliipili pamoja na mama yake mzazi na timu yake nzima. Kijana huyu wa Dodoma...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba tutulizane, naona mmeanza mapema kuongea jamani. Kijana huyu ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Mavunde

pamoja na mama yake mzazi na timu yake ameweza kuajiri vijana zaidi ya kumi, na pia lishinda tuzo ya *MC bora*. (*Makofi*)

Wageni wa mwisho ni Mheshimiwa Daniel Mtuka Mbunge wa Manyoni Mashariki; huyu ana ugeni wa familia yake, mke wake na watoto wake. (*Makofi*)

Katibu, tuendeleo.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa Kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu kama kawaida. Tutaanza na Mheshimiwa Mbatia na baada tutaendelea na Mheshimiwa Maida, Mheshimiwa Ezekiel na Mheshimiwa Jamal baadaye wajiandae.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyoko mbele yetu imeingia katika migogoro mingi tu, hii bajeti ya mwaka huu. Kwanza nianze na suala la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1633 Kanisa Katoliki lilimdhaliisha na akafungwa mwanasayansi mmoja anaitwa Galileo kwa sababu ya kwamba alisema dunia inazunguka jua. Baada ya miaka 350 Vatican tarehe 30 mwezi wa kumi siku ya Ijumaa mwaka 1992 waliomba dunia radhi na

walimuomba mwanasayansi huyu radhi, kwa sababu ni mfumo, uwajibikaji wa pamoja. Zaidi ya miaka 350 Galileo aliombwa radhi na Vatican. Sioni kwa nini tunaona aibu Serikali kuomba radhi Watanzania kuhusu suala la madini, kwa sababu ukiangalia tangu mwaka 1994 mpaka leo hii sheria na mikataba ni uwajibikaji wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukasema kwa sababu Serikali ilikuwani ya mwaka 1995 ni tofauti na Bunge hili, hata Bunge la 2015 watu walifukuzwa Bungeni huku kwenye masuala ya Sheria za Gesi pamoja na Mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushabikia tu hapa ndani; mwaka 2002 nilikwenda Harare, tulikuwa Zimbabwe, kwenye mgogoro huu huu wa mapambano ya kiuchumi. Vita vya kiuchumi ni vibaya sana, kweli kweli! lakini lazima tuwe wakweli. Wakati wa malumbano wakaanza kusema kwamba kuna watu wengine wanaitwa wametumwa na wazungu, wengine wamefanywa nini, leo hii Zimbabwe haina hata sarafu yake, Zimbabwe imeangamia kabisa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vita hii; na nipende kuweka wazi Kambi ya Upinzani hakuna Mbunge hata mmoja kutoka Kambi ya Upinzani anayepinga wizi wa dhahabu ya Taifa la Tanzania, hayupo. Tunaangalia maslahi mapana ya mama Tanzania na msimamo wa Kambi ya Upinzani, wezi, wizi wa rasilimali za Taifa tuzishughulikie sote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yakifikiwa lazima tukubali historia tulitoka wapi, tunajifunza kwa historia na kwa kuwa sasa Serikali iliyoko madarakani imelitambua hilo, tuko tayari kabisa kabisa kushirikiana kwa hili. Tuko tayari kabisa kabisa kupambana vita hivi endapo tutaacha kuwa na propaganda za kisiasa ambazo hazilisaidii Taifa la Tanzania. Tanzania ni yetu sote, Tanzania si mali ya kikundi cha watu wachache, tubishane kwa hoja, lakini yale mambo ya msingi Mheshimiwa Waziri yenye maslahi mapana kwa Tanzania tuyazingatie sote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo leo hii tutarudi kwenye makosa yale yale ya mwaka 1997, 1998 na mwaka 1997 nilikuwa kwenye Bunge hili, mwaka 1998 nilikuwa kwenye Bunge hili, sheria zilivyoletwa wengine wakabaguliwa tutarudi *back to square one*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme na nirudie tena na Watanzania watusikie vizuri kabisa, mapambano haya tuliyaanzisha na kwa kuwa wenzetu mlio wengi mmekubaliana na sisi, tuko tayari kuungana na nyie kwa sauti moja endapo tutaacha propaganda na tuwe tayari kushugulika kweli kweli tushirikishane kweli kweli kwa maslahi mapana ya Tanzania. Si mtu yeyote ajitokeze aseme kwamba hili ni langu, hili ni langu, kuna msaliti, kuna huyu, hapana! Tunatahadharisha tu *and it's better to be pro-active rather than being reactive*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tukiangamia, tunaangamia sisi sote, Watanzania wanaoumia wanaumia wote, watoto wanaokosa huduma wanakosa wote. Waliouwawa migodini haikuchagua huyu ni wa CCM huyu ni wa Upinzani, huyu ni wa nani, tuliumia sisi sote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo vita hivi vituunganishe kama Taifa la Tanzania lakini tuwe wakweli wa dhati kabisa tushirikiane, tuungane kwa pamoja, tutavusha Taifa la Tanzania. Wengine wakionekana wasaliti, wengine hapana ni wa kudandia, wengine ndiyo wenye akili zaidi kuliko wengine tunaliangamiza Taifa la Tanzania, tutarudi kama mambo ya Zimbabwe, tusiruhusu masuala ya Zimbabwe yaje Tanzania na Bara la Afrika unaona tunavyochezewa. Tuanze kufikiria zaidi miaka 10, 20, 30 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yale tuliyozungumza mwaka wa 1997, 1998 yangezingatiwa leo hii tungekuwa tumepiga hatua mbele.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini amejibu hapa, amesema hata mrahabatunaopata tofauti na kwenye dhahabu ni asilimia tatu na almasi asilimia tano na ni kwa

mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa mikataba. Sasa tuunganike sote, tuone Taifa linavyoibiwa kwa maslahi mapana ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, ningependa kulitahadharisha Bunge na leo ni siku ya Ijumaa. Mtume Muhammad aliwahi kuwausia waumini wake, maarifa ni kitu chake kilichompotea muumini, popote akipatapo na akichukue. Hili suala la madini lazima Wabunge wapewe semina kwanza, kwamba uchumi wa madini ukoje, biashara ya madini ikoje. Tupewe semina kwanza tujue duniani biashara hii ikoje, tukifanya mabadiliko ya sheria kwa mhemko tulionao tutatandikwa kweli kweli kwa sababu tutafanya ni ushabiki kabla hatujajua mambo haya na tukubali huyu ana taaluma hii, huyu ana taaluma hii, tuwe na taaluma shirikishi, tushirikiane pamoja kwa maslahi mapana ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ili tuweze kutoka hapa, tuwe na mifumo endelevu ambayo inahimili. Leo hii yuko Rais Magufuli, kesho atakuja Rais mwingine, lakini kuna mifumo ambayo ni ya Kikatiba. Tukawa na Katiba mpya ambayo Rais yeyote yule anayekuja lazima ataheshimu katiba, sheria na taratibu, tutasonga mbele tukitoka hapa tulipo kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema haya kwa nia njema kabisa kabisa. Bila kupata elimu ya kutosha ya uchumi wa madini tutapata matatizo makubwa sana na lazima tukubali kushiriki kwa pamoja tutafute suluhisho ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine, Bunge letu hili huwa tunashabikia vitu ambavyo hatuvijui, Mithali 18:13 inasema kujibu au kushangilia kabla ya kusikiliza ni upumbavu na jambo la aibu. Sasa tusije tukaanza kujishangilia, kujidhalilisha sisi wenyewe tunamdanganya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ushabiki huu ambao unaendelea kwenye Bunge letu. Tunaona mambo ya ajabu ajabu ambayo yanaendelea kwenye Bunge letu,

niombe tena chonde chonde; kwa mfano tuko kwenye viwanda viukuze uchumu wetu lakini viwanda tulikuwa navyo. Viwanda vilishabinafsishwa na kwenye zoezi la kubinafsishwa hata sisi wengine tuliumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi nimeshtakiwa Mahakama Kuu nadaiwa dola milioni moja kwa ajili ya mambo ya ubinafsishaji, Dkt. Mwakyembe anajua ile kesi ya *NBC* nashtakiwa mimi na wanaotushtaki ni hao hao wa upande mwingine ambao ndiyo wanashirikiana na hao kutudhalilisha kwa sababu ya kulitetea Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri nakuomba angalia sana Sekta ya Madini, angalia Uvuvi. Ukiangalia tozo zilizoko kwenye sekta ya madini, tozo zilizoko kwenye masuala ya uvuvi wa bahari kuu tukiwekeza vizuri kwenye sekta ya madini tukaondoa kodi zisizo na tija kwenye sekta ya madini, tukaondoa tozo zilizoko kwenye sekta ya madini ambazo ziko karibu kodi na tozo zaidi ya 57, tutavutia watalii kutoka milioni moja kwenda kwenye milioni mbili. Tutoke kuwa *niexpensive destination* hapa Tanzania utalii peke yake utaendesha uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunashika nafasi ya 110 kati ya Mataifa 133 katika ushindani wa utalii na mapato ya utalii; lakini ni wa pili katika vivutio vya utalii duniani. *Let us think big, let us think globally and act locally. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba Taifa hili tukiwekeza vizuri kwenye madini, kwa mfano hata kwenye uvuvi, bahari kuu ina kilometa za mraba 230,000; mapato gani tunayopata kwenye uvuvi? Nendeni mkasome ile na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tulikuwa wote pamoja kwenye ile ripoti ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato.

Sasa tuwe tunaanza mapema kutengeneza na tuwe na muendelezo wa bajeti hizi ya mwaka 2015, 2016 ninazo zote hapa 2017. Angalia hata deni la Taifa, limetoka trilioni 35, likaenda 39 leo hii ni trilioni 50.8. Tanzania tunazidi kwenda kusiko, lazima tuwe na bajeti ambazo ni endelevu kwa maslahi mapana ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vyanzo hivi vipya vya mapato tushirikiane sote. Kwa sababu tukisema tu deni la Taifa himilivu, watoto wetu na vizazi vijavyo vitakuja kututandika makaburi yetu viboko kwa sababu tulikuwa hatuwezi tukafiki vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, ahsante sana muda wako umekwisha.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mwenyezi Mungu akubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maida Abdallah, baadae Mheshimiwa Ezekiel na Mheshimiwa Jamal na Flatei Massay wajiandae.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia uchumi wa Taifa hili. Tunampongeza Mheshimiwa Rais na tunasema Watanzania wengi tupo nyuma yake, aendelee na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii wakiwemo pamoja na wataalam waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kukamilika kwa bajeti hii ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti pia niwapongeze wananchi wa Tanzania waliopongeza au wanaoendelea kupongeza bajeti hii ya Serikali, bajeti hii ni nzuri na ina matumaini makubwa kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nithubutu kusema kwamba wananchi wa Tanzania wengi ni wa kulima na wameipongeza bajeti hii kwa sababu imeweza kuwafutia kodi mbalimbali katika ushuru mbalimbali wakiwemo wakulima, wafugaji wamefutiwa kodi za mazao, wamefutiwa kodi kwenye chakula cha mifugo, wamefutiwa kodi katika vifaranga lakini pia nithubutu kusema kwamba wananchi hawa wameendelea kupongeza Serikali hasa pale mkakati wa Serikali wa usambazaji wa mradi wa umeme vijijini.

Lakini pia wananchi hawa, wamekuwa wakipongeza Serikali kwa kufutiwa gharama za *service charge* katika gharama za umeme, kwahiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa jitihada zake za kuleta au kwa kuwarahisishia wananchi uchumi ulio nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali kwa vile wananchi wengi ni wa kulima katika Taifa hili, na Serikali kupitia sekta yake ya kilimo au kupitia sekta ya kilimo imekuwa ikiandaa mikakati mbalimbali ya kukuza kilimo lakini pia imekuwa tofauti katika kufikiwa malengo ya kilimo kutokana na uchache wa fedha.

Kwa hiyo, basi niombe sana Serikali kupitia sekta ya kilimo kuingiza fedha haraka au Hazina wapeleke fedha haraka ili sekta yetu ya kilimo iweze kukua na ile mikakati iliyopangwa ya kukuza kilimo iweze kufikiwa na tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende katika Benki ya Wanawake. Katika vitabu vya Serikali vile vya mpango pamoja na vya bajeti vimekuwa vikieleza kwamba sasa hivi Benki hii imekuwa ikiendelea katika maeneo mengi katika Tanzania Bara, na imeshafungua vituo na imeshaanzisha vituo karibuni 252 katika maeneo ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nithubutu kusema kwamba benki hii uanzishwaji wake tulishiriki wananchi mbalimbali na wafanyabiashara mbalimbali waliopo Tanzania Bara na Zanzibar. Lakini pia kuna hisa walizonunua au walizowekeza katika Benki hii, hadi leo benki imekuwa ikiendelea kufungua vituo au matawi katika maeneo ya Tanzania Bara lakini Zanzibar wamekuwa wakichelewa kuhusiana na suala la ufunguaji wa vituo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali kuendelea pamoja na kuwa inaendelea Tanzania Bara lakini pia iendeele kufungua vituo Tanzania Zanzibar kwa sababu Zanzibar kuna wananchi wajasiriamali, Zanzibar kuna wakulima, Zanzibar kuna wafugaji na wao wanahitaji mikopo kupitia benki hii na benki hii haianishi wanawake tu inakwenda moja kwa moja kwa wananchi wote katika jamii. Kwahiyo, niombe sana Serikali kujielekeza kule Zanzibar kufungua vituo Unguja na Pemba ili nao waweze kufaidika na hisa walizoziweka viongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nilitaka nizungumzie kuhusu shilingi 40 zilizowekwa katika lita ya mafuta, wananchi hawajaona tatizo kuwekwa shilingi 40 kila lita moja ya mafuta kwa sababu kodi mbalimbali walizokuwa wanalipa ilikuwa ni zaidi ya shilingi 40. Kwa hiyo wamefurahi na hawana tatizo ya lita ya mafuta kuongezeka shilingi 40, shilingi 50 haitumiki hata ukienda dukani basi huwezi kutumia shilingi 50 wala hawaoni tatizo shilingi 40 kwa kila lita ya mafuta kuongezwa katika suala la ulipaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe sana Serikali pamoja na kuwa imewajali wakulima, lakini pia iwajali na

wafanyabiashara, kuna wafanyabiashara wakubwa, kuna wafanyabiashara wadogo. Pia wafanyabiashara hawa wamekuwa na utitiri wa kodi, utitiri wa kodi kwanza kulipia mzigo bandarini, wanaposafirisha mizigo yao kupeleka dukani, wanapofikanao mzigo huu dukani na kila wanapouza bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kuwa Serikali au Mheshimiwa Rais amefikiria suala la wakulima lakini pia lifikirie na wafanyabiashara kwa sababu wafanyabiashara wengi kodi zimekuwa kubwa, imekuwa wamefunga biashara zao na walikuwa wanaajiri watumishi mbalimbali, kundi kubwa la vijana sasa hivi halina kazi wafanyabiashara wamekuwa wakifanya kazi wenyewe na kuwaacha wafanayakazi wao. Kwa hiyo, wengi wa vijana hawa baada ya kukosa kazi wameingia katika masuala ya ubakaji na hujuma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, niombe sana Serikali pamoja na kuwa katika bajeti hii tumewafikiria sana wakulima lakini tuwafikirie na wafanyabiashara kwa sababu ndio wanaongeza uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na suala la mapato ya fedha yanayotokana na watumishi wa Jamhuri ya Muungano walioko Zanzibar. Mpaka leo hii na suala hili limekuwa muda mrefu sasa, kusanyo la shilingi bilioni 1.75 hili ni suala la muda mrefu, kwa hiyo, mishahara hii imekuwa ikikuwa siku hadi siku wamekuwa watumishi hawa wakiongezewa mishahara, kwa hiyo, niombe sana Serikali kufanya tena mchakato au tathimini ya wafanyakazi walioko Zanzibar kutoka kipindi cha nyuma hadi sasa hivi wameongezeka kwa kiasi gani, lakini pia mapato yanayotakiwa kuingia sasa hivi Zanzibar kuhusiana na watumishi hawa *income tax* ni kiasi gani tusiendelee tu na asilimia 1.7 kama tunavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipewe elimu kuhusiana na suala la asilimia 4.5 inayoendelea kwa sababu asilimia hii 4.5 ni ya muda mrefu kwa upande wa Zanzibar

wananchi wamekuwa wakituuliza maswali mengi, kwa hiyo niombe sana Serikali kutoa elimu zaidi kwa sababu uchumi toka tulipo ingia katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuwa Tanzania ni muda mrefu, uchumi wetu umekuwa ukikua siku hadi siku, tofauti na uchumi ulivyokuwa nyuma, kwa hiyo, asilimia 4.5 naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe elimu kuhusiana na asilimia 4.5 ili wananchi wa Zanzibar waweze kuridhika na wasiwe na maswali kuhusiana na maswali kuhusiana na kero za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maida. Kabla hatujaendelea na mchangiaji kuna wageni wamefika wapo kwenye jukwaa zetu ni Makatibu wa CCM wa Mkoa wa Iringa pamoja na Wilaya zake wakiongozwa na Katibu wa Mkoa ndugu Mgalla karibuni sana Makatibu wetu wa CCM wa Mkoa wa Iringa pamoja na Wilaya zake. *(Makofi)*

Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Ezekiel Maige na baadaye Mheshimiwa Jamal na Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Venance Mwamoto wajiandae.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. La pili naomba niseme bajeti ni nzuri, naiunga mkono, nishauri tu kama ambavyo Wabunge wengi wamesema kwamba eneo la maji au fedha tulizotenga kwa ajili ya maji bado tatizo ni kubwa ni vizuri eneo hili likatizamwa angalau fedha zikaongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala hilo la bajeti, naomba nizungumzie suala la mapato ya Serikali. Kama tunavyojua bajeti unahusu mapato na matumizi na unapozungumzia mapato ya Serikali na hasa kwa Mbunge unayetoka Bulyanhulu huwezi ukaacha kuzungumzia suala la makinikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa hatua ambazo amezichukua kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi tumezungumza. Naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba kuna Mbunge mmoja amezungumza hapa kwamba kuna Tume nyingi zimewahi kuundwa na akasema tume hii ya Profesa Osoro na Profesa Mruma ni idadi tu ya nyongeza ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamishe Mbunge huyo aliyesema hivyo kwamba pengine hajachukua muda wa kufuatilia naomba nifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba tume ya Bomani ambayo mimi nilikuwa mmoja wapo pamoja na wenzangu kina Dkt. Mwakyembe kazi yetu sisi tuliambiwa tufuatilie/tufanye mapitio ya sera na sheria kuangalia na nchi zingine wanafanyaje ili tutoe mapendekezo kwa Serikali kwa ajili ya kurekebisha maeneo ambayo hatufanyi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya kazi kwetu hatukua tunafanya uchunguzi (*investigation*) ndiyo maana tume yetu tulikuwa tunafanya kazi kwa kufanya mikutano ya hadhara tunatangaza tupo wapi wananchi wanakuja wanaeleza na hayo tuliyajumuisha kwamba wananchi wa maeneo wanayozunguka migodi wana mawazo haya. Kwenye eneo la usafishaji kwa mfano wa makinikia *observation* ya Kamati ilikuwa ni kama ifuatavyo naomba nikusomee tulisema hivi; "kukosekana kwa mkatakati wa kisera wa uanziswaji wa viwanda vya uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini kumesababisha madini na mchanga wa dhahabu kusafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya usafishaji na uchenjuaji, hali hii imesababisha Serikali kushindwa kudhibiti aina na kiasi cha madini kinachozalishwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *observation* hii ya Kamati inaonesha kwamba kuna "*smoking gun*" inaonyesha kwamba kuna tatizo kwenye hili, ndio maana sasa Mheshimiwa Rais Magufuli sasa akaunda Tume ya kuchunguza kwa hiyo, tofauti ya hizi tume za mwanzo za ushauri na mapitio ya sera, Tume ya Profesa Mruma na Tume ya Profesa Osoro zilikuwa zinachunguza jambo hili mahususi

kwamba kuna nini na kitu gani ambacho kinafanyika.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jipya amblo halijafanyika, kwa hiyo, Tume ya Osoro na Tume ya Mruma ni tofauti na Tume ya Bomani na kwa mara ya kwanza sasa tunapata tume mahsusi kwa ajili ya kuchunguza, na baada ya hatua hiyo matokeo ya uchunguzi yalipopatikana hatua zimechukuliwa *very aggressively, very bold, very fame, very patriotic*. Ni kwa *approach* hii niliwahi kusema hata kwenye kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwamba kampuni kama ya Acacia ndipo inapoweza kuja kwenye mazungumzo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwa wawekezaji hawa ni *arrogant*, ni fedhuli katika hali ya kawaida si rahisi wakaja kwenye meza ya mazungumzo bila kuwabana na bila kuwa na *data* za kutosha za kiuchunguzi, ndio maana leo unawaona wanakuja kwa sababu uchunguzi umefanyika na imedhihirisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, na wananchi wa Kakola, wananchi wa Bulyanhulu wanampongeza sana na tayari wameshamuomba Mkuu wa Wilaya awaruhusu wafanye maandamano kama itawezekana kwa ajili ya kupaza sauti zao maana wamepoteza ardhi, wamepoteza wenzao na mambo mengine lakini amepatikana mkombozi ambaye hatua anazochukua zinagusa kabisa mioyo yao na maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo naomba nizungumze *local issues* na hili nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Profesa Kabudi ambaye wanazungumza au wanasimamia suala hili wananchi wa kule ambako makinikia yanatoka wanaona kabisa kwamba na wanaomba *issue* zao zizingaiwe, zitizamwe na ziwepo katika majadiliano yatakayo fanyika baina ya Serikali na mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo tunaomba litizamwe pamoja na kuibiwa huku kwenye Serikali Kuu na Halmashauri tumeibiwa, kwa takwimu za Profesa Osoro Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Wilaya Msalala tunadai kati ya shilingi bilioni 795 hadi shilingi trilioni mbili bilioni 283 za *service levy* kwa takwimu za Profesa Osoro kwa uzalishaji wa Bulyanhulu na Buzwagi kati ya mwaka 1998 hadi 2017. Tunaomba jambo hili halmashauri fedha hizi ziwemo katika majadiliano na Halmashauri tuzipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili uchunguzi ufanyike kuangalia makampuni mengine ambayo ni *related companies* ambazo zinafanya biashara kwa sababu zimekuwepo na hii tunaita *transfer price bills*, makampuni yanayotoa huduma kule hayalipi *service levy*, kwa hiyo, tunataka kujua yamefanya biashara kiasi gani ili Halmashauri tuweze kutoza *service levy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu tunaomba sana katika mikataba na *practice* za kimataifa, mwekezaji anatakiwa kutumia angalau asilimia moja ya mapato yake kwa ajili ya huduma za kijamii. Kwa kutumia takwimu za Profesa Osoro toka mwaka 1998 hadi 2017, Kahama tunapaswa tuwe tumewekezewa au tumesaidiwa kwenye miradi ya kijamii asilimia moja ya uzalishaji wa Acacia ambayo ni sawa na shilingi trilioni 1.320. Kwa hiyo tunaidai *cooperate social responsibility* tufanye *reconciliation* kile walichofanya na trilioni 1.320 ili tuweze kulipwa kinachohitajika kingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaomba lifanyiwe uchunguzi ni kwa kuna madai ya wafanyakazi wanaugua, wako wafanyakazi wengi nilikuwa nikiongea sana na Waziri wa Kazi wafanyakazi wanaopata madhara ya kiafya, kwa hiyo, ufanyike uchunguzi kuhusu afya za wafanyakazi na waliokuwa wafanyakazi na wengine ambao wamekwisha kuathirika walipwe fidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna wananchi 4,600 waliondolewa kwenye lile eneo

hawakulipwa fidia yoyote, kwa hiyo, katika majadiliano suala la *compensation* nalo lizingatiwe na likumbukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kwa kuwa haya yameonekana kwenye makinikia peke yake tunaamini hata kwenye vitofari vya dhahabu nako kuna matatizo. Kwa hiyo, uchunguzi uongezeke tuangalie kwenye vitofali na kwenye migodi mingine, haiwezekani *TMAA* wakawa wachawi kwenye Bulyanhulu halafu wakifika *Geita Gold Mine* wakawa watakatifu, *practically* na kule kuna matatizo uchunguzi ufanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho wote tunajua kwamba mwekezaji huyu amekubali kujenga *smelter* na tunajua makinikia yanatoka Bulyanhulu na *smelter* itajengwa Tanzania, niombe Wizara na waratibu wa suala hili basi wafahamu kwamba *economically* na mazingira yote *smelter* tunaomba ijengwe pale ambapo makinikia yapo, tunaomba *smelter* ijengwe Bulyanhulu, naomba mtufahamishe mtuambie inatakiwa ardhi kiasi gani na maandalizi ya namna hiyo yaanze tutenge ardhi, muweze kujenga *smelter*. Sitaratiji kusikia kwamba *smelter* inajengwa sehemu nyingine yoyote tofauti na Kahama kwa sababu za mazingira hayo ambayo tunajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niseme napongeza sana bajeti hii namuunga mkono sana Mheshimiwa Waziri na bajeti yake lakini kubwa zaidi wananchi wa Bulankulu, wananchi wa Msalala wanampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua anazochukua tunaomba haya maeneo ya uchunguzi yanayohitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi yafanyiwe uchunguzi, madai ya wananchi mbalimbali ambayo wananathirika na jambo hili yajumuishwe katika majadiliano baina ya Serikali na mwekezaji ili wakati Serikali inalipwa zile trilioni 108 na sisi Kahama tunalipwa bilioni 795 *service levy* tunalipwa vile vile trilioni 1.320 kwa ajili ya *cooperate social responsibility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ezekiel Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Jamal Kassim na baadaye Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango na Bajeti ya Serikali. Kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo amefanya hususani katika suala la kusimamia rasilimali la taifa hili kuhakikisha rasilimali hizi zinanufaisha taifa hili na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi toka alivyoanza kazi, toka alivyoapishwa mambo aliyoyafanya ni makubwa ni mambo ambayo yanajieleza yenyewe kwamba ni miongoni mwa Marais ambao wameji-*commit* katika kutusaidia kuleta maendeleo katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na timu yao kwa bajeti nzuri, kusema la ukweli bajeti hii imeenda kujibu ile dhana ya kwamba tunaenda kwenye Tanzania ya viwanda, tumeona namna gani sera za *fiscal* yaani kodi zilivyowekwa ili kusaidia uanzishwaji wa viwanda vya kati na vikubwa. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na maeneo machache ya kuchangia kama sehemu ya ushauri, eneo la kwanza ambalo ningependa kuchangia ni suala la kodi ya mapato. Kodi ya mapato kwa mujibu wa Katiba yetu ni kodi ya Muungano na chombo ambacho kinasimamia kodi hii ni Mamlaka ya Mapato ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua nchi yetu ina sehemu mbili kuna sehemu ya Zanzibar ambayo Zanzibar ina Serikali yake ambayo kwa upande mmoja inategemea kodi ambazo zinatokana na mapato ambayo kwa upande wa Zanzibar *TRA* ndio inakusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria yetu ya kodi ya mapato taasisi zote ambazo zitafunguliwa kama sehemu ya tawi la makao makuu, basi ofisi hizo hazitatoza kodi ya mapato, yaani kodi ya mapato itatozwa *at a corporate level*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini, kwa upande wa Zanzibar tumekuwa na makampuni mengi ambayo Makao Makuu yake yako Dar es Salaam yanaendesha shughuli zao za kibiashara Zanzibar. Kwa harakahara tuna taasisi za fedha kumi yaani mabenki kumi ambayo zinafanya biashara Zanzibar. Tuna kampuni za simu tano, tuna kampuni za bima na kampuni mbalimbali ambayo yanatoa huduma na yanafanya biashara Zanzibar lakini kwa mujibu wa sheria yetu ya kodi ya mapato hazilipi kodi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ambayo inayokuswanya na *TRA* Zanzibar ndiyo kodi ambayo inaenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya shughuli zake za uendeshaji na kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua Zanzibar, kiuchumi, uchumi wake ni mdogo, pia vyanzo vyake vya mapato ni hafifu. Naamini sasa busara itumike kwa makampuni haya ambayo yanafanya shughuli zake Zanzibar kama sehemu ya matawi basi na yenyewe yaanze kulipa kodi Zanzibar ili iweze kusaidia kuongeza mapato kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hivyo basi iweze kufanya shughuli zake za maendeleo na kijamii kama ambavyo tumeahidi kwenye ilani yetu ya chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Mwaka jana tulivyokuwa tunapitisha *Finance Act* kwenye Sheria ya *VAT*, tulipitisha kwamba bidhaa zote ambazo zitatengenezwa Tanzania Bara na kununuliwa Zanzibar na mnunuzi ambaye atakuwa amesajiliwa na *VAT* basi biashara hizi hazitatozwa kodi au bidhaa hizi hazitatozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kumekuwa na uzito katika utekelezaji wa suala hilo, kuna kesi nyingi sana, wafanyabiashara wetu ambao wananunua bidhaa hizi ambazo zinatengenezwa Tanzania Bara ikiwemo mabati, bidhaa za urembo wakitozwa kodi hiyo na wakienda Zanzibar wanatozwa tena. Kwa hiyo, kumekuwa na tozo mara mbili ambayo wafanyabiashara wetu wamekuwa wakitozwa na sheria iko wazi imeainishwa na tulipitisha. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*windup* labda utupe msimamo wa Serikali juu ya hili pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka jana tulipitisha Sheria ya *Finance Act* tulifanya mabadiliko katika Sheria ya *The Electronic and Postal Communication Act* kwa kuyataka makampuni yetu ya simu kwanza yawe *listed* katika *Dar es Salaam Stock Exchange*, lakini pia yatoe asilimia 25 ya hisa zake kwa wananchi au wakazi wa Tanzania. Lengo kuu ambalo Mheshimiwa Waziri alilolisema ilikuwa kwanza kuwapa fursa Watanzania nao kushiriki katika uchumi huu mkubwa ambao unakuwa wa sekta ya mawasiliano lakini pili kujenga uwazi wa kujua kwamba nini hasa biashara hii ya makampuni haya ya simu yanapata kutokana na muda mrefu kutokuchangia vile ipasavyo kwenye kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Watanzania kupitia Rais wetu tumeamka kwamba kwenye sekta ya madini tunaibiwa. Kila mtu aliyenyanyuka katika Bunge hili kuchangia, watu wote wamezungumza kwamba kwenye sekta ya madini tunaibiwa. Aidha, tunaibiwa kutokana na kutokuwa na uwazi wa kutosheleza kwenye biashara hii au sababu zinginezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kwa vile Rais amesema sheria hizi atazileta Bungeni tuzifanyie maboresho na mikataba hii.

Kwa hiyo, niishauri Serikali itakapoleta sheria hizi wakati umefika sasa wa sheria hizi pia, makampuni haya makubwa ya madini yawe *listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* iwe sharti namba moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti la pili lazima kuwe na *local content participation*. Lazima nao wafaidike na rasilimali yao, japo hatuna pesa nyingi lakini kwa kidogo kidogo tulichokuwa nacho naamini kabisa tunaweza tukachangachanga hicho na tukapa. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hicho anachosema makampuni yawe *listed* yako *listed* tayari kwa miaka kadhaa, Acacia wako *cross listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* tangu mwaka 2014.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jamal unapokea hiyo taarifa?

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria nimezungumzia suala la sheria, lazima iwe *mandatory* si suala la mtu kupenda, tuna makampuni mengi zaidi ya Acacia, yanachimba madini. Kwa hiyo, lazima tuweke sheria ambayo makampuni yote ya madini yawe *listed*, lakini ...

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja Mheshimiwa Jamal.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya yote kuna umuhimu yakawa *listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu jamani tumwachie dakika moja yake amalizie.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza kwa kuunga mkono hoja, kuipongeza bajeti hii, naamini ni bajeti ambayo inatupa mwanga wa dira yetu ambayo tumeiweka ya kwenda Kwenye Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jamal Kassim. Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Emmanuel Papian wajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya leo kuchangia katika bajeti hii ambayo kimsingi nadhani itakuwa ya kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache ya kuishauri Serikali katika bajeti hii. Yako mambo ambayo kimsingi nimeyasoma katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli naona tu nielezee kidogo. Masuala haya ya mipango mkakati, katika miradi ya mkakati ambayo Mheshimiwa Mpango umeeleza kwenye mipango yako, nikuombe basi kwa kuwa umeeleza miradi hii ya kiuchumi ya vipaumbele...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu, tumsikilize Mheshimiwa anachangia, naomba utulivu hapo mbele.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Mchuchuma ambao umeonekana kipaumbele katika bajeti yako, mradi wa mitambo ya kusindika gesi, Mradi wa Biashara ya Kurasini, mradi wa uwekezaji wa Bagamoyo, mradi wa Mtwara, miradi hii ambayo inaonekana kwenye mpango wako kwa kuwa umeweka miradi hii kama eneo la mkakati wa kuinua uchumi wa Serikali na nchi yetu basi

maeneo haya nishauri tu, miradi hii sasa ifike mahali kwa pesa nilizoziona zimetengwa humu. Kwa mfano Mradi wa Biashara ya Kurasini iko bilioni 109 ambayo imeshalipwa fidia pale, pesa zimekaa pale. Niombe kutokana na mkakati huu Serikali ipange namna gani nzuri ya kuendelea na mipango hii ili walau Tanzania ikaweza kuendelea kutokana na mipango hii ambayo tumejiwekea yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kushauri katika eneo hili la maeneo hasa ya maji vijijini. Maji vijijini ukiangalia kwenye bajeti iliyopita fedha za maji vijijini imeenda kwa asilimia 19. Niombe kwa kuwa umeonesha kwenye mpango wako huu kiwango hiki cha maji basi iende kadiri ilivyopangwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha. Pia angalia maji vijijini tunahitaji sana kwa sababu tozo ya maji haipo sasa na Wabunge tunapendekeza tozo hii iweze kuingia humu, Serikali ikubali basi ushauri huu ili walau maji yaweze kwenda vijijini. Hakuna eneo lolote unaweza kumwambia mtu katika eneo la vijijini hatuna maji kwahiyu tuangalie katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni habari ya *REA*. *REA* imeonekana kuchukua kasi yake na wananchi wanaifurahia, lakini nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Waziri wa Nishati naamini Kalemami umefika kwenye eneo langu. Mbulu Vijijini tunahitaji umeme wa *REA*, hakuna viwanda bila umeme. Kwa hiyo nikuombe katika bajeti hii utuone vizuri sana sisi wananchi wa Mbulu Vijijini. Pia barabara hatuna, nimeamua kusema harakahara haya ili yaeleweke. Sisi kule barabara hatuna na umepita kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kalemami ulifika Mbulu, ukaiona barabara ile, ulisema kabisa kwa maneno yako nanukuu; "mngeniambia barabra hii iko mbaya namna hii ningetafuta barabara nyingine" haya ni maneno yako Mheshimiwa Waziri. Sasa nikuombe kitu kimoja kwa ajili hii basi miradi hii tunayoiomba pesa ziende. Mheshimiwa Mpango anafahamu nimeleta maombo yangu kwake kuhusiana na msamaha wa kodi ya *VAT* katika *grand* ambayo tumepewa.

Narudia tusaidie basi katika mabadiliko ya sheria ambayo yanatakiwa kuja Bungeni, naomba sasa sijaona vizuri humu ulete mpango huo ili walau sheria hii ibadilishwe, pawe na mwanya wa kusamehe kodi kwa fedha za wafadhili mmoja wanaotaka kufadhili kujenga madaraja ya kwetu. Nafikiri hili unalifahamu na utaamua kulifanyia kazi na sisi Wabunge tuangalie maeneo haya, kwa sababu mfadhili anatusaidia na sisi tunasaidiwa katika bajeti yetu basi tuone namna gani sheria iruhusu kusamehe kodi kwa maeneo haya ya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri jambo moja, wenzangu wengi wameongelea sana kuhusu madini, nimeona pia katika kitabu chako cha hotuba yako Mheshimiwa Mpango ukurasa wa 49 umeandika kwamba Serikali haitaruhusu usafirishaji wa madini kwenda nje yaani kutoka kwenye mgodi kwenda nje, hili sina tatizo nalo. Nataka nishauri kitu kimoja, ukitaka kuzuia hii madini tuanzishe soko la madini, liwepo hapa nchini ili walau soko hili likitambulika Serikali ni rahisi kukusanya mapato katika soko. Tatizo letu lililoko hapa watu wakichimba madini katika maeneo yetu wanakwenda kwa njia za panya wanauza nje kwa sababu kuna soko huko nje. Kwa hiyo, ninashauri Serikali ianzishe soko la madini yetu yote yanayoonekana yanapatikana nchini ili wananchi wasitoroshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naomba niongee leo kama ushuhuda. Sisi wote tumeingia humu kuwakilisha wananchi wetu, lakini pia Serikali imeanza kazi na nimshukuru sana na niseme kabisa namuombea Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa sababu ameonesha nia ya kuisaidia Tanzania kwa kujitoa muhanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hakuna anayeweza kusema anamuombea kwa upande fulani ninaoufahamu, lakini nimshukuru sana leo Mheshimiwa Mbatia amesema hapa mwenyewe kwa kauli yake na nimtaja kwa jina kwa sababu *Hansard* zinarekodi, anamuunga mkono Rais kwa suala hili la madini na ule mchanga ambao umesemwa sana sitaku kuusemea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biblia inasema kila mtu atabeba msalaba wake mwenyewe, na sisi naomba Waheshimiwa Wabunge nataka niwahamasihe jambo moja. Kubeba msalaba wake mwenyewe kwa siye tunaoabudu kwa dini ya Kikristo na Waislamu ambao wamefunga mwezi huu wa Ramadhani tumuunge mkono Rais wetu, sheria zitakapoletwa Bungeni tuanze kuweka vizuri mipango yetu ili katika haya Mheshimiwa Rais amejilipua, anahitaji kutusaidia na ameomba ridhaa wananchi tumempa. Habari ya kwamba ametoka chama gani, chama A, chama B tumeingia kwa vyama lakini ukiangali *research* inaonyesha tuangalie maslahi ya nchi, kwa sababu wanachama wetu wa vyama vyote hawafiki hata robo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutee Tanzania, tumeingia humu kwa vyama vyetu lakini sasa tutee mama yetu Tanzania. Kila mtu ameapa hapa na tumeapa kuitetea Tanzania, tunateteaje sasa? Nimesikia mchangiaji mmoja akisema hapa bado wakati wa kumpongeza Rais Magufuli. Unasemaje bado wakati mwenzako ameonesha nia? Mimi ninamsikitikia sana ndugu yangu Lissu, akionyesha nia mtu mmoja mshangilie kwa nia hiyo baadaye uhoji matokeo. Lakini nikuombe kaka yangu, mtani wa Singida tumtete huyu ndugu aliyeonyesha nia kwa sababu ni Rais hakuna Rais mwingine zaidi ya huyu. Tukimtetea kwa nia aliyoonyesha atasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote wanahitaji maendeleo, na sasa tumeibiwa kwenye madini, tunaona tumeibiwa kwenye madini, na nikuombe Rais asiishie kwenye haya maeneo tu aende kwenye maeneo yote ya uchimbaji wa madini akadhibiti huko kabisa kwenye migodi ili migodi hii ionekane, iingize pesa za kigeni ili Tanzania tupate maji, barabara pia tupate vitu vingine vya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio nilitaka niseme ili watu waelewe na Waheshimiwa Wabunge waelewe kutoka CCM na kutoka CHADEMA kwamba Mheshimiwa Rais amesema kwamba analeta sheria ya mabadiliko ya madini huku tukasaidie hali hii kwa kutumia uwingi wetu humu.

Uwingi maana yake nini? Sisi Wabunge kwa sababu ndio tunaobadilisha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda mbele zaidi ninajua kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Mpango kwanza nimshukuru sana amejitahidi sana kuelezea maeneo mengi sana lakini Serikali itusaidie katika maeneo haya ambayo imeanzisha tawala mbalimbali imeelekeza maeneo haya ya vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele ni kweli lazima tuiendee lakini kuna tozo ambayo sisi tunaiomba kama Wabunge kuongeza kwenye mafuta shilingi 40 tu. Najua yataongezeka, najua kuna tatizo kupanda na kushuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu Serikali ikubali tuongeze jambo hili la ongezeko la tozo kwenye mafuta ili tupate maji vijijini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina jinsi kwa sababu muda umekwisha naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay. Tunaendelea na Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Lucy Mayenga wajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza leo kupata nafasi hii ili niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tulipokuwa tunakwenda kwenye uchaguzi tuliomba atuletee Rais wa namna gani. Kwa hiyo nimshukuru, tusiposhukuru kwa kidogo huwezi kupata zaidi. Mwenyezi Mungu amesikia kilio chetu tumepata Rais ambaye tulikuwa tumemwomba kwa hiyo, ahsante sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, alivyoingia wakati anagombea kuna vitu aliahidi; aliahidi kusimamia rasiliamli za Taifa, ameanza kazi na mmeona. Aliahidi kununua ndege, aliahidi kujenga reli, aliahidi kuendeleza ujenzi wa barabara, aliahidi kuboresha huduma za afya, aliahidi kurudisha heshima na nidhamu kazini, aliahidi kubana safari za nje, aliahidi kuendelea kuboresha ukusanyaji wa kodi, aliahidi kuleta amani kwa watu kufanya kazi kupunguza kuandamana. Kwa sababu unakuta maandamano mengi yalikuwa ni kwa sababu watu hawana kazi za kufanya, lakini leo watu wanafanya kazi, muda wa kuandamana haupo, kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia aliahidi kuendelea kupunguza kodi, hasa za wakulima, mmeona kwenye bajeti yetu kodi zimepunguzwa, niseme sasa wengi wameona, yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata bahati kubwa tusameheane, kwa sababu jana Mheshimiwa Dkt. Rwakatare na mimi niseme wazi Mheshimiwa Dkt. Rwakatare yupo hapa tunawapa kazi, Mchungaji ya kuombea Bunge hili ili watu tubadilike ukishirikiana na Mchungaji, Mheshimiwa Bilakwate yupo na Sheikh Ulega. Fanyeni kazi kubwa ya kuombea Bunge letu ili tubadilike tutetee maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni kweli kwa muda mrefu tumeibiwa, sasa tumesema basi na bahati nzuri tumepata bahati ya kupata Rais wa Wanasheria ambaye yuko humu ndani, tunakuomba Mheshimiwa , kwa sababu tumesema yaliyopita si ndwele utusaidie sasa tupambane tupate haki zetu kutoka kwa hao wazungu, kweli wewe ni rafiki yangu, tafadhali tuungane kwenye hili. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa mchangiaji hujui sifa za masheikh, Mheshimiwa Ulega tangu lini ni Sheikh? Hujui sifa za Masheikh, Mheshimiwa Ulega sio Sheikh Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ustadh Ulega na Mheshimiwa Ustadh Lissu yupo pia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nizungumzie habari ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango; niseme ningekuwa niko kule Kigoma ningesema Mheshimiwa *ushimwe chane* yaani ubarikiwe. Umetendea haki Taifa, umetendea haki Bunge, umewatendea haki Watanzania wote na Wanakigoma. Niseme kazi ni kwetu wenyewe sasa kusimamia, suala la kusimamia rasilimali za nchi sio la Serikali peke yake, ni suala letu sote kuhakikisha tunasimamia rasilimali zetu kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Jimbo langu sasa la Kilolo kidogo. Kwenye Jimbo la Kilolo Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba atahakikisha tunapata maji safi na sasa hivi kazi imeanza, tumeanza kupata maji pale Ilula na sehemu nyingine mambo yanakwenda vizuri. Lakini pia kuna suala la kilimo cha umwagiliaji, kilimo hiki lringa Wilaya ya Kilolo na Mkoa wa Iringa tuko milimani, kwa hiyo tunategemea sana kilimo cha mabondeni, wanasema vinyungu. Sasa ni suala la Serikali kutoa fedha kuboresha mifereji ili kile kilimo badala ya kuendelea kuzuia waache watu walime, waweke mpango mzuri, mifereji ya umwagiliaji ijengwe ili watu waendeleo kulima badala ya kuendelea kuwazuia watu kulima kwa sababu tukifanya hivyo kuna hatari ya kupata njaa kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya na mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kigoma kilimo cha mabondeni wanaita masebura, ni kilekile kwamba mnalima mabondeni, nikisema hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na

Mipango amenielewa, kwamba masebura ni kilimo cha mabondeni sio cha kwenye vyanzo vya maji, vyanzo vya maji ni mbali lakini cha mabondeni wananchi waachwe waendeleo kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutafsiri vizuri sheria kutatufanya tulete njaa kwenye nchi hii. Kwa hiyo, nikuombe kabisa Mheshimiwa uniombe kwa Mheshimiwa Waziri wa Mazingira na Waziri wa Maji waweze kutafsiri vizuri zile sheria, kwamba kwenye vyanzo vya maji wazuie mita 60 lakini kwenye mabonde hawawezi kulima mita 60, hawaharibu vyanzo vya maji kule, wataalam wetu wasiwe wavivu wa kufikiria, ili washauri vizuri Serikali waende eneo husika wakaone kinachoendelea ndipo washauri Serikali, kwa sababu sasa hivi baada ya kutoa tangazo hilo Wakuu wa Wilaya kwa sababu wako kazini wanatetea vibarua vyao, Wakuu wa Mikoa, Watendaji wa Vijiji wameanza kuwanyanyasa wananchi. Sasa hata ile maana yote ya kupunguza kodi itakuwa haina maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *REA* nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliyepita kwa kuanzisha *REA* na Mheshimiwa huyu kuendelea kwa sababu leo nchi nzima inaenda kuwa nchi yenye nuru, taa zitawaka. Nishukuru kwamba katika Wilaya ya Kilolo vijiji vingi Mheshimiwa amenihakikishia tutapata na tutapata kwa sababu vyanzo vingi vya maji, vyanzo karibu vitano vya maji vinatoka Wilaya Kilolo, ndivyo vinavyojaza Bwawa la Kihansi, kwa hiyo lazima na mimi nipate ile ndiyo *royalty* au niseme ni *privilege* kwangu kwamba lazima tupate ili tuendeleo kutunza vyanzo vya maji. Sasa ili tusiwakorofishe hilo, naomba Mheshimiwa tushirikiane waendeleo kulima vile vinyungu vyao kwa kufuata taratibu ambazo zipo kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumza vizuri kabisa ni suala la barabara; Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Rais amehamia Dodoma, Wizara zimehamia Dodoma lakini asilimia 70 ya mbao zinazojenga hapa Dodoma zinatoka Wilaya ya Kilolo, lakini barabara ya Wilaya ya Kilolo iko *dhooful-hali*, Waarabu

wanasema *dhooful-hali* yaani iko katika hali mbaya. Kwa hiyo, ningepomba utusaidie tuweze kupata lami, ni kilometa kidogo ziko kilometa takribani 17 na Serikali sasa hivi ilikuwa na mpango wa kila mwaka inajenga kilometa moja, lakini...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto, nimekuongezea dakika moja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwahiyu naomba Mheshimiwa utufikirie ili tuweze kupata barabara ya lami lakini pia yale maboma ambayo yamebakia hayajamalizika, wananchi wamejitolea waweze kumalizia, Mheshimiwa tenga hizo fedha, uwezo huo unao. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwamoto. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian na baadaye Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mendrad Kigola.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Rais kwa maamuzi mazuri anayofanya kwa ajili ya nchi yetu.

Jambo la kwanza ninaloshukuru, nashukuru kwamba wale wenzetu wataalam Wakurugenzi wa Acacia wamekuja kuona ni jinsi gani wanaweza ku-*negotiate* na Serikali kulipa deni lao. Naomba niseme jambo, wakati mnakwenda kwenye *negotiation* hiyo, naomba wale mabwana walipe kwanza trilioni 35 mezani ili muweze kuanza mazungumzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mazungumzo yoyote yale walipe trilioni 35 kwanza zikae mezani halafu muanze kuchakata maneno, mengine mtazungumza na mtaendelea mbele kujua ni namna gani wanatakiwa kulipa lakini heshima ya nchi yetu kwanza, bajeti yetu ya Tanzania kwa mwaka mzima wailipe mezani *down payment* kuonyesha kwamba ni *commitment fee* kwa ajili ya kuilipa nchi yetu gharama zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niombe wale wataalam wetu waweze kwenda Ghana wajifunze ni namna gani wao kwenye madini walifanikiwa. Watengeneze ile ripoti waangalie ni namna gani wao wamefanikiwa vipi halafu sasa watakapokaa na hao wenzetu wajue ni *techniques* zipi za kuwatega na kutengeneza hili jambo likae vizuri ili siku nyingine lisijitokeze na nchi yetu iache kupoteza kwenye suala la madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Rais kwa kuonyesha jinsi gani amejit-*commit* katika hili, Rais kutoka nje kwenda Ulaya kila wakati sio zuri, hawa weupe na wao waje hapa wainame pale Ikulu wa-*bend* kwa Rais wetu, ametujengea heshima. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kwamba hawa watu na wao tunaweza kuwamudu, hawa watu kila siku ukienda kuwainamia wanafikiri sisi ni wajinga kwa sababu weusi. Sasa safari hii Rais ametujenga heshima, Bunge hili tumuunge mkono na tuhakikishe kwamba anatumutea kwa jinsi ilivyo, wawe wanakuja wanainama Ikulu, wana-*bend* wakimaliza wanapanda ndege zao wanaondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ameshamaliza kazi, sasa Bunge hili pekee ndiyo chombo pekee kinachoweza kumaliza migogoro iliyobaki. Tukubali tuungane tuwe wamoja tujenge nchi tukiwa *serious*, nje tucheke lakini ndani *we need to be serious* ili Tanzania ifike mahali inapotakiwa kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malipo yanayotakiwa kupatikana kwenye zile Halmashauri ambapo ile mikodi imekuwepo, wamechimba wananchi wetu wameendelea kuteseka, *levy*hawapati wanadai wenzao wanatimua vumbi. Kabla ya wataalam wetu kukaa kujadiliana na hawa watu wawe wameshalipa zile *service levy* kule kwenye yale maeneo, wakimaliza ndiyo warudi mezani ili waweze kuanza sasa mazungumzo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 93 wa kitabu hiki kuna Ranchi za Taifa. Ranchi hizi za Taifa zimekuwa

zinasakamwa sana lakini naomba niseme *National Ranching Company* ni eneo pekee ambalo leo watafiti wetu wa *Ph.D Program* kwenye *agriculture* na mifugo wanafanyia hapo, moja. Mbili, vijana wetu wa *field diploma* na *certificates* wanafanyia *field* hapo ndiyo jicho pekee unaloweza kutafiti na kuona ukaandikia mwanafunzi alama za *field* aliyoifanya kwenye maeneo yake vyuoni. Sasa tunaomba *NARCO* iongezewe fedha kutoka shilingi milioni 126 kwenda shilingi milioni 250 ili iweze kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kwamba wana-*develop production* ya mifugo mitamba kwa ajili ya maziwa hapa nchi.

(ii) Kukarabati maeneo ya majengo yao kwa sababu mengi yamechakaa kwenye ranchi zetu zote, ukiangalie zile *headquarters*, ukiangalia maeneo ya malisho, ukiangalia zile *paddocks*, kote kumechakaa. Tunaomba Serikali ilione hili lakini itambue haya maeneo kwa *beacons* kupunguza *invasion* ya vijiji na watu wanao-*cross* kutoka maeneo mablimali ili haya maeneo yawe *earmarked* yalindwe kwa sababu ya *training institutions* kwa ajili ya nchi yetu. (*Makofi*)

(iii) Kuna kiwanda kile cha Ruvu, tunazungumza habari ya mifugo kuwa mingi, tunazungumza habari ya kuvuna mifugo, lakini hakuna *meat industry* ambayo inaweza kupeleka wale watu wakauza mifugo yao pale. Tunaomba hicho kiwanda kijengwe haraka ili hiyo mifugo ipate mahali pa kuweza kuvunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la hii barabara yetu ya kutoka Handeni – Kibirashi – Kibaya – Singida; hii ni barabara ambayo inafungua fursa za kiuchumi kwenye ripoti ya kitabu chako hiki. Niombe barabara ya Iringa – Dodoma iko kwenye *final touches* mnamalizia, barabara ya Dodoma – Babati mko kwenye *final touches* mnamalizia, tunaomba *priority* iwe barabara hii kwa sababu zifuatazo:-

(i) Tunakwenda kujenga bomba la mafuta tumefanikiwa jitihada zimefanyika za Serikali, *along* hiyo barabara tunaomba basi hii barabara wakati bomba

linajengwa sambamba na hii barabara ijengwe kiwango cha lami ili kuruhusu mizigo kuweza kupitika kwa urahisi lakini hizo fursa tuzifungue. (*Makofi*)

(ii) Hiyo barabara peke yake inafungua ile Bandari ya Tanga kuweza kupitisha mizigo inayokwenda Rwanda, Burudi na Kongo. Ile barabara itapunguza msongamano wa Bandari ya Dar es Salaam ili Bandari ya Da es Salaam ipunguze *congestion* magari yatembee kupita kule ili yaweze kutoka na kwa haraka zaidi na kupunguza mizigo na nchi yetu ipate mapato kwa sababu ya kupunguza msongamano. (*Makofi*)

(iii) Ikitokea tukawa na *production* ya kutosha njia pekee inayoweza kupeleka mazao nje kwa maana ya Kenya wakiwa na *demand* ni njia ya Mombasa, lakini kwa sababu *area* ya *production* ni Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, njia pekee ni hiyo ambayo itapitisha yale mazao. Tunaomba hii barabara ifunguke kwa lami ili njia hizo ziweze kupitisha mazao magari yaende Mombasa kwa haraka na kuhakikisha kwamba hiyo barabara na gharama za nafuu kwa mkulima na mazao yetu wakulima wetu wakapate faida kutokea Mombasa, nchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna benki zetu za biashara. Mheshimiwa Waziri tunaomba ufumbe macho hizi benki kuna mahali zilikosea mmeziadhibu vya kutosha, tunaomba ufumbe macho uwasamehe; Benki za *CRDB* ziko zina *shake*, *NMB* ziko zina *shake* na hizi benki nyingine za biashara, tunaomba tunazidi kusisitiza wafungulieni nafasi wafanye kazi watu wetu waweze kukopa wafanye kazi, ili watu wetu waweze kulipa kodi na sisi tupate mapato kwa maana ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo muhimu la zaidi ninachoomba, Benki ya Kilimo hii ndio njia pekee tunayoweza ku-*access* wakulima 85% ya Watanzania, wakulima na wafugaji wanaofanya kazi, njia pekee ya kuwafikia ni njia ya Benki hii ya Kilimo, hii benki tunaomba ipewe mtaji. Hawa jamaa katika hizo shilingi trilioni 35 nilizozungumza

atakazoweka *down payment* mezani triloni tano peleka Benki ya Kilimo, ikae huko ndio wakulima wetu wakafutie jasho kwa kukopa hizo pesa wakafanye kazi za uzalishaji wakaweze kuinua kipato chao cha maisha kwa maana ya benki hii, kupitia hii benki. Hii benki ndio itakuwa njia pekee na mkobozi kwa ajili ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuko kwenye kanda kame, Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Simiyu, haya ni maeneo kame sana kwa nchi yetu. *Priority* iwe ni kuangalia ni namna gani ya kuhakikisha kwamba haya maeneo uanapata maji. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, *issue* kubwa ya maeneo haya ni uwezo wa kupatikana mabwawa makubwa mapana yenye uwezo wa ku-*support* watu na mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe tunalo Bwawa kubwa la Dongwa ambalo limeingizwa kweye programu ya mwaka 2017/2018, niombe hili bwawa litakapochimbwa lina *worth* ya shilingi bilioni 24; tunaomba mtusaidie hili bwawa lichimbwe kwa sababu hili bwawa linapeleka maji Wilaya ya Gairo, hili bwawa linapeleka maji Kongwa kwa maana ya Mkoa wa Dodoma, hili bwawa linapeleka maji Kiteto kwa maana ya Mkoa wa Manyara. Kwa sababu hili bwawa litakuwa kubwa sana mkilichimba mtakuwa mmeokoa wilaya tatu kwa wakati mmoja, lakini watu wengi wataweza kuondoka kwenye hiyo shida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nikuombe. Nasisitiza nakuomba ile milioni 50 ya kila kijiji, niombe utume wataalam wako wawili/watatu waje pale Kiteto waone tulivyo-*strategize* namna gani ya kuweza kutumia pesa kwenye *VICOPA*. Ile timu yako itakapoona inaweza kujua ni wapi pa kuingilia na zile pesa zikaweza kufanya kazi vizuri.

Sisi tunaamini na ninakuahidi na mimi ndio nitakuwa msimamizi na mimi ndio nitakuwa mdaiwa wa kwanza na ninaomba nisaini nikishindwa kurejesha hizo pesa nisigombee Ubunge mwakani na kadi yangu ya chama nirejeshe kwa ajili ya wale wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimeji-*commit* kwamba hizo pesa nitazirejesha kwa sababu nina uhakika kwa *nature* ya mazingira tuliyotengeneza ya *VICOBA* pesa ya Serikali haitapotea, wananchi kiuchumi watanyanyuka na sisi tuna uhakika wa kufanya kazi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mayenga na baadaye Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad wajandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipatia nafasi hii, ninakushukuru sana. Nianze kwa kum-*quote* Profesa mmoja wa Kenya ambaye anaitwa Patrice Lumumba, yeye alisema kwamba; "*Magufuli is the real deal.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wangu kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya kiasi ambacho amewafanya mpaka baadhi ya watu wameanza kuchanganyikiwa, wanahisi kama Mheshimiwa Magufuli amekaa miaka saba, wakati ndio kwanza ana mwaka mmoja na nusu. Na ninapenda kuwaambia kwamba hii ni mpaka 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ambayo leo hii nimeamua kusimama hapa, kwanza ni utendaji wake, lakini vilevile ni jinsi ambavyo ameshughulikia suala hili la makinikia. Suala hili la makinikia wananchi wangu, kwa mimi ambaye natokea Mkoa wa Shinyanga, wamenituma wanasema kwamba, katika vitu ambavyo utazungumza usiache kuelezea furaha kubwa tuliyokuwanayo sisi kwa jinsi ambavyo Rais ameweza kutusaidia, walau kuonyesha njia ambayo tunajua sasa tutafaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesoma magazeti, kuna gazeti moja nikasoma limeandika kwamba, kuna utafiti wa TWaweza, wanasema kwamba sijui umaarufu wa Mheshimiwa Rais Magufuli umeporomoka kwa sababu anapendwa na watu wa kada ya chini! Mimi nilikuwa nataka niseme jambo moja, wala hajakosea kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania ni maskini wale ambao ndio wanachukua asilimia kubwa asilimia 70. Kwa hiyo, kwa Rais kukubalika kwa watu asilimia 70 na kupingwa au kutokukubalika kwa ile asilimia 30 mimi naona ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mtu yeyote, kiongozi yeyote ambaye unajua unachokifanya hiki ndicho ambacho kinatakiwa kufanyika. Wewe hutakiwi upendwe na watu wachache ambao tena wengi mara nyingi wanakuwa ni mafisadi au wanakuwa ni watu ambao umewagusa kwa namna moja au nyingine, inatakiwa wewe upendwe na wale watu ambao ndio wengi.

Kwa hiyo, kwa Rais kukubaliwa na watu wa kada hii ya chini ndio hasa kitu ambacho tunakiunga mkono na kwa kweli, ndio kinaonyesha kwambam Rais wetu yuko imara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho wakati nachangia...

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa!

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga ya kwamba ni kweli kabisa utafiti

wa TWaweza umekuja kipindi ambapo Serikali yetu ilikuwa ikishughulika na watu wenye vyeti *fake* na mafisadi wengine. Katika hali ya kawaida watu wote hao lazima wachukie. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lucy endelea.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote mwenye akili timamu lazima apokee hiyo taarifa. Ni ukweli kabisa utafiti umefanyika *between* mwezi wa tatu na mwezi tano na ndiyo kipindi masuala ya vyeti *fake* yamesemwa masuala ya mafisadi yamesemwa kwahiyu hawa wenzetu hii asilimia 30 tunawajua ni wakina nani na hawa wa Makinikia na wao pia tunawajua na wenyewe pia wanajijua na wengine wako humu humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye kuzungumzia suala hili la makinikia mimi nina ushauri mdogo. Mtanisamehe sauti yangu kidogo inakwaruza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili la Makinikia mimi nilikuwa na ushauri kidogo biashara hii ni biashara kubwa sana, ninampongeza sana sana Profesa Mruma na pamoja na Profesa Osoro. Profesa Mruma nimekuwa naye kwenye *board* ya *Williamson Diamond* kwa kipindi cha miaka kama nane, kwa hiyo biashara hii ya *diamond* ninaifahamu kwa kiwango cha chake. Biashara hii inaitwa *holding business*. Biashara hii hata ikija kutokea duniani leo hii dhahabu zote zikaisha almasi zote zitakaisha kwenye mashino yetu aidha Afrika au sehemu nyingine yoyote. *Of course* sana sana ni Afrika. Biashara hii bado itaendelea kufanyika kutokana na *nature* ya hii biashara jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu nilikuwa naomba kushauri kwamba amekuja huyu *CEO* wa Barrick, lakini inatakiwa sisi kama Tanzania tukae naye. Mimi ambacho naomba kushauri naomba kwamba timu yetu ya Tanzania tufanye upembuzi mzuri sana wa watu wa kukaa na huyu mtu. Hawa wenzetu ni wazoefu sana wa hizi biashara ni *tycoon* wa hizi biashara, ni biashara ambazo zina

pesa nyingi sana lakini wenzetu wame-*deal* na hivi vitu maeneo mbalimbali kupita kiasi zaidi yetu sisi. Kwahiyo, lazima kwenye kuchagua watu wa kukaa nao meza moja lazima tuchague watu ambao vichwa vyao viko sawa sawa kikweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala hili la makinikia mimi nilikuwa naomba kuuliza Wizara ya Fedha, miaka ya nyuma *BOT* walitoa *wayver* kwa makampuni yote ya madini ambayo wanachimba hapa Tanzania ambayo yanatoka nje kwamba mnaruhusiwa kuweka pesa zenu nje. Ile *wayver* ilitolewa wakati ule Gavana akiwa Dkt. Balali mpaka sasa hivi *wayver* ile haijarudishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya haya makampuni walisema kwamba sisi tunataka tuweke pesa zetu huku nje kwa sababu hapa Tanzania hakuna mabenki ambayo ni *international*, lakini vile vile na sisi ambao ni wafanyabiashara ya hizi biashara. Sisi mikopo yetu tunaitoa huko nje. Sasa hawa watu sasa hivi *international bank* zipo nyingi hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kweli mimi nitaomba jibu hapo baadaye utakapokuja kuhitimisha uje utuambie ni sababu zipi zilizofanya mpaka leo hiki kitu kimekuwa kimya hakisemwi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tunavyoelewa kwamba pesa hizi zilikuwa zinawekwa hapa Tanzania, sisi Tanzania hapa tumekuwa tunalalamika bei ya dola imekuwa kubwa wafanyakabiashara wanalalamika. Pesa hizi zikiwa zinawekwa hapa tutafaidika hata mzunguko wetu wa pesa, urari wa biashara utaweza kuonekana na mzunguko wetu wa pesa itakuwa ni rahisi zaidi kwa sababu hata dola itachuka *at least* ita-*stabilize* vizuri kuliko ilivyo sasa hivi. Nilikuwa naomba jambo hili liweze kuliangalia kwa macho makali zaidi na kwa kweli ulifanyie kazi kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo nilikuwa nataka nizungumzie. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake dada yangu Dkt.

Ashantu wanafanya kazi nzuri sana ni watu ambao siyo waongeeji sana lakini kwa kazi wanapiga vizuri sana. Mmefanyaka kazi nzuri sana bajeti ni nzuri sana kusema za ukweli. Huwezi kuwa mtu mwenye akili timamu ukasema bajeti hii ina matatizo ina dosari za hapa na pale kwa sababu ni ile tu kwamba hatuwezi kumaliza matatizo yote kwa mara moja. Lakini hatuwezi kusema kwamba bajeti hii mbaya, bajeti hii ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwenye suala zima la kuwasaidia wajasiriamali wadogo tusiishie tu kwenye masuala ya *administrative* pamoja na *facilitation*, mimi nilikuwa naomba tu tujikite zaidi kwenye jinsi ya kuwasaidia hawa wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kukuambia ujaribu kumulika pale *Airport - TRA* ya kwako. Kuna matatizo makubwa sana wakati tumekaa tunazungumzia habari za kuwawezesha wafanyabiashara wadogo, Mheshimiwa Waziri wafanya biashara hawa wadogo wako akina mama, wako vijana wanaangaika wanakwenda nchi mbalimbali kuja kuleta bidhaa. Wanafanyabiashara ambazo mitaji yao ni dola 20000/30000 siyo pesa nyingi, lakini mtu analeta mzigo akifika pale *airport* anapata usumbufu wa hatari. Inakuwa inamkatisha mtu tamaa mpaka anaona kwa nini nimeanza kwenda. Anapata *visa* anamaliza anatoka anakenda huko nje kwenda kufanya hiyo biashara lakini akiingia hapa Tanzania anapata usumbufu kupita kiasi na rushwa pale imezidi. Mimi nakuambia kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie, Wizara ya Afya, uchumi ni afya, Wizara ya Afya nilikuwa naomba nitoe wazo Bunge hili liunde Kamati ya kushughulikia suala zima la Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeoza, haifai na kama ikiwezekana Mheshimiwa Rais na angekuwepo hapa leo Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani ningempa *message* kwa sababu yeye alijua jinsi ya kuzungumzia angeifuta kabisa. Ofisi ya Mkemia Mkuu inatakiwa ifanye *control* ya *chemicals* ambazo zinaingia Tanzania jambo

ambalo hawafanyi hata kidogo. Kuna kampuni inaitwa *TECHNO* imeingiza *chemical* kampuni moja tu. Imeingiza *chemical* ambazo ni nyingi wanaulizwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali hawajui hata idadi ya *Chemicals* ambazo zimeingizwa hapa Tanzania. Kemikali hizi zinatumiwa hospitalini, kwenye mashule yetu, wanafunzi wanakwenda kufundishwa kwa ma-*chemicals* ambazo zime *expire*, wanafunzi wanakwenda kufundishwa kwa *chemicals* ambazo nyingine siyo zenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu kama hivi tukiendelea kukaa tukivinyamazia, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara kwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali akakutana na hili jambo linatia aibu nasikitika tu kwamba sikupata nafasi ya kulizungumza kwa urefu wakati wa Wizara Afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Kigola baadaye Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Juma Kombo wajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika haya maeneo mawili Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali.

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri na *cabinet* nzima ya Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri mliyoandaa ambayo Watanzania tunaipokea kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwanza na masuala yanayohusiana na jimbo langu ambao kwenye jimbo langu tuna kazi kubwa ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ambayo mpaka sasa hivi Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi hatuna hospitali. Na bahati nzuri sana kwenye kamati zetu za madiwani vikao vya madiwani kwa pamoja tumesharidhia kwamba hospitali hiyo

itajengwa katika Kata ya Igowole na bahati nzuri kata ile wameshatoa eneo kubwa sana. Na eneo lile tutajenga Makao Makuu ya Halmashauri pamoja na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri katika fedha zake atusaidie katika ujenzi ule ambao kwenye *plan* tumeshauanza mwaka huu. Na kama halmashauri tumeshatenga shilingi milioni 100 ambayo inasaidia kuendeleza katika ujenzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naiomba Serikali watu wa Mgololo ambao walikuwa wanafanyakazi katika Kiwanda cha *MPM* watu wale walikuwa wanadai madai yao kati ya Serikali na Mwekezaji; bahati nzuri ile kesi ilienda mahakamani na imeisha na hukumu imetoka. Ninaomba kwa sababu wameshinda na wanatakiwa walipwe kama shilingi bilioni 18, naomba Serikali iwalipe wale wafanyakazi wamepata mateso ndani ya miaka karibu karibu kumi na moja, lakini hatima yake sasa hivi ilishafikia, sasa naiomba Serikali iweze kuwalipa ili wananchi wale watokane na matatizo ambayo wameyapata kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee masuala ya maji, tuna mradi mkubwa sana pale Sawala ambao ni mradi wa Serikali na ni muda mrefu sana, ni miaka sita sasa na mkandarasi tulikuwa tumempata. Yule mkandarasi alijenga matenki ya maji na *system* ya maji, lakini bado mradi ule haujaisha. Wananchi wa Kata ya Mtwango, Vijiji vya Sawala, Rufuna, Kibao wanapata shida sana ya maji. Na Serikali ilishaahidi kwamba mwaka huu inaweza kutimiza ahadi hiyona ikamaliza. Kwa sababu ujenzi ulianza, naiomba Serikali katika bajeti hii. Bahati nzuri nimeona kwenye bajeti mmetenga shilingi bilioni mbili basi itumike vizuri ili tuweze kumaliza mradi ule na wananchi wa Sawala waweze kupata maji vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali hii ya Mheshimiwa wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu amefanya vitu vingi sana ndani ya mwaka mmoja. Kila mtu anavijua na bahati

nzuri Wabunge wenzangu wamesema mara mbili mara tatu wanarudia rudia na mimi napenda nirudie; kwa mikono miwili nampongeza sana Rais wetu John Pombe Magufuli kwa kazi yake anayoifanya nzuri na sisi Watanzania wote kwa pamoja lazima tumuunge mkono na tumuombe kwa Mwenyezi Mungu aweze kufanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana, kuna watu wengine wanatoa maeneno ya kupinga. Kwanza Rais wetu ni *doctor*. Wewe huwezi kuwa ukampinga *doctor* bila *reason*, lazima uwe na *fact* za kumpinga. Sasa huyu anaonesha kwa vitendo kwamba tukisema tuorodheshe vitu alivyofanya ndani ya mwaka mmoja kwa mtu mwenye akili timamu lazima atakubaliana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo tu kile cha kuanza kusema elimu bure amefanya na tumeona, kitendo cha kusema kununua ndege amenunua ndege tumeziona kwa macho siyo kwa kuambia tu tumeona kwa macho. Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tuna tatizo kubwa sana ya madawati kwa kushauriana Wabunge pamoja na Rais wetu madawati amepeleka kwenye shule zetu na maswali tumepunguza. Mheshimiwa Rais alisema kwamba kujenga majengo pale *Universty of Dar es Salaam* wanafunzi walikuwa wanapata shida sana mabweni, amejenga. Sasa kuna watu hapa kama hatumpongezi hata Mungu atatushangaa. Lazima tumpe haki yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wakati anaingia madarakani alisema nchi hii ni tajiri, na sisi tunakubaliana alisema ina maziwa, ina mito, ina madini na akasema atadhibiti vizuri ile mianya ya ufisadi amefanya. Sasa mtu anaposisima anapinga maneno haya mazuri na anafanya kwa vitendo itakuwa ni wa ajabu. Juzi hapa tumeona katika ripoti sipendi sana nirudie Watanzania wengi sana tumeshangaa katika ripoti ile, na ripoti kweli imesikitisha kwamba fedha nyingi sana zilikuwa zinapotea lakini sasa hivi ameanza kudhibiti vizuri na bahati nzuri hata wale ambao alikuwa wanahusika na wafadhili wale wawekezaji wanakubaliana kwamba lazima wakae wazungumze lakini

sisi lazima tukubaliane nalo. Sasa isionyeshe tena watu wengine wanapinga kitu ambacho kinaeleweka. Na zile hela tukipewa tunajua kabisa tukisema kwamba Tanzania itafikia uchumi wa kati, tukilipwa zile fedha lazima uchumi wa kati tutafikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema nchi hii ni ya viwanda, viwanda haviwezi kujengeka kama hatuna fedha. Lakini bahati nzuri sana ukikusanya mapato ya kutosha unaweza ukapanga mipango na ikapangika na kama huna fedha huwezi ukapanga mipango ikapangika. Lakini Rais wetu anatusaidia kutafuta fedha/vyanzo vya mapato. Hicho ni chanzo cha mapato tayari kwa sababu kudai madeni, kuziba mianya ni sehemu ya chanzo cha mapato cha kukusanya fedha ili tuweze kupata fedha nyingi tuweze kuendeleza miradi yetu ambayo inatukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, juzi hapa amesema ujenzi *standard gauge*, na tukijenga kweli *standard gauge* Tanzania hii lazima uchumi utakuwa wa kati. Kwa sababu mizigo yote ambayo inasafirishwa kwa njia ya barabara ambayo barabara zinaharibika kila siku, mizingo mizito ikasafirishwa kwenye reli halafu wasafirishaji wa abiria tukasafiri kwenye barabara za kawaida. Barabara zitaweza kudumu wa muda mrefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nisizitize sana, Serikali imeahidi kupeleka umeme kila kijiji na kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini katika vijiji vyote 88 na bahati nzuri walisema watapeleka katika vitongoji vyote; wamesema watapeleka, naomba Serikali kwenye bajeti hii mwaka 2017/2018 ifanye kama ilivyokuwa imepangwa hili litatusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye masuala ya maji bahati nzuri Waziri wa Maji alisema tuandike *proposal* inahusiana na matenki yale nane ambayo yalikuwa bado hayayangwa ambapo lilikuwepo tanki la maji pale Igowole, Nyololo, Itandula, Idunda, Ihomasa na Sawala amesema atamalizia. Naomba afuate kama tulivyomwandikia

*proposal* ile ambayo tumempelekea ili wananchi wa jimbo langu la Mufindi Kusini ili waweze kupata maji bila matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niwashukuru sana wafadhili wanaonisaidia ufadhili maji katika Jimbo langu Mufindi Kusini akiwepo *Mr. Fill* na Mama Jully mpaka sasa hivi tunavyoongea wako Mufindi, wale wanatusaidia sana kuchimba maji katika Jimbo langu la Mufindi Kusini na sasa hivi wameniahidi kwamba watasaidia kuchimba maji katika shule za msingi na Sekondari.

Kwa hiyo, wawekezaji hawa mimi nawapongeza sana na nawaomba Wizara ya Maji iwa-*support* hawa wafadhili. Pale wanapohitaji msaada basi watoe msaada ili waweze kupata moyo kuendelea kutoa msaada wa maji katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naunga mkono bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja kwa sababu ni bajeti ambayo inaeleweka, kila mmoja anai-*support* na sisi tunawaomba kwa utekelezaji mwema, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigola, tunaendelea na Mheshimiwa Silinde baadaye Mheshimiwa Juma ajiandae na Mheshimiwa Omar Mgumba na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kupata fursa ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango. Sisi kama Taifa tuna tatizo kubwa sana la kiuchumi yaani kwa lugha nyepesi tunaweza tukasema tuna *economic crisis* na ndiyo tatizo la *ki-mindset* kwa watu wote. Tatizo tulilionalo kama Taifa tunataka kutatua matatizo ya kiuchumi kwa majibu ya kisiasa, hilo ndilo tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mapato kila siku yanashuka. Hata kule *TRA* mapato yanashuka mpaka

yameachwa kutangazwa sasa hivi. Lakini majibu yanayokuja ya kisiasa. Niseme tu kwamba hata bajeti ya mwaka 2017 ambayo sisi kama Wabunge hususan Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tumekuwa tukiita ni bajeti ya kihistoria. Mimi nasema ni bajeti ile ile kwa sababu hakuna jambo jipya ambalo unaweza ukajifunza kwenye hii bajeti. Na niseme tu kwa mara ya kwanza hii bajeti ina *tone* ya kisiasa yaani siasa ni nyingi kuliko hali halisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa huu utaratibu tutashindwa kupata suluhu ya tatizo na ndio maana siku mbili/tatu uliona *issue* ya makinikia sasa badala ya ku-*solve* kitaalam suala la makinikia linatakiwa li-*solve* kisiasa kwa hiyo ikawa sasa *politics* inatawala kwenye jambo ambalo linatakiwa watu walijadili kitaalam, hilo ndilo tatizo tulilionalo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye bajeti karibu kila kitu ni kile kile, nchi za wenzetu kwa mfano nchi ya Kenya wanapoandika bajeti kama hii wanakukambia bajeti yetu kwa mwaka huu itapunguza tatizo la ajira kwa kiasi fulani. Sisi bajeti yetu imezungumzwa yote, lakini haikuambi mwaka huu wa fedha 2017/2018 tutapunguza ajira kwa kiwango gani. Majibu ni yale yale tatizo la kiuchumi linatafutiwa suluhu ya kisiasa. Hilo ndilo tatizo tunalokabiliana nalo. Bajeti za wenzetu inapojadili namna ya kupunguza umaskini inaeleza vizuri kabisa, bajeti ya mwaka huu shilingi trilioni 31 kwenye bajeti ya maendeleo shilingi trilioni 11 tutapunguza umasikini kwa kiwango cha asilimia moja, wenzetu wanaeleza bajeti hii haielezi, hata mpango wenyewe haulezi hauende *direct* kwenye haya mambo. Tatizo ni lile lile, matatizo ya kiuchumi tunataka kuyatatua kisiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nchi nyingine Bunge halijadili madawati au sijui Halmashaluri yangu haina vyoo, hayo ni mambo yanayotakiwa yajadiliwe kwenye ngazi za Halmashaluri. Bunge tunatakiwa tuzungumze mambo makubwa sera za kiuchumi za kitaifa. Tuishauri Serikali namna ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, haya ndiyo mambo ambayo tunapaswa kuyajadili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja, mwaka 2014 Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Kinana alipokuwa Mbeya katika uwanja ule wa CCM akasema vizuri kabisa kwamba CCM tunapaswa kuwaomba radhi Watanzania kwa sababu tumewakosea sana. Haya maneno hata ukienda kwenye *YouTube* utaikuta ile hotuba ya Mheshimiwa Kinana alieleza vizuri sana kwa sababu alikuwa anajua na aliainisha kwa nini tuwaombe radhi Watanzania, sasa hapa hakuna kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii bajeti ya kihistoria, mimi nilijadili hapa namtafuta mtu maskini anaondokaje kwenye wimbi la umaskini, sioni, ndiyo zinaongezeka hizi sera. Wamekuja hapa na kufuta hiyo *annual motor vehicle license* ya shilingi 40 halafu unasema kwamba itaongeza tu shilingi bilioni 27.

## TAARIFA

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayeongea, nakubaliana naye kwamba Mheshimiwa Kinana alisema CCM itawaomba radhi Watanzania. Naomba nimpe taarifa kwamba radhi ambayo CCM imewaomba Watanzania na tumetekeleza kuomba radhi ni pale ambapo CCM imewaletea Rais ambaye hajapata kutokea, Rais ambaye ana uthubutu, jasiri na anawapenda Watanzania. Hakuna radhi pekee na kubwa kuliko hiyo ambayo CCM imeifanya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nimpe taarifa hiyo ajue kwamba tulishaomba radhi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde taarifa hiyo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kangi Lugola ni rafiki yangu wa karibu sana na anapozungumza kauli kama hizi unajua ukimjibu kisiasa atapotea kabisa kwa sababu nchi hii tumeshawahi kuwa na Rais Mwamba wa Afrika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sasa ukisema Nyerere unaweza ukamtoa kwenye hiyo reli unakuwa unakosea sana na siyo majibu mazuri. Akumbuke vizuri kabisa kwamba wapo akina Mkapa na Kikwete hatujawahi kupuza mchango wao pamoja na kwamba wamewahi kuwa na makosa. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Kangi ukatambua mchango wa wale wazee wengine maana yake wakikusikia wewe uliyekuwa unawaunga mkono leo ni kama vile unaona hawakuwepo, siyo jambo jema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida na uwepo wa Rais Magufuli, hatuna shida na jambo hilo lakini tunachokijadili, tunajadili ni namna gani Chama cha Mapinduzi kinavyotekeleza hizi sera ambazo hazitekelezeki. Unajua kuna kitu kimoja watu wanasema ametoka Kikwete amekuja Magufuli lakini wote wanatekeleza Ilani ya chama kimoja. Magufuli hatekelezi sera za kwake binafsi, anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ndivyo alivyofanya Kikwete, Mkapa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwezi kuwatofautisha Magufuli na Chama cha Mapinduzi ama Kikwete na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, jibu jepesi ni kwamba Serikali iliyokuwepo madarakani kwa kipindi chote ni ya chama kimoja ya Chama cha Mapinduzi tu. Kwa hiyo, makosa yote ambayo tunayataja yameletwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hicho ndicho tunachokijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu vizuri kwamba tunahitaji kujadili mambo ya msingi, kwa mfano Waziri wa Fedha hapa amekuja ameongeza shilingi 40, kuna watu wameeleza hapa wanaona kama vile ni kisenti kidogo lakini cha ajabu sisi tume-*question* pale unaongeza shilingi 40 kwenye mafuta ya taa, hebu Mheshimiwa Waziri wa Fedha nieleze kwenu Buhigwe ni gari gani inatumia mafuta ya taa

ama kuna Bajaji inatumia mafuta ya taa yaani unakuta hakuna majibu. Sasa *of all* kwenye ile lita moja ya mafuta ya taa bado Serikali inapata shilingi 425, tozo inatoka pale. Kwa hiyo, ukiongeza shilingi 40 maana yake mwananchi wa kijijini atalipa tena shilingi 465 nyingine, sasa hayo ni maswali ambayo tunapaswa kujijuliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda watu hawajui, kwa siku sisi kama Taifa tunatumia lita 8,300,000; lita 5,000,000 zinatumika kwenye mafuta ya dizeli, lita 3,000,000 tunatumia kwa ajili ya mafuta petroli na lita 300,000 yanatumika kwenye mafuta ya taa. Sasa jaribuni kukokotoa ndiyo mtajua kiwango ambacho kinakwenda kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuli-*propose* hata kwenye Kamati hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza kujua, tulisema ni bora ikaongezeka shilingi 50 kwenye mafuta iende kwenye maji ili wananchi wa vijijini wapate maji kwa sababu tatizo la nchi hii ni maji. Waziri akakataa akasema hiyo Sh.50 ikiongezeka itaongeza gharama ya mafuta na wananchi maskini watapata shida. Sasa leo kafanya kitu kile kile kwenye *angle* nyingine, sasa maana yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ni kutokuaminika, sijui ni kutojielewa au kijichanganya, hayo ndiyo mambo ambayo sisi siku zote tumekuwa tukiyapinga na tunalieleza Bunge lijaribu kuyaangalia. Ingekuwa vizuri sisi kama Bunge kwa umoja wetu tukakubaliana hapa kwamba pamoja na kwamba *motor vehicle* imefutwa, kwa kifupi siyo kwamba imefutwa isipokuwa tumebadilisha tu utaratibu wa kulipa. Kufuta maana yake hicho kitu hakitakiwi kuonekana mahali popote, ni kwamba tumebadilisha kutoka kulipa *direct* inakwenda kulipwa *indirect*, mfumo ni ule ule yaani kupunguza maumivu ya namna ya kulipa, haijafutwa. leleweke vizuri haijafutwa ila tumebadilisha utaratibu, kama ni kufuta unaoindoa pale.

Sasa hii shilingi 40 kama Bunge tuidhinishhe humu ndani iende kwenye miradi ya maji vijijini ili wananchi wote wapate maji safi na salama lakini ikienda huko huko itaishia tu kuwa

katika matumizi ya kawaida na mwisho wa siku haitafanya jambo lolote la msingi kwenye bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa angalia *trend* za bajeti zote za miradi ya maendeleo, kwa miaka nenda rudi bajeti za miradi ya maendeleo zimekuwa zikitekelezwa kwa kiwango kile kile chini ya asilimia 40. Sasa leo unapokuja na bajeti ya *tone* ya namna hii, mwakani sisi tutakuhoji tu vilevile. Maana yake hapa tumeficha uso wetu kwamba mwaka jana ni kama vile hakukuwa na jambo lolote lililofanyika lakini ukweli mwaka jana Wizara ya Fedha na Mipango mmefeli kwa kiwango kikubwa tofauti na matarajio ambayo tulikuwa nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri akajisifu akasema mimi ni ndiyo nimeingia, nisikilizeni, mambo yatakavyokuwa motomoto basi sisi tukakosa mpaka hoja, iwe ni Wapinzani na Chama Tawala tukakaa kimya tukasema ngoja tusingi kinachokuja, kilichotokea ni nini? Ni yale yale ambayo miaka ya nyuma yamekuwa yakifanyika, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo upo chini. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia kwa dakika moja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningepomba Serikali itakapokuja kuhitimisha ituonyeshe namna gani inaweza kutekeleza ile bajeti yake ya miradi ya maendeleo na iainishe vyanzo vipya. Kitu kingine tunakushauri chukua kwenye bajeti yetu mbadala, kuna vyanzo tumekushauri ikiwemo *Euro Bond*, *float Euro Bond* utapata karibu shilingi trilion 2.2 itakusaidia kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo. Ni ushauri wa bure ambao kama ukitaka unaweza kuchukua na usipotaka basi lakini kwa maslahi ya Taifa, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad baadaye Mheshimiwa Omary Mgumba na Kiteto Koshuma wajiandae.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia angalau kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza niwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutupa maelekezo mazuri na kutuongoza na kufikia kwenye ufanisi hadi leo tumo na tunaendelea kujadili katika Bunge hili la bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote humu tunakumbuka kwamba katika dunia hii nchi yoyote hata zile ambazo zimeendelea, tukielekea kwenye uchaguzi kitu cha mwanzo wagombea Urais wanachokijadili ni suala la kuongeza ajira kwa wananchi wao hususani kwa vijana. Pili wanajadili mkakati imara na madhubuti wa kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na msemaji aliyepita hivi punde, Mheshimiwa Silinde kwamba bado Mheshimiwa Mpango katika hotuba hii hajatuonyesha mkakati imara wa Serikali namna gani na kwa njia zipi ataondoa tatizo la ajira kwamba ni kwa namna gani atawaajiri vijana wa Kitanzania. Pia ni mkakati gani atakaoutumia katika kuhakikisha umaskini uliokithiri wa Watanzania unapungua kwa kiwango fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nina imani, suala hili mara nyingi linajitokeza hapa Bungeni, dada yangu pale Mheshimiwa Angellah Kairuki ana jawabu lake moja mara zote huwa analizungumza kwamba tunafanya uhakiki na baada ya kumaliza uhakiki tutaajiri vijana wa Kitanzania kwa kiasi fulani. Hebu wakati wa kufanya majumuisho, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Kairuki mje basi mtueleze ni lini sasa mtawaajiri vijana wa Kitanzania. Tunaenda kwenye mwaka wa pili sasa wa Rais John Pombe Magufuli bila vijana wa Kitanzania kupewa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kulizungumza ni mfumo wa kodi ambao tunauendeleza Tanzania. Miongoni mwa mambo ya Muungano suala la

Wizara ya Fedha siyo suala la Muungano lakini kodi ni suala la Muungano, kwa maana ya TRA. TRA ipo na inakusanya kodi kwa maslahi ya nchi nzima ya Tanzania kwa maana ya Zanzibar na Tanzania Bara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ni sahihi kabisa kwamba Zanzibar haifuati mfumo wa kodi wa kilimwengu kwa maana ya mfumo wa kuthaminisha bidhaa kwa ajili ya kodi, ni sahihi kwamba Zanzibar mfumo huu imeukataa na haiufuati. Haiufuati kwa sababu ya uchumi wake mdogo na *population* ya Wazanzibar ni ndogo, uchumi wa Zanzibar hauwezi kuulinganisha na uchumi wa Tanzania Bara. Tanzania Bara ina mchango mkubwa katika kufanya uchumi wa Zanzibar hauendi mbele kwa sababu ya mfumo mbovu wa kodi tunaouendeleza Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba suala la Mtanzania yeyote kutoka Zanzibar na kitu pengine cha shilingi milioni moja, kwa mfano *tv* akalipishwa kodi pengine laki moja na nusu Zanzibar, anakuja kutumia katika matumizi yake ya kawaida lakini anafika Tanzania Bara bandarini anaambiwa alipe *difference*, hii sio sahihi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ipo haja sasa ya kutafuta namna bora ya mfumo wa kodi ili kuhakikisha kwamba wajasiriamali wadogo wadogo wa Zanzibar wana-*enjoy* soko la Tanzania Bara. Leo anatoka mjasiriamali na mzigo wake mdogo wa shilingi pengine milioni moja au moja na nusu anakuja kutafuta riziki Tanzania Bara, lakini mzigo ule Zanzibar kalipia kodi pengine shilingi laki mbili, lakini akifika Tanzania Bara anaambiwa lipia tena laki mbili tukiwa na dhana eti ni *difference*, hii siyo sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena mdogo wangu mmoja alizungumza kule kwamba hata zile bidhaa zinazotoka ndani ya nchi, zinazozalishwa Tanzania Bara au Zanzibar lakini zikivuka kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar au kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara pia zinalipishwa kodi. Hata Afrika Mashariki tumeandaa utaratibu wa kusameheana kodi kwa bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya Afrika Mashariki, leo iweje ndani ya Tanzania moja tuna mifumo ya ajabu ya

kulipishana kodi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii siyo sahihi.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe ushauri tungekuwa na mfumo kwamba basi kama tuna *difference* tungekuwa na baadhi tu ya bidhaa au aina fulani ya bidhaa au thamani fulani ikifikia ndiyo suala la *difference* hapa mnalizingatia. Siyo sahihi kwamba mjasiriamali ana mzigo wake mdogo anakuja kutafuta riziki Tanzania Bara au mjasiriamali anaondoka hapa na mzigo wake mdogo kwenda Zanzibar tuwe na mfumo wa ajabu wa kodi ambao unadumaza upande mmoja wa Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, ni sahihi kwamba Zanzibar stahiki yake kwa mujibu wa sheria ni asilimia 4.5. La ajabu la kwanza, Mheshimiwa Mpango, ipo haja sasa kuufanyia *review* ya mfumo huu wa asilimia 4.5 na kuuangalia upya kwa sababu ulipitishwa miaka 40 nyuma. Uchumi wa nchi hizi unabadilika, lakini uchumi wa Tanzania Bara siyo uchumi wa Zanzibar, uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa bidhaa, uchumi wa Tanzania Bara umejitawanya katika mambo tofauti tofauti. Sisi kule Zanzibar hatulimi korosho, ufuta wala pamba, uchumi wetu unategemea bandari na bidhaa kutoka nje. Inapofika mahali kwamba suala la mfumo wa Tume ya Pamoja ya Fedha kutokuwepo...

## TAARIFA

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Na tujue kwamba...

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anazungumza anasema Zanzibar hatulimi korosho, lakini nimthibitishie tu kama Makunduchi tunalima korosho za kutosha.

Kwa hiyo, kama anataka aonane na Mbunge wa Makunduchi akaangalie korosho zilivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo unapokea hiyo taarifa?

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jawabu limetoka, tena limetoka kwa watu wa CCM kule nyuma kwamba Makunduchi wanalima korosho, lakini mbili/tatu za kula wenyewe, sisi tunazungumzia zao la biashara... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mpe elimu.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mattar ni rafiki yangu, umerogwa na nani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Tume ya Pamoja ya Fedha, nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapokuja kuhitimisha ulitolee majibu suala hili kwa sababu limechukua muda mrefu na hili ndiyo mwarobaini wa kukuweka wewe salama. Mheshimiwa Mpango nataka nikuhakikishie kwamba Wazanzibari hawatokuelewa bila suala hili kupata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mpango na tuna ushahidi kwamba hata hiyo asilimia 4.5 kwanza haifiki kikamilifu, ikifika ni asilimia 2.5 au 3.5 lakini pia hata huo mrejesho wenyewe hauendi. Mheshimiwa Mpango hadi sasa hivi Zanzibar inakudai mrejesho tena karibuni wa shilingi bilioni 30, Mheshimiwa Mpango umerogwa na nani? Yaani wewe huna haya wala aibu? Yaani Zanzibar leo inaikopa huna aibu? Kwa uchumi ule mdogo unakuja kuikopa Zanzibar? Hili Mheshimiwa Mpango inabidi uje utujibu ni lini fedha hii utairejesha Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nizungumzie suala la madini. Hili suala limezungumzwa kwa mapana yake. Mimi nataka kuzungumza kitu kimoja kwamba

ili Watanzania wawaelewe CCM na wafute ile dhana inayosambaa kwenye mitandao kwamba CCM ni ukoo wa panya, baba mwizi, mama mwizi na mtoto mwizi ni kwa waliohusika kupelekwa mahakamani. Hii ni kwa sababu viongozi walioshutumiwa wote walikuwa viongozi waandamizi wa CCM, majanga haya yanafanywa viongozi hao ni viongozi wakuu wa CCM, ni Mawaziri, Makatibu Wakuu na kadhalika, tuone sasa viongozi wale wanapelekwa mahakamani, wamechunguzwa na wamechukuliwa hatua stahiki kwa sababu tayari ripoti mnayoita ya kisayansi imethibitisha kwamba viongozi hawa wamehusika kwa namna moja au nyingine. Hapo ndiyo msemu huo tutau-*delete* sasa kwenye mitandao kama CCM ni ukoo wa panya kwamba baba mwizi, mama mwizi na viongozi wengine wezi. (Makofi)

**MHE. KHATIB SAIDI HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ameshamaliza Mheshimiwa Kombo.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa bado anaongea kwa hivyo ana haki ya kuisikiliza.

**MWENYEKITI:** Samahani, amemaliza basi. Mheshimiwa naomba ukae ameshamaliza, umechelewa kidogo tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Kiteto Koshuma na Mheshimiwa Oscar Mukasa wajandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya bajeti kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue fursa hii ya dhati kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetupa nafasi ya kufika siku hii ya leo ya Ijumaa

ndani ya Mwezi wa Ramadhani. Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua kubwa alizozichukua na kwa kutanguliza uzalendo kwa nchi yake, ameweka uzalendo mbele kuliko maslahi yake binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya utendaji wa Wizara ya Fedha kwa kuleta bajeti nzuri inayoonyesha mwelekeo halisi wa Taifa letu kwa mwaka huu. Pia kama walivyozungumza wenzangu ni bajeti ambayo imetoka kwenye mawazo ya Watanzania na Wabunge wenyewe. Nakumbuka tulijadili kwa kina Mpango ulipoletwa hapa Bungeni kama Wabunge tukapendekeza mapendekezo mengi na Serikali imeyapokea. Kwa hiyo, hilo tunapaswa kushukuru kwa sababu kama alivyosema Mbunge mmoja mwaka jana Serikali haikutusikiliza lakini mwaka huu hii bajeti ni ya kwetu, michango mingi ilitokana na michango tuliycopendekeza wakati wa Mpango. Kwa hiyo, tunajisikia kwamba tunai-*own* bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa wanasema kwamba unapomsifia mwizi msifie na yule anayemfukuza. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete aliyetuletea chuma kama alivyosema yeye. Alituambia mimi naondoka nawaletea chuma hiki ili kitekeleze pale nilipochoka mimi yeye aende kwa kasi zaidi. Leo ndiyo tunamuelewa Mheshimiwa Dkt. Kikwete kwamba chuma kinatema cheche. Tofauti yake na Marais waliotangulia huyu wa sasa ni mpole sana, kwa hiyo, ni vizuri akaongeza kidogo ukali na usimamizi wa karibu katika mali za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu tumechezewa vya kutosha. Nimuombe Mheshimiwa Rais, kwa sababu Serikali iko hapa, aende nje ya boksi, kama alivyosema mwenye ng'ombe amekwenda kumkagua Mchungaji kama ripoti anayomwambia ni sahihi, basi ni vizuri akaenda pia kukagua kwenye vitalu vya uwindaji. Huko nako mambo si mazuri kama tulivyokuwa tunasikia Mabunge ya zamani. Kwa kasi hiyohiyo aliyoifanya kwenye madini aende

na upande wa huko ili tujiridhishe kama taarifa wanazotupa wachungaji ni sahihi ili mwenye ng'ombe wake ajiridhishe kwa sababu kama alivyosema tulimchagua Watanzania kwenda kusimamia rasilimali hizi ili ziweze kutunufaisha wote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo makubwa sana huko vijijini, leo barabara za Kinole, Mkuyuni na Mkulazi hazipitiki. Tatizo kubwa hatuna rasilimali fedha ya kuweza kuzitengeneza, tunaambiwa maskini na tunadanganywa kwa misaada midogomidogo kumbe kama Taifa, kama anavyosema Mheshimiwa Rais, tuna uchumi mzuri na mapato mazuri. Kwa mwendo huu aliouanza naamini barabara zote hizo zitaweza kutengenezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, niende kwenye mchango wangu wa leo. Mchango wangu wa leo kitu cha kwanza naomba kuishauri Serikali, pamoja na bajeti nzuri na mipango mizuri na nia nzuri ya kuwatumikia Watanzania lakini nataka kupendekeza kwenye mfumo wetu wa bajeti. Sina tatizo na mfumo wetu wa *cash budget* kwa maana kwamba utekelezaji wake unategemeana na mfumo wa upatikanaji wa fedha, shida yangu kidogo iko kwenye huo utekelezaji.

Leo hapa kama Bunge tumekaa tumekubaliana au tulishakubaliana haya yaliyoletwa na Waziri kwenye bajeti kuu au bajeti za kisékta tunaamini ndiyo vipaumbele na ndiyo mipango ambayo wananchi wametutuma ili kwenda kuitekeleza. Kwa mfano inatokea wakati mwingine ile mipango tuliyokubaliana humu haikutekelezwa na mwaka wa fedha umekwisha, mwakani tukija ingawa tunaanza *zero* na ile mipango yote tuliyopanga msimu uliopita tunaisahau kama vile tulishaikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nataka nitoe mfano kabisa, nianze na mfano wa Kitaifa kabla sijaenda kwenye Jimbo. Kama Taifa katika kwenda kwenye uchumi wa viwanda au wa kipato cha kati tulikubaliana mwanzoni lazima tuongeze uzalishaji kwenye kilimo, kuboresha

miundombinu kwa miaka mitano iliyopita. Kwa bahati mbaya sana kilimo chetu hakikuboreka miaka mitano kuanzia 2010 mpaka 2015 lakini bado leo tulivyoanza 2015 Mpango wa Miaka Mitano tumeacha mambo ya kilimo, kuimarisha uzalishaji na kuongeza tija katika kilimo kama vile tulishakamilisha kila kitu na kilimo kinakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi upo katika kitabu chako mwenye Mheshimiwa Waziri umesema kabisa hali ya kilimo haiendi vizuri, kilimo kinashuka kutoka asilimia 2.3 kwenda asilimia 2.1. Nilitarajia kwamba sasa uje na mikakati mizuri ya kwenda kuimarisha kilimo lakini sasa tumekiacha kama vile tulishamaliza. Niseme kabisa Taifa hili tunategemea sana kilimo, zaidi ya asilimia 70 tunategemea kilimo, tukiacha sekta hii nyuma maana yake tumewaacha Watanzania wengi nyuma.

Kwa hiyo, kwa sababu hizi sekta nyingine ni *consumption*, ukizungumza afya na elimu zinahitaji fedha, lakini hii tukiimarisha ni sekta ya kuzalishaji, ni ya haraka sana kutubadilishia uchumi wa wananchi wetu mmoja mmoja lakini pia uchumi wa Taifa, itatuongezea mapato ya kigeni ili kuweza kuimarisha uchumi wetu kama Taifa. Pamoja na kwamba labda ilisahaulika, niishauri Serikali kuweka mikakati thabiti ya kuimarisha kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mapendekezo katika hili, miongoni mwa changamoto tunazozipata kwenye kilimo moja ni upatikanaji wa mbegu. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali kwa sababu *resource* ni ndogo tukawezesha vyombo vyote vya usalama, hususan Magereza tukatafuta mashamba yao kwa sababu wanayo ya kutosha tukawekeza bwawa kubwa la umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha kisasa ili tuzalishe mbegu. Tuanzie hapo tu, tuzalishe mbegu ili tuondokane kabisa na tatizo la upatikanaji wa mbegu nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ili kuimarisha uzalishaji ni vizuri kuingia mikataba na makampuni wazoefu wenye teknolojia, wenye ujuzi, wenye ufahamu katika mazao kwa ajili ya kuzalisha miche kwa ajili ya mazao ya biashara. Kwa

mfano, kama wanavyofanya Naliendele kwa ajili ya korosho, tutafute sasa watu wenye uzoefu ili wazalishe miche kwa ajili ya kahawa, kokoa, mazao yote ya muda mrefu na kuigawa bure kwa Watanzania yaani ruzuku ipelekwe kwenye kuzalisha tu hiyo miche halafu tuigawe bure kwa Watanzania ili tuweze kuongeza uzalishaji mkubwa sana katika mazao ya kilimo ili tuondoke hapa tulipo kwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema tatizo kubwa la mfumuko wa bei ni suala la ukame na upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, ni vizuri mngeweka sasa mikakati ya kuondokana na kukabiliana na ukame na ukosefu wa mvua kwa kujenga mabwawa na majosho kwa ajili ya wafugaji na mambo yote ambayo yanahusiana na maji, hatuwezi kujenga nchi nzima lakini tunaweza tukaanza na sehemu fulani. Mheshimiwa Waziri anafahamu tuna Bwawa la Kidunda ni la muda mrefu sana. Kwa nini tusingeanza na hili ili liweze kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kulisha Taifa hili na tuwe na uhakika wa chakula, malighafi na ajira kwa watu wetu, hususan wanaoweza kuishi vijijini na sehemu nyingine zipo fursa nyingi za kutengeneza mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu katika suala la leo, nikupe mfano mwingine kuhusu mfumo ule wa bajeti. Kwa mfano, mwaka jana mlitutengea shilingi bilioni 17 kwa ajili ya kulipa fidia kwa watu waliopisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda pamoja na kutengeneza ile barabara ya kwenda Kidunda. Hata hivyo, mpaka leo hata senti tano haijafika na tumebakiza wiki mbili tunamaliza mwaka. Kwenye bajeti mmetutengea shilingi bilioni 1.5 kwa Bwawa hilo la Kidunda wakati fidia tupu inadaiwa shilingi bilioni nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wiki mbili hizo zikiisha tutawaambia nini wananchi maana mnatusababishia ugomvi mkubwa sana na wananchi Mheshimiwa Waziri kwa kushindwa kutekeleza bajeti kama ilivyopangwa. Kwa sababu sisi kama wawakilishi wa wananchi tukitumwa hapa

tumetumwa na wananchi kuja kuleta shida zao baadaye tukirudi tuwaeleze Serikali imewapangia kuwafanyia nini. Kama mwaka jana nimewaeleza wametengewa shilingi bilioni 17 kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo pamoja na kulipwa fidia yao. Mwaka jana nimewaambia watu wa Kinole wametengewa shilingi milioni 105 kwa ajili ya kutengeneza barabara yao, barabara ile haijatengenezwa mpaka leo na leo kuna ugomvi mkubwa sana inaonekana kama vile Mbunge hawasemei wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu utakwisha na mwakani hata nikimdai Meneja wa *TANROADS* atasema haipo kwenye bajeti, nikimdai Meneja wa Maji anasema kwamba haipo kwenye bajeti mwaka huu Mheshimiwa tumetengewa shilingi bilioni 1.5, kwa hiyo haiwezekani kutekeleza tsubiri mwakani. Nikuombe sana, ni vizuri muangalie mfumo huu wa bajeti ili uendane na hali halisi kwa sababu yale mnyotuaambia hapa tunakwenda kwa wananchi kuwaeleza, sasa isije kuonekana kama sisi viongozi tunasema uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii tena kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana, Mwenyezi Mungu ampe uhai mrefu na uzima Rais wetu ili aweze kuonesha maajabu ndani ya nchi yetu, ndani ya Afrika na ndani ya dunia. Rais Trump alisema Waafrika wengi tatizo tuna Marais wezi, lakini Mheshimiwa Dkt. Magufuli amemhakikishia hakuna Marais wezi, tuna Marais wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Omary Mgumba. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma baadaye Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu wajiandae.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze

kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu katika kujadili bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kunijalia afya njema, uwezo na hekima katika kujadili majadiliano mbalimbali katika Bunge hili. Leo hii napenda sana nimuombe Mwenyezi Mungu anijalie hekima ili niendeleo kuishauri Serikali yangu ambayo ni sikivu na naamini kabisa kwamba watanielewa na kufanyia kazi maoni yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza, naomba kidogo nikosoe jambo moja. Kuna Mbunge amemaliza kuchangia akasema kwamba Serikali ya CCM ni wezi, lakini katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8 inaonesha ni jinsi gani Serikali inavyomilikiwa na wananchi kwa maana kwamba watendaji wanafanya kazi kwa niaba ya wananchi. Kwa hiyo, itakuwa si sahihi nikiendelea kuruhusu Mbunge mmoja kusema kwamba Serikali ya CCM ni wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hilo ambalo yule Mbunge ametoka kuchangia akasema Serikali ni wezi liweze kufutwa kwenye *Hansard*. Kwa sababu Wana-CCM siyo wezi na ndiyo maana mara kwa mara Serikali ya CCM imekuwa ikijikosoa pale ambapo inaona imekosea, bali ni mtendaji mmojammoja ndiye anayekosea, hivyo huwezi ukasema kwa kutumia ule msemu kwamba samaki mmoja akioza wameoza wote, anashughulikiwa mtendaji mmojammoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba tena niende katika kipengele kingine cha kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Ninayo furaha kubwa sana kwa siku ya leo kumpongeza Rais wetu. Kwa sababu gani ninampongeza Rais wetu? Rais huyu ni fahari ya Watanzania, ni fahari ya Wanachama wa Chama cha Mapinduzi, ni fahari ya mataifa mbalimbali na ni fahari kwa dunia nzima. Mambo ambayo anayafanya Mheshimiwa

Rais Dkt. Magufuli anastahili kupewa pongezi yeye kama yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge siku moja alidiriki kusema kwamba Mheshimiwa Magufuli alisema ni Serikali ya Dkt. Magufuli, hapana, siyo kwamba alisema chagua Serikali ya Magufuli bali alitaka tumuamini yeye kama mtu lakini si kwamba Serikali ni ya kwake, Serikali inamilikiwa...

## TAARIFA

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye niliyesema kwamba Serikali hii ya Magufuli. Kabla ya Rais kuwa Magufuli, katika wagombea wa CCM akina Lowassa, kabla ya kina Lowassa hawajatolewa asimame mmoja aliyekuwa anamuunga mkono Magufuli, asimame mmoja tu hapa. Kwa hiyo, hii ni Serikali ya Magufuli siyo ya CCM. Waongo, wanafiki tu ninyi nyote, nyote mliimba tuna imani na Lowassa, mliimba ninyi nyote wahuni ninyi. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Magufuli kweli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto, naomba uendelee tafadhali.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Bwege kwa kweli siwezi kuikubali na ndiyo maana nilianza kwa utangulizi wa kuongelea Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lowassa alikuwa ni mtendaji na atawajibika kama mtendaji. Mimi sitaki kuyahesabu yaliyopita, nasonga mbele na haya tuliyonayo sasa hivi. Ndiyo maana nikasema siku ya leo naomba Mungu aendelee kunipa hekima na naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, kwanza naomba unilindie dakika zangu kwa sababu nilizitenga kwa makundi, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli sisi wana CCM tunayo kila sababu ya kujivunia. Hata mimi mwenyewe naposimama hapa siku ya leo nasimama najidai kwa sababu tumemchagua Rais, tukamnadi sisi wenyewe, tukatembea kijiji kwa kijiji, nyumba kwa nyumba, shuka kwa shuka tukitafuta kura za Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Leo hii siwezi kuona aibu kuivaa nguo ya kijani kutembea barabarani kumuongelea Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa sababu mambo anayoyafanya naamini kabisa hakuna Mtanzania ambaye angeweza kuthubutu, mambo aliyoyafanya ni ya msingi sana na ni mazito na yanawagusa wanyonge. Ndiyo maana katika michango yangu ndani ya Bunge hili nimekuwa nikimtaja Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwamba ni Rais ambaye yuko tayari kuwatumikia wanyonge na napoona kuna kitu ambacho kinawakandamiza wanyonge nimekuwa nikijaribu kuishauri Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudi katika michango ya bajeti. Naomba kuchangia suala la Deni la Taifa. Katika kitabu chake Waziri wa Fedha na Mipango ameongelea suala zima la ustahimilivu wa Deni la Taifa. Mimi sipingani na hilo lakini nachokisema ni kwamba Deni la Taifa kama ni stahimilivu waendeleo kukopa lakini Deni la Taifa linapokuwa linaongezeka halafu Watanzania wanaendelea kuishi katika maisha ya umaskini, tunaona hakuna sababu ya kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali jambo moja, tunapokopa na tunapoendelea kuongeza Deni la Taifa kama anavyosema kwamba bado ni stahimilivu, liende likawekezwe kwenye miradi ambayo inaweza ikawasaidia Watanzania. Kwa mfano, kuna matatizo ya maji mpaka leo kila Mbunge akisimama humu ndani analalamikia suala la maji katika jimbo lake, Mkoa wake na Wilaya yake. Sasa najiuliza swali, hivi Deni hili la Taifa ambalo linaongezeka siku hadi siku halafu wananchi bado wanaendelea kulia na maji, mnasema kwamba tunamtua mwanamke ndoo kichwani lakini katika hili bado hatujafaulu. Naomba

niendeleo kuishauri Serikali iweze kuzingatia mambo haya ya kurekebisha masuala mazima ya miradi ya maji. Kuna miradi mingi sana ambayo inaanzishwa lakini haikamiliki. Kwa hiyo, utaona ni jinsi gani Deni hili la Taifa bado halijawa la kuwanufaisha wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo Mkoa wa Mwanza. Kwa mfano, kuna mradi mkubwa wa maji kule Ilemela ambao ulikuwa unafadhiliwa na *World Bank*, mradi huu ulikuwa ni wa vijiji kumi lakini katika hivi ni kijiji kimoja tu cha Kayeze ambacho ndiyo kimepata maji, lakini vijiji vingine kama vile Nyafula, Kasabangu, Nyamadoke, Kabangaja, Sangabuye na kwingineko kote huko bado hawana maji. Ukiangalia pale Mwanza tumezungukwa na Ziwa Victoria, fikiria wale tu ambao wanaishi kandokando ya Ziwa Victoria wanaenda kuchota maji machafu ina maana Serikali imeshindwa kuwasogezea maji katika nyumba zao. Naomba sana Serikali ilianganalie suala la usambazaji wa maji katika vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika mradi ambao unatokea Misungwi kuelekea Kahama na Shinyanga umeviacha vijiji vya Nyangomango, Ilambogo na Ibinza. Siku moja Mheshimiwa Mbunge wa Misungwi hapa aliongea kwa uchungu sana na watu hawakumuelewa lakini mimi nilimuelewa kwa sababu nimepita katika vijiji vile na nikaona tatizo lililoko pale. Hatutaweza kuvumilia hali hii ambapo miradi ya maji inapita halafu inaviacha vijiji vile vya kandokando pale vyote havina maji halafu mnaona maji yanapita kutoka Ziwa Victoria yakienda sehemu nyingine halafu vile vijiji vinakosa maji. Naomba sana Serikali iweze kujirekebisha katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia upande wa Sengerema kuna mradi mkubwa ambao unatakiwa kusambaza maji lakini bado kuna vijiji ambavyo havina maji, kwa mfano Kijiji cha Kwang'washi na chenyewe hakina maji, wananchi kila siku wanalia, akina mama wanaamka wanatembea kilometa zaidi ya 20 kwenda kutafuta maji. Kwa kweli kama tuko tayari kusaidia wananchi wetu ambao ni

wanyonge, hebu tuwasaidie katika kutatua matatizo yao ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu sijaona suala la kilimo. Kama tunavyofahamu asilimia 75 ya Pato la Taifa inachangiwa na kilimo. Sioni ni kwa sababu gani tunashindwa ku-*link* bajeti kuu ya Serikali na suala zima la Kilimo. Naomba Waziri wa Fedha na Mipango atakaposimama atueleze sisi Waheshimiwa Wabunge suala la kilimo analiweka vipi, tunaelekea wapi, kwa sababu kama tunaenda kwenye uchumi wa kati au uchumi wa viwanda tutafikaje kwenye uchumi wa viwanda wakati kilimo hakitiliwi maanani. Naomba sana Serikali iweze kutilia maanani suala la kilimo kwa sababu kilimo kitaweza kusaidia wananchi wengi kuajiriwa kwenye mashamba lakini hatimaye pia kuondokana na suala zima la njaa, kwa sababu tunaona vijiji vingine wanakufa na njaa na hili hatuwezi kuacha kulisemea kwa sababu wananchi hawatatuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee hali ya uchumi. Kwa masikitiko makubwa sana nilipokuwa nikisoma kitabu cha fedha na mipango, Waziri anasema kwamba hali ya uchumi ni nzuri. Kusema ukweli hali ya uchumi si shwari, hali ya uchumi ni mbaya sana, wananchi wanaishi maisha ya kimaskini, hata hajui kama atapata hata mlo mmoja, si tu milo miwili au mitatu, hajui hata kama atapata mlo mmoja. Naomba Serikali inapokuwa inaandika vitu ijaribu kuangalia maisha ya Watanzania kwanza yako vipi. Inawezekana wataalamu ambao wanaandika hivi vitabu wao wana maisha mazuri, kwa hiyo, hawafikirii wale Watanzania ambao wana maisha mabaya, ambao maisha yao hayako katika hali nzuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Oscar Mukasa na baadaye Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Upendo Peneza wajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia namshukuru Mungu kwamba amenipa fursa na ametupa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yake kwa kazi nzuri, nasema ni kazi nzuri kwa vigezo vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ukisikiliza hotuba yake hata ukisoma kwa kiwango kikubwa utakuta mambo mengi ambayo ameyasema mule ni mambo ambayo sisi wenyewe Wabunge tulishauri hapa. Tuliwapigia kelele sana mwaka jana, tukayapigia kelele sana humo katikati na nataka kusema mimi ni mmoja ya watu ambao amethibitisha kwamba nilikuwa nakosea, Waingereza wanasema *amni-prove wrong*. Mwaka jana nilitoka hapa na fikra kwamba Mheshimiwa Mpango hasikilizi, lakini mwaka huu *amni-prove wrong* anasikiliza, kwa hiyo, hicho kigezo cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo cha pili, kwa sababu amesikiliza, utagundua kwamba mengi aliyoyasema kwa kweli hata wasikilizaji, wananchi wetu huko vijijini kabla hata hawajaona habari ya utekelezaji itakuwa vipi kwa sababu hiyo ni hatua nyingine lakini angalau kwa hatua ya kwanza wanaona bajeti hii ni ya kwetu. Akishindwa kutekeleza hiyo ni habari nyingine sisi tutamwambia kama Wabunge lakini kwa hatua ya kwanza wanaona kabisa hii bajeti ni ya kwetu sisi ndiyo walengwa. Kwa hiyo, nampongeza na timu yake kwa mambo hayo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanasema kufanya vizuri haitoshi tunatakiwa kufanya vizuri zaidi. Yapo mambo ambayo bado sikubaliani na Mheshimiwa Mpango. Maisha

ya binadamu ukijaribu kuweka vipaumbele ni jambo gani la kwanza ambalo hilo lisipokuwepo uhai wake hautakuwepo, la kwanza ni hewa ya kupumua ambayo kwa bahati nzuri ama mbaya hiyo haipo kwenye bajeti.

Pili, ni chakula na la tatu ni maji yaani ni afadhali Watanzania wote tutembeu uchi hapa lakini tuna maji na tuna chakula. Hivyo ndiyo vipaumbele kwamba hewa ndiyo ya kwanza, huwezi kuongelea nguo wala viwanda kama hakuna hewa, imechafuliwa, ina gesi yenye sumu haiwezekani...

## TAARIFA

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msemaji anayezungumza sasa hivi kwanza akae halafu hili la kusema kwamba ni bora Watanzania wote twende uchi, lakini maji ndiyo yapatikane sisi siyo wanyama. Mwenyezi Mungu ametutofautisha kati yetu na wanyama. Atafute maneno mengine ayafute hayo kwamba Watanzania twende uchi hilo hapana. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Haya, tuendeleo Mheshimiwa Mpango na mambo ya msingi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, kwanza kabisa ni hewa ambayo haipo kwenye bajeti. Pili, chakula na tatu ni maji halafu mengine yote pamoja na umuhimu wake yanafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama ukurasa wa 8 mpaka wa 9 wa Kitabu cha Hali ya Uchumi, anasema hivi Mheshimiwa Mpango kwamba Pato la Taifa lilitarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 lakini limekua kwa asilimia saba badala ya 7.2 na akafafanua kwamba ziko sekta ambazo ndiyo

zimechangia tusifikie lengo hilo na sekta mojawapo ni kilimo ambayo ilitarajiwa kuchangia kwa asilimia 2.9 lakini ikachangia kwa asilimia 2.1, amesema vizuri pale. Ukiangalia vipaumbele vya bajeti sasa kilimo kimeguswa kwenye shamba moja la miwa. Sasa mimi nikakaa najiuliza pamoja na kwamba sipingani na shamba la miwa kwa sababu nadhani anakwenda kujibu ile habari ya ukurasa fulani hapo hapo anasema, moja ya mazao ambayo tullilazimika kuleta kwa wingi kutoka nje ya nchi mwaka jana ni sukari, nafikiri anakwenda kujibu hilo, lakini nilitarajia kilimo kwa ujumla wake kipate kipaumbele. Hata kama huwezi kuwa na majibu ya matatizo yote lakini lazima kwenye vipaumbele vya Kitaifa vilivyo kwa ngazi ya bajeti tofauti na ngazi ya Wizara moja moja lazima kilimo kitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukurasa wa 11 wa hali ya uchumi pia anasema; mfumuko wa bei wa mwezi wa Aprili, 2017 ulikwenda juu ya wastani ya mwaka wa mfumuko wa bei, ukaenda 6.4 badala ya 5.2 ambayo ni wastani kwa sababu kulikuwa na hofu ya upungufu wa chakula kwa sababu watu waliona msimu wa mvua unachelewa. Hii yote inakuonyesha namna gani tunahitaji kujikita siyo tu kwenye kilimo tunapaswa kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kama unavyofahamu hatujawahi kutumia *potential* yetu ya kilimo, uwezo wetu wa kilimo cha umwagiliaji kwa kiwango kinachostahili. Kwa hiyo, nilitarajia kwenye vipaumbele vya ngazi ya Kitaifa, vya ngazi ya bajeti kuu siyo ngazi ya sekta moja moja habari ya angalau kilimo cha umwagiliaji kionekane ni kipaumbele. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango nimeshangaa sana kutoona kipaumbele cha kilimo zaidi ya shamba moja la miwa kwenye bajeti kuu, naomba ufanye mapitio kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya maji sasa ambayo imepelekea mtu akatoa taarifa hapa, sina matatizo na taarifa hiyo lakini mimi nilikuwa najikita kwenye mantiki kama mantiki umeiona nakushukuru, kama huioni bahati mbaya nitakuelekeza baadaye. Biharamulo leo tunavyozungumza, katika vijiji 80 vya Wilaya ya Biharamulo huwezi kuhesabu vijiji zaidi ya 15 au 16 ambavyo ukienda kuongea ajenda

nyingine tofauti na maji watakusikiliza. Leo Mji Mdogo wa Kabindi pale mpaka watu jana nilikuwa nazungumza nao wanapanga kufanya maandamano wanasema kwamba sasa hali ni mbaya. Tunaomba Mheshimiwa Mpango hebu weka hii habari ya maji, Wabunge wamesema mengi sitaki kurudia, habari ya maji hebu tuifikirie Kitaifa na kimkakati. Hii habari ya kuiacha kwamba ni suala la kudonoadonoa kila Mbunge anakwenda anakimbizana na Waziri wa Maji anampa msaada kimradi kimoja, kisima kimoja na vitu kama hivyo haitatufikisha. Kwa taarifa za kitafiti zilizopo habari ya kutafuta maji inachukua zaidi ya asilimia 40 ya muda wa Watanzania wa kufanya shughuli nyingine za uzalishaji mali kwa sababu wanahangaika kwenda kutafuta maji ya kutumia nyumbani kwao na kwa ajili ya maisha ya kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo kwenye hotuba yake ukurasa wa 31 na yeye aliorodhesha pale vipaumbele akavitaja, cha kwanza anasema, kuboresha mfumo wa utafiti wa utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau, kuimarisha usimamizi kabla na baada ya mavuno, kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa pembejeo, zana za kilimo na vitu kama hivyo, kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo, kuratibu na kuboresha matumizi endelevu ya ardhi, kuunda na kupitia sera, kuwezesha uwezesaji wa sekta binafsi na kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini. Nililazimika kwenda huku maana yake nilidhani inawezekana kwenye bajeti kuu tumesahau hii habari ya umwagiliaji kwa sababu ndiyo itatutoa, tunazungumzia hapa habari ya ukame mpaka mfumuko wa bei unapanda nikasema ngoja nirudi kwa Waziri wa Kilimo inawezekana yeye anaongelea umwagiliaji lakini na yeye hasemi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna tatizo na tumuombe Waziri wa Fedha, uzito wa suala la kilimo kwa upana wake uliotolewa hapa hautoshi. Kwa hiyo narudia, moja, suala la muhimu kabisa kwa binadamu ni pumzi ambayo wewe huna mamlaka nayo kwenye bajeti isipokuwa kama itatokea uchafuzi wa hali ya hewa inawezekana ikakuhusu.

Pili, ni chakula tunaomba utoe uzito unaostahili kwenye chakula na tatu ni maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati unasimama hapa kutujibu tunaomba utuambie mustakabali wa kilimo kwa upana wake na tusingahau hii ndiyo sekta ambayo inaajiri Watanzania angalau asilimia 65. Ninyi Kitaifa mnaongelea asilimia lakini Biharamulo unaongelea asilimia 90 mpaka 92 wote wanajihusisha na kilimo. Kwa hiyo, tunaomba utakaposimama hapa Mheshimiwa Waziri utuonyeshe ni namna gani unaingiza suala la maji na kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye habari ya makinikia maana naona kwa wiki hii usipoongelea makinikia unaweza kuwa upo tofauti kidogo kwa sababu kuna *statistical normality* na *ideal normality* kwamba ukienda kule kwa watu wafupi Congo sijui wanaitwa kabila gani, wote ni wafupi wewe ni mrefu. *Statistically* pale wewe ni *abnormal*, wao *statistically* ni *normal* kwa sababu ndiyo wengi ila *ideally* wewe uko kawaida wao wako *abnormal*. Kwa hiyo, lazima niongelee makinikia na mimi nitayaongelea kwa sentensi chache tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vita kuna mambo kadhaa lakini makubwa matatu ambayo mimi nataka kuyasemea. Moja, kuna lengo (*goal*) yaani mnalenga nini, mbili, kuna mkakati (*strategy*), mnajipangaje kwa ujumla na kwa upana wake na tatu kuna *tactics* (mbinu). Sasa kwamba lengo letu ni kushinda hii vita ya kwamba tumenyonywa miaka mingi siamini kama kuna Mtanzania ambaye hana lengo hilo, lakini kwa ngazi ya mkakati hiyo ndiyo ngazi ambayo yuko Rais. Rais anachotaka kufanya, mimi nimemsikiliza, nimemfuatilia unamuona huyu mkakati wake ni kutafuta namna gani siku tukikaa meza moja na hao tushike upande wa mpini na wao washike makali au angalau tuwe na meza moja, ndiyo mkakati alionao ukimsikiliza na ukimfuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiwasikiliza wengine wanaochangia unaona kwamba kila mmoja anataka kuchangia kwa ngazi ya *tactics* (mbinu) ambalo ni jambo

zuri lakini kwa bahati mbaya mtu anataka kuchangia kwa ngazi ya *tactics* (mbinu) lakini anafikiri ili mbinu yake ionekane imesaidia ni lazima abomoe mkakati, sasa hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana falsafa wanasema, ukiwa na mkakati mzuri bila mbinu utakuwa na mawazo mazuri bila utendaji, lakini ukiwa na mbinu nzuri bila mkakati ni vurugu. Ndiyo maana hapa unaona mwingine anasema haya tunajenga nyumba, wewe bomoa tofali hili badala ya wote kusema jenga. Kwa hiyo, tutambue kwamba lengo letu ni moja, Rais yuko kwenye ngazi ya mkakati...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia kwa dakika moja Mheshimiwa Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko kwenye ngazi ya mbinu, kwa hiyo, kila mtu atoe mchango wake wa mbinu ambayo hailengi kubomoa mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya mimi kuungana na Wabunge wenzangu katika kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya. Sote tunafahamu kwamba Rais wetu Magufuli ni binadamu kama binadamu wengine. Kila binadamu anapofanya jambo jema anapenda kupongezwa na kwa kufanya hivyo tunampa nguvu katika kutekeleza majukumu

yake. Naomba niungane na Wabunge wenzangu lakini niungane na wananchi wote kwa ujumla, kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya na niseme binafsi naendelea kumuomba kwa Mwenyezi Mungu ili afanye kazi yenye kuleta tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Halmashauri. Kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa ALAT-Taifa. Kama tunavyofahamu kwamba Mkutano wa ALAT-Taifa unaunganisha Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya, Wakurugenzi lakini wamo na Wabunge kutoka katika kila Mkoa. Mimi ni Mbunge ambaye nawakilisha ALAT-Taifa kutoka kwenye Mkoa wangu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu kupitia kikao ambacho kilifanyika tarehe 22 - 24 Septemba, 2016 mkutano ambao ulifanyika Mkoa wa Mara, kupitia Halmashauri zetu mambo mengi sana waliyazungumza. Miongoni mwa mambo ambayo yalizungumzwa ni pamoja na Halmashauri nyingi kukosa watendaji walioajiriwa wa kada mbalimbali. Jambo hili limezungumzwa sana na Wabunge wenzangu na mimi nimeona ni bora nisisitize kwamba wakati sasa umefika kuhakikisha tunaajiri watendaji katika kada mbalimbali ikiwemo Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na wale wakuu wa idara ambao wanafanya kazi moja kwa moja katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilizungumzwa ni kuchelewa kupelekwa kwa peza zile za vyanzo vilivyofutwa. Tatizo hili limekuwa sugu, nimeona ni bora nisisitize jambo hili kwamba wakati sasa umefika wa kuhakikisha vyanzo vile ambavyo tulivifuta tunapeleka pesa kwa wakati. Kwa kufanya hivyo, tutazisaidia Halmashauri zetu kutekeleza majukumu ambayo yamepitishwa kupitia bajeti za ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuchelewa kupelekwa kwa OC. Hili jambo naomba nilizungumze na naomba nitolee mfano kwa Halmashauri ya Wilaya ya

Tunduru, toka mwaka jana mwezi Julai OC katika idara zile mbalimbali hazijaenda. Naomba kuisisitiza Serikali tupeleke OC katika zile idara kwa kufanya hivyo tutazisaidia idara zetu kutekeleza majukumu yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba niliseme tena kabla sijasahau na kwa umuhimu wake, naomba nizungumzie barabara kwa kiwango cha lami inayotoka Mbinga-Mbamba Bay. Napozungumzia Mbamba Bay maana yake naigusa Wilaya ya Nyasa. Sote tunafahamu kwamba Wilaya ya Nyasa ni miongoni mwa Wilaya zilizoko mpakani. Wilaya hii inapaswa sasa kuona umuhimu wa kutengenezewa barabara kwa kiwango cha lami. Tunafahamu matatizo ambayo yanaweza yakajitokeza kwenye barabara za mipakani.

Kwa hiyo, ni vizuri kuhakikisha tunatengeneza barabara hiyo kutoka Mbinga mpaka Nyasa kwa kiwango cha lami. Nimeona niliseme hili nikiwa nafahamu kwamba mara nyingi hata watumishi wanaopelekwa kwenye barabara hizi za mpakani wamekuwa na wasiwasi na hasa wakiangalia masuala ya miundombinu. Naomba nisisitize Serikali yangu katika kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa barabara ya lami kwa kiwango cha lami kutoka Mbinga mpaka Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba nilizungumzie ni suala la shilingi milioni 50. Wenzangu wengi wamelisema na wengine wamekuwa wakifananisha na mamilioni ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Mimi naomba niseme hizi shilingi milioni 50 zilikuwa ahadi kutoka kwa Rais wetu aliahidi baada ya ushindi wa chama chetu na sina shaka kwamba tulishinda kwa kishindo na mimi nachofahamu utamaduni wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni kutekeleza kile tulichoahidi, niombe sana tutekeleze kwa kupeleka hizi shilingi milioni 50. Nafahamu tunapozungumza Serikali za Vijiji ni mamlaka kamili zina Wenyeviti, Halmashauri za Vijiji na zina Wenyeviti wa Vijiji, tupeleke hizi pesa wao sasa wataona ni nini kifanyike kupitia hizi shilingi milioni 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo mimi naomba nilizungumze hapa, ni suala la vifo vya akina mama wajawazito, naguswa sana na jambo hili nikiwa mimi ni sehemu ya wazazi. Tumelisema sana akina mama kupitia kwenye vikao hivi lakini kinachosikitisha zaidi hata ukiangalia kwenye bajeti zetu jambo hili linaonekana halipewi kipaumbele. Mimi nimeona niliseme hili kwa huzuni kubwa sana nikiwa nafahamu kwamba ninapozungumzia suala la vifo vya akina mama wajawazito ziko sababu nyingi zinazosababisha vifo. Sababu mojawapo ambayo mimi nimeiona ni ukosefu wa vifaa tiba. Mpaka hivi tunavyozungumza kwenye zahanati zetu akina mama wanatakiwa waende na mabeseni na vifaa vya kujifungulia. Sisi kama Serikali wakati sasa umefika mama anapokwenda kwenye kituo vile vitu anavikuta hapo hapo kwenye zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni suala la wataalam. Tumezungumza sana suala la kuajiri watumishi wenye ujuzi wa kutosha katika zahanati zetu. Ni jukumu langu kama mama kusisitiza kwamba sasa wakati umefika wa kuona tunakuwa na wataalam wa kutosha kwenye maeneo ambayo wakina mama wanajifungulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maeneo ya kutolea huduma. Napozungumzia maeneo ya kutolea huduma nagusa zahanati na vituo vya afya. Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakuwa mashahidi tuliahidi kujenga zahanati kila kijiji na kujenga kituo cha afya kila kata. Naomba sana wakati sasa umefika wa kutekeleza na ni vizuri sasa kwa kuwa Serikali hii sikivu basi ni bora na wananchi wetu waone inasikia kwa vitendo, itekeleze vile vitu ambavyo imeahidi na mimi naamini kwa kufanya hivyo itaturahisishia hata katika kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo mimi naomba niliseme na kweli wenzangu wengi wamelisema ni suala la miradi ya maji. Tunayo miradi ya maji ambapo mpaka hivi tunavyozungumza haileti tija kwa wananchi wetu. Kama tunavyofahamu wahanga wakubwa wa jambo hili ni akina

mama. Tumtue mama ndoo, tukaribishe huduma hii kwa mama, hivi tunavyoona akina baba wanapendeza, wamevaa suti nzuri ni kazi ya sisi akina mama katika kuhangaika kutafuta maji. Kwa hiyo, mimi kama mama, kama mwanamke ambaye na mimi ni miongoni mwa waathirika wa jambo hilo ninalazimika kusisitiza Serikali kwamba wakati umefika wa kuhakikisha tunatenga bajeti za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iko mingi lakini miradi mingine ni viporo na kwa kuweka miradi viporo tunaisababishia ile miradi kuongezeka gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, kupitia kikao hiki nisisitiza sana, iko miradi mingine mpaka hivi tunavyozungumza ilikabidhiwa kwa wananchi, lakini haitoi maji, wakati sasa umefika kwa Serikali yetu kuona uwezekano kupitia Halmashauri zetu kubaini miradi yote ambayo haijatekelezwa ipasavyo lakini kuitengea pesa miradi mipya ya maji kuhakikisha tunaondokana na hili tatizo la miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Katika kipindi ambacho nimekaa hapa Bungeni, miongoni mwa Wizara ambazo zimetulia ni pamoja na Wizara hii. Dalili ya kuonyesha Wizara hii imetulia ni kusikilizana kwa Waziri na Naibu wake lakini kama hiyo haitoshi kusikilizana kwa Waziri, Naibu na watendaji katika Wizara. Mimi naamini kwenye Wizara mkiwa na wimbo mmoja kila kitu kitafanikiwa. Mnafanya vizuri, binafsi nawapongeza sana na naendelea kuwatia nguvu, endeleeni kufanya kazi, endeleeni kuchapa kazi sisi tunawatumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana kwa suala la kuondoa ushuru wa mazao ya chakula. Miongoni mwa vitu ambavyo vilikuwa vinawagombanisha viongozi na wakulima ni suala la ushuru ilikuwa shida sana katika Halmashauri yetu. Mimi naona katika vitu ambayo mmeitendea haki Serikali yetu, mmewatendea haki wakulima wetu ni katika kuondoa suala la ushuru kwamba sasa wakulima wameruhusiwa kusafirisha tani moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye hili eneo naomba tusije tukasahau, kwamba kupitia hapo hapo Halmashauri zilikuwa zinapata pesa. Nalisema hili kwa sababu nina uzoefu nalo, mimi kama mkulima naweza nikawa na tani zangu kumi, nitakachokifanya ili nisafirisha kwa kutimiza huu wajibu wa tani moja ni kuandika jina la mwanangu, mjomba wangu, shangazi ili kuhakikisha tani kumi zote zinasafirishwa. Kwa kuwa Serikali imeamua kuwarahisishia kusafirisha tani moja ni vizuri tuweke mkakati mzuri na tuziagize Halmashauri zetu ni mbinu gani zitatumika ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na baadaye Mheshimiwa Upendo Peneza ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili nami nipate kuchangia bajeti hii ya Serikali. Nianze kabisa kwa sababu muda ukiisha unaweza hata ukasahau kuunga mkono bajeti hii au hoja ya Waziri wa Fedha, kwa hiyo, nasema kutoka mwanzo naiunga kwa nguvu zote hoja hii ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza na kumshukuru sana na kumuomba Mwenyezi Mungu Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa ujasiri wake huo aliouonyesha kuhusu suala la makinikia na kuibua ukweli wa uwekezaji wa kinyonyaji na uovu unaotudidimiza badala ya kutuondolea umaskini na udhalili. Rais amefanya jambo kubwa na kwa kweli hajajifanyia mwenyewe amewafanyia Watanzania. Kwa hiyo, sisi wote tumuunge mkono, tumsaidie na tuone kwamba hii *economic order* ya dunia inapokuja kwenye nchi yetu lazima kuwe na watu ambao wanajitolea na lazima

iingie kwenye vitabu vya historia kwamba Mheshimiwa Magufuli amesaidia sana katika kuondoa *economic order* ya kinyonyaji. Tukifaulu hapa tujue nchi hii itakuwa imechangia mchango mkubwa sana katika uchumi wa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima kama alivyoelekeza litakuwa kwenye sera na kwenye sheria tutakavyoziangalia hapa Bungeni. Wote ambao ni wataalamu tuziangalie kwa uzuri ili kazi hii aliyoifanya ilete manufaa kama yeye alivyokuwa anategemea. Mwenyezi Mungu atampa yeye na sisi nguvu tuwe pamoja kuona kwamba madini ambayo Mwenyezi Mungu ametupa yanaleta manufaa katika nchi yetu na kuendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu wake Mkuu na watendaji wote kwa kuikalia bajeti hii. Bajeti hii imefanyiwa kazi, ina ubunifu mkubwa, imesikiliza kilio chetu ambacho kimetokana na wananchi, nawapongeza sana. Haitoshi kuwa na bajeti bali utekelezaji ndiyo utakaoleta maana kubwa. Naomba tutekeleze bajeti hii na kule kwenye Halmashauri kama ushuru hautatozwa hovy hovy, nawaambia kilimo, ufugaji, uvuvi utaendelea na huduma mbalimbali zitapatikana bila shida. Kwa hivyo, suala la usimamizi lazima lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ione umuhimu wa kilimo, ufugaji na uvuvi. Wenyewe ndiyo waliotuambia kwamba kilimo kinachangia asilimia 29.1 na viwanda vinachangia asilimia 25 na uchangiaji wake unapanda, lakini kilimo ukuaji wake unashuka na ni wao wenyewe ndiyo wameandika. Naomba tu *reverse* hii *trend* ya ukuaji wa kilimo kwenda chini kwa sababu mchango hautaongezeka kwenye Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, ili kilimo kiendeleo tuhakikishe kwamba bajeti ya kilimo inayotengwa basi itolewe kwa wakati. Ukienda ukasaidia wakulima

kupata mbegu wakati msimu wa kupanda umepita hujasaidia wakulima. Wakulima wakitaka pembejeo wakati ukifika lakini hawapati hawatafaidika. Naomba sana tuangalie ni wakati gani tunafanya mambo yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia madini yanakua kwa asilimia 13, uchukuzi na mawasiliano unakuwa kwa asilimia kubwa sana, lakini ukiangalia mchango wao kwenye pato la Serikali ni mdogo sana. Hicho ndiyo kielelezo kwa nini umaskini wa Tanzania haupungui kwa sababu kule kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi ambapo kwa kiasi kikubwa ndipo walipo wananchi wote wa Tanzania hakujapewa uzito. Kwa hiyo, Watanzania hawataondokana na umaskini kama hatutawakazania. Naomba sana hili mlitambue, mmetuonyesha wenyewe kwenye takwimu. Kwa hiyo, naomba sana muone kwamba ili kuondokana na matatizo ya wakulima, kwanza tuhakikishe kwamba wanapata pembejeo, huduma za ugani, masoko na wanapata viatilifu kwa wakati ili mazao yao yasiliwe na wadudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kitu kimoja, kilimo na ufugaji hautaendelea kama migogoro ya wakulima na wafugaji itaendelea. Nataka niwaambie kwamba hifadhi zinajulikana narudia, kilimo mahali wanapolima panajulikana kwa sababu mazao yanaonekana, wafugaji hawaoni maeneo yao kwa sababu ng'ombe akirudi nyumbani, hamtajua kwamba hilo ndiyo eneo la wafugaji. Naomba mtenge bajeti ya kwenda kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima nao hawatapata hasara kwa sababu kama wafugaji wanajua maeneo yao katika kila Wilaya, hawatakuwa na sababu ya kupeleka ng'ombe kwenye mashamba ya watu, hawatakuwa na sababu ya kupeleka mifugo kwenye hifadhi, naombeni sana mfanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee habari ya maji, akina mama ndiyo wanaolima mashambani, wakitumia masaa mengi kutafuta maji maana yake muda wa kuwa shambani unapungua. Naomba ile tozo ya shilingi 50 iende kwenye suala la maji. Nampongeza Mheshimiwa

Waziri ameonyesha maeneo ambayo yanaongeza bajeti ya maji lakini sehemu hiyo sio ya uhakika. Kama Mfuko wa Maji ukipata tozo hizi kutoka kwenye mafuta au mahala pengine mtakapoamua, tutakuwa na uhakika wa bajeti ya maji na maji ndiyo uhai kama alivyokuwa amesema Mbunge aliyetangulia kuongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kuongelea ujenzi wa vituo vya afya na zahanati vijijini. Ndugu zangu wananchi wamejitolea kujenga madarasa, zahanati mpaka kwenye lenta na vituo vya afya. Serikali ione basi pale ambapo wananchi wamechangia na yenyewe ichangie. Mahitaji ni mengi, vipaumbele mkiviweka sawasawa, nina hakika bajeti hii itakuwa mkombozi wa Mtanzania na tutaendelea kuona manufaa na umasikini utaendelea kutoweka. Mheshimiwa Waziri utaweka historia kama bajeti hii itatekelezwa. Mheshimiwa Waziri tutaona ulivyotumia nguvu yako kama bajeti itakwenda ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita ilitoka kwa sehemu ndogo sana, umeeleza na tumeelewa hatuna ugomvi na wewe lakini sasa hivi kazana na ukusanyaji wa kodi. Hakuna mtu ambaye atakuwa na hiari ya kulipa kodi. Kuna maeneo ambayo tukiyasahihisha kodi itaongezeka na mapato ya Serikali yataongezeka. Kule ambako mmeondoa hizi tozo za ushuru mpeleke nguvu zenu kama kwenye madini, utalii na maeneo ambayo kuna fedha. Tukifanya hivyo ndugu zangu tutakuwa tumejielekeza na tutakuwa na mkakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tuwe wamoja wakati huu wa vita, vita inataka umoja na mshikamono, vita inataka umakini mkubwa. Msifikiri hao watu watakuwa tayari kurudisha hayo ambayo wametaka kuyachukua, watatudanganya danganya na sisi tuone wapi tunadanganywa. Naomba suala hili la makinikia tulishughulikie wote, Rais ameshaonyesha njia, wataalam na wananchi kwa pamoja na ikiwezekana nchi nzima irindime kuwa na maandamano ili dunia nzima ione kwamba Tanzania ina watu wajasiri wakiongozwa na Rais wao anayepita kwa ujasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kunipa nafasi hii na Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu, Mwenyezi Mungu ambariki Waziri wetu wa Fedha na Naibu wake na Naibu wake na Watendaji wao na Mwenyezi Mungu abariki Bunge hili na naomba bajeti hii iweze kutekelezeka. Narudia tena, naunga mkono kwa nguvu zote bajeti hii na kwa moyo mmoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na tunamalizia na Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nachukua fursa hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisaidia na kuweza kuchangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho napenda kuanza nacho ni kitu ambacho kimeongelewa na Wabunge na Watanzania wengi, ni suala la makinikia pamoja na ripoti ambazo zimetokana na Tume ambazo ziliundwa na Mheshimiwa Rais. Siku zilizopita tumepata pia kusikia kwamba *President* wa Barrick amekuja kwa ajili ya kuweza kufanya mazungumzo, ingawa kauli tunazozipata, kauli iliyotoka mdomoni mwa Rais na kauli iliyotoka katika Kampuni yenyewe ya Barrick ni maneno ambayo kidogo yanakinzana ambapo tunashindwa kuelewa ni kitu gani hasa ambacho kimeongelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho napenda tujiulize, ni kwamba tunaenda kufanya *negotiations* kwa kitu gani, tunaenda kufanya mazungumzo kwa ajili ya nini, tunaenda kufanya mazungumzo kwa ajili ya makinikia ama tunakwenda kufanya mazungumzo ili kuweza kuangalia vitu vyote ambavyo tumepoteza kutokana na mikataba hii? Kama tunakwenda kufanya mazungumzo ili kuangalia ni jinsi gani ambavyo Tanzania tumeweza kupoteza kutokana na sisi wenyewe kama Serikali, sisi wenyewe kama nchi, sisi wenyewe kama viongozi ambao wamekuwepo kwa kuingia mikataba mibaya ambayo imetuletea wizi namna hii, migodi yote iweze kuhusishwa katika mazungumzo haya. Kama

tunataka tuangalie suala zima la mikataba, kama tunataka kuangalia suala zima la sheria, ni lazima tuangalie kwa migodi yote, hatuwezi kwenda kwenye mazungumzo na mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye hili suala zima la makinikia, napenda kutoa tahadhari kidogo, kumekuwa na taarifa ambazo zinakinzana, lakini ningetaka kuiamini Serikali kwa Tume na ripoti ambayo imeitoa. Naomba pia tuangalie na tuweze ku-*verify information* ambazo tumezitoa na Serikali iende kwenye hatua ya mbele zaidi kufanya uhakiki ili kama tunaenda kwenye *negotiations*, kama tunaenda kwenye mazungumzo twende kama watu wasomi, twende na timu imara, twende na watu ambao wanaweza kusimamia kitu ambacho kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kutokana na muhtasari wa ripoti iliyotolewa inazungumzia kwamba makinikia haya yameanza kusafirishwa toka mwaka 1998 lakini ukisoma katika ripoti ya Lawrence Masha na ripoti ya Jaji Bomani inaonesha kwamba *production* ya mgodi huu imeanza mwaka 2001. Kwa hiyo, hebu tukaangalie mambo yetu vizuri, twende tusidharaulike, kama tunapeleka Maprofesa kweli ionekane tuna *information* ambazo ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala hili halijatuletea athari au kuibiwa tu kama tunavyosema au Serikali kupoteza mapato lakini suala hili la migodi na mikataba ambayo Serikali imeingia imeleta mpaka wananchi wetu kupoteza maisha. Wananchi wetu wamepoteza maisha huku migodi hii ikilindwa na askari polisi wetu. Vyombo vyetu vya usalama vimepiga risasi watoto wetu wa Kitanzania kulinda uwekezaji wa Wazungu. Ndiyo maana tumepata vifo vya wananchi wengi vilivyotokea kule Tarime lakini na athari kubwa sana ambazo ziko katika Mkoa wangu wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya bado hayajaisha, ni miaka imepita tangu wananchi wa Tarime

wamekufa lakini bado athari na shida zinaendelea. Ukisoma katika ripoti ya Jaji Bomani inataja maeneo mawili ndani ya Geita, eneo la Nyakabale ambalo wananchi wanaishi ndani ya leseni ya mgodi. Wananchi ambao barabara yao ya mwanzo imefungwa, hawawezi kupita barabara yao ya mwanzo kwa sababu ya mgodi. Wananchi wanateseka, wanahatari ya kubakwa kutokana na hii njia ambayo imetengenezwa na mgodi. Wananchi hawana huduma hata ya umeme wala maji katika eneo lao kwa sababu ni eneo lenye leseni ya mgodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wananchi wa Katoma wametajwa kwenye ripoti ya Bomani kwamba wananchi wa Katoma na Kompaundi hawa ni watu wanaoathirika na mitetemo ya mgodi, nyumba zao zinapasuka. Waziri Kalemani alikuja Geita kuongea na hawa watu wa migodi ili kuhakikisha ya kwamba haya yote yanamalizika.

#### TAARIFA

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Unanimalizia muda bwana.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Katoma na Nyamalembu, nikiwa Waziri wa Ardhi wote walipewa fidia na nilishajulisha Bunge hili. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Upendo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu akae chini, kwa sababu kama yangukuwa yamefanyika hayo, tusingekuwa na kikao na Kalemani juzi

hapo Geita. Akae chini hajui kinachoendelea Geita, haishi Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kitu ambacho nasema ni kwamba ninaumia kwa sababu haki za watu zinaendelea kuvunjwa. Tunaongelea kodi kupotea lakini haki za binadamu zinavunjwa katika maeneo haya yanayozunguka maeneo ya migodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe *suggestions*, tuna kitu ambacho kinaitwa *service levy, 0.3 percent ya gross revenue* ya hii migodi, mimi natoa wazo kwa Serikali na kwa Waziri Mpango, Serikali ilete sheria humu ndani, tutengeneze *Development Fund*. Pesa hizi zote zinazokusanywa zitaingizwa kwenye hiyo *Development Fund* ili kuhakikisha zinaenda kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo husika ili wananchi hata baada ya shughuli za mgodi kuondoka waone kwamba kodi zilizopatikana zilijenga miundombinu kwa ajili ya watu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichangie katika suala la kuweka mfumo wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia. Nilipokuwa mgeni kabisa ndani ya Bunge hili nilichangia kuhusu suala la *sanitary pads*, nikasema Serikali iweke pesa ili kuhakikisha watoto wetu mashuleni wanapata *sanitary pads*. Ni kitu ambacho hakijafanyiwa kazi na Wizara ya Afya wala hakijafanyiwa kazi na Wizara ya Elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaona kwamba kama ni shughuli za maendeleo, watoto wa kike na wanawake wana haki sawa ya kushiriki katika uchumi wa Taifa lao. Kutokana na utofauti uliopo, wanawake na wasichana wanashindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli hizi. Kwa hiyo, niombe Serikali ipange pesa kwa kuzingatia kwamba kina mama wanaweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwawekee hela za kutosha kwenye dawa na hapa nilipendekeza kwamba pesa ya dawa ihamishwe kutoka kwenye *development budget* zipelekwe

kwenye *recurrent expenditure*. Hela za dawa peke yake, vifaa tiba vibaki kwenye *development budget* ili kuhakikisha kwamba hela za dawa na maji ya uchungu zinapatikana ili akina mama wetu waweze kupata tiba na kuepusha vifo wakati wanajifungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye masuala ya kilimo, akina mama ambao wana uwezo wa kumiliki ardhi mpaka leo hii ni asilimia nane tu, wengine wanatumia ardhi ambazo ni za waume zao na ardhi za ukoo. Kama Serikali katika bajeti yake, inaweka mifumo gani ya kuhakikisha kwamba akina mama wanaweza kutengewa pesa kuwainua ili na wao waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo za maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho naomba nipendekeze kwenye suala la *property tax* ambalo limeshazungumziwa na wengi. Mimi natoka katika Halmashauri ya Mji wa Geita hapo ndipo ninapoishi na wananchi wale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Peneza muda wako umeisha.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu wa leo, kabla sijaendelea na mengine na kumaliza niwatangaze kabisa wachangiaji ambao wataanza jioni.

Tutaanza na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Suleimani Zedi, Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Rose Tweve. Hawa wataanza baada tu ya kuingia jioni.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Baada ya kusoma majina hayo ambayo wataanza kuchangia jioni, kuna taarifa moja kutoka kwa Katibu wa Bunge kuhusu utaratibu wa kuwasilisha nyaraka mezani, naomba nisome kama ilivyo. Kwa nyakati kadhaa, wakati wa mijadala ya hoja mbalimbali humu Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakitoa nyaraka zinazoonyesha ushahidi wa mambo wanayochangia na wakati mwingine kuwasilisha nyaraka hizo Mezani kwa ajili ya rejea. Ili kuleta uhalali wa nyaraka hizo na kwa mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge (*The Parliament Immunities, Power and Privileges Act, Cap. 296*) na Kanuni za Bunge utaratibu ufuatao unatakiwa ufuatwe.

1. Nyaraka zinazowasilishwa Mezani zinatakiwa kuwa zimesainiwa kwenye kila ukurasa na Mbunge anayewasilisha; na

2. Nyaraka zinazowasilishwa zinatakiwa kuwa ni zile zilizohakikiwa na kuthibitishwa na mwanasheria kama ni nakala halisi (*certified copies*).

Kufuatia utaratibu huo, Mheshimiwa Said Ahmed Kubenea, Mbunge, ambaye aliwasilisha Mezani nyaraka jana tarehe 15 Juni, 2017 anatakiwa afike Ofisi ya Katibu wa Bunge ili atimize masharti hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo hapa linatoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Maskauti, anatangaza kikao cha Wabunge wanachama wa Chama cha Wabunge Maskauti Tanzania kwamba leo tarehe 16 Juni, 2017 kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika ukumbi wa Msekwa C kuanzia saa 8.00 mchana. Tafadhali mnaombwa kuhudhuria na pia mzingatie muda.

Baada ya kusema hayo, niwashukuru sana kwa yote ambayo tumeyafanya kuanzia asubuhi ya leo hadi mchana. Mwenyezi Mungu awabariki sana na nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae! Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa Kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

(Majadiliano Yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na mjadala wetu, tunaanza na watu wetu ambao niliwataja asubuhi tunaanza na Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nianze na hoja yangu kwenye ukurasa wa 47 kitabu cha bajeti kwenye maneno madogo sana ambayo nataka kuzungumzia kuhusu *Electronic Revenue Collection System*; ambayo mfumo mpya ulianzishwa hivi karibuni, mfumo ambao kimsingi nakubaliana nao na nakubaliana nao kwa sababu kabla ya uanzishwaji wa mfumo huu makampuni ya simu yalikuwa yakikusanya fedha wenyewe baadae wakiwaita Serikali ndio wakiaanza kugawana mapato. Pamoja na kuwepo mfumo wa *TTMS* lakini mfumo wa *TTMS* ulikuwa haukusanyi kodi, hiyo ndio kasoro Mheshimiwa Zungu alipigia kelele sana ulikuwa haukusanyi kodi.

Kwa hiyo, sasa kilichoendelea nikwamba makampuni ya simu yalikuwa na uwezo mkubwa sana wakufanya ambavyo wanajua dhidi ya kodi ya Serikali. Na hasa napongeza hata kwa upande wa Zanzibar sasa kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiingiza vocha maana yake kodi ya Serikali pale pale inachukuliwa na kwa

upande wa Zanzibar ukiingaza vocha kodi inachukuliwa pale pale inakwenda *ZRB*, kwa hivyo kiufupi nikukubaliana na Serikali kwenye jambo hili ni jambo zuri na linafaa kuungwa kuungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilikuwa nazungumzia suala la michezo ya bahati nasibu. Michezo ya bahati nasibu sasa hivi pamoja nakuleta *negative impact* katika jamii, lakini imekuwa ni sehemu ambayo kama Serikali watakaa pamoja kuifanyia kazi ni sehemu ambayo inapatikana kodi kubwa sana kwa Serikali. Kwa mfano, sheria iliyokuweco sasa inawapa *Gaming Board* kukusanya kodi, lakini kwa mchezo ambao ulivyoendelea lazima tubadilishe sheria, *TRA* kwa sababu wanamtandao mpana wao ndio waweze kukusanya kodi kila maeneo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na habari hii unaijua vizuri, nadhani katika bajeti ijayo kwa sababu nafikiri tumechelewa katika bajeti ijayo lazima tubadilishe sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ile GGR manaake ile *Gambling Gross Gambling Revenue* ambayo tunakusanya kwenye *betting* peke yake tuna- *charge* asilimia sita, asilimia sita ambayo kwa mujibu wa makadirio ya *Gaming Board* kwa mwaka huu kwa mwaka 2016/2017 basi tungeliweza kukusanya shilingi bilioni 24. Lakini kwa mujibu wa makadirio ya mwaka 2017/2018 tutaweza kukusanya shilingi bilioni 39 nukta kadhaa, lakini tukiongeza kutoka kwenye *sport betting* asilimia sita kwenda asilimia 20 pekeyake tutaweza kukusanya shilingi bilioni 37 kwa hivyo hilo ni eneo moja. Lakini katika *casino* pia tuna-*charge* sasa hivi katika pato ghafi la kamari tuna-*charge* asilimia 15, lakini tukiongeza tukifika asilimia 20 manaa yake tutaweza kukusanya shilingi bilioni 20. Kwa hiyo hapo bado hatujaenda katika zile za *slot machine*; *slot machine* kwa sasa tunachaji shilingi 32,000 kwa *slot machine* moja.

Kwa hivyo lakini tukipeleka kwenye 60,000 tunaweza ku-*charge* shilingi bilioni 2.7 pia tunaweza kwenye upande wa *competation* yaani *lottering* Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunapoteza fedha, lazima tubadilishe sheria. Sheria

ile tubadilisha ili isiwe inamilikiwa na mtu mmoja, tuongeze watu ambao wataweza kuendesha *lottery* ya Taifa ili tuweze kukusanya shilingi bilioni 10 na inawezekana kabisa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi ningeomba katika bajeti ijayo jambo hili tukae jumla ya fedha ambazo tutazikusanya itafika shilingi bilioni 69 naa na kama *TRA* watakusanya vizuri basi tunaweza kufika hata shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu tuzungumzie suala la *medical tourism, sports tourism* na *beach tourism*. *Medical tourism* wenzetu wa Kenya wametenga kwa pesa za Tanzania shilingi bilioni 22. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ametuonesha njia, tunayo ile *Jakaya Kikwete Cardiac Institute* tunapokea wageni mbalimbali ambao wanakuja pale sasa kupata matibabu. Lakini ina *double impact* ya kwanza tunapata fedha moja kwa moja kutoka kwa wageni. lakini wageni wale wakifika pia wanatumia fedha kwa ajili ya mawasiliano, wanasafiri, wanakula tunapata pesa nyingi kutoka kwao. Lakini kinachosikitisha mpaka sasa Serikali haikutenga fedha yoyote katika eneo hili jambo ambalo tukilinganisha na *trainsza standard gauge* pamoja na ndege ambazo Serikali wanazininua tukiweza kuimarisha sekta ya afya katika nchi yetu na mzunguko wa nchi zilizotuzunguka hiyo itaweza kutusaidia sana na itaisaidia Serikali kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri tunachokizungumza hapa ni kwamba hata sasa, hata hawa wataalamu ambao wanaendesha hiyo Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete bado hatuna wa kutosha kutoka nchini kwetu tunaagiza watu mbalimbali wanakuja kufanya, hatujawekeza fedha kuwasomesha watu wetu katika eneo hilo. Kwa hivyo mimi niombe Serikali kwamba katika jambo hili ijitahidi inavyopaswa lakini iweze kuwekeza fedha kwa mfano, Tanzania sasa hivi kwa mujibu wa takwimu za karibuni wanasafirisha Watanzania wanaokwenda India kutibiwa karibu watu 23,000. Ukitizama Kenya wanakwenda karibu watu 40,000; ukitizama Sudani watu 8,000; ukitizama Nigeria

karibu watu 34,000 wanakwenda, sasa tungeifanya sisi tungepata fedha nyingi sana. ili Mheshimiwa Waziri nikushauri kwamba bajeti ijayo uhakikishe kwamba unatenga fedha katika eneo hili kwa ajili ya maslahi ya Tanzania na watu wetu na afya itaboreka nina uhakika sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena suala la *blue economy*, Ethiopia hawana hata bahari, bahari yao ndogo sana kule pembeni pembeni lakini wana meli *commercial ship* 18 Tanzania tumezungwa na bahari hatuna *commercial ship* hata moja. Mizigo yote yanapita baharini asiimia 95 hili ni eneo situ kwamba kila kitu kifanywe na Serikali lakini Serikali itakapoonyesha dhamira basi *stakeholders* watakuja kufanya hiyo shughuli si lazima mfanye ninyi, kwa hivyo eneo hilo nalo pia lina tatizo.

Mheshimiwa Waziri *aqua culture* yaani ufugaji wa samaki. Uganda wanatumia ziwa Victoria pekeyake *aqua culture* inachangia pato la Taifa asilimia 7.5 tuna maziwa tuna Victoria, Tanganyika, tuna Nyasa tuna na bahari yaani *acro culture* hatuchangii hata shilingi 100 katika Pato la Taifa haiwezekani, lazima Mheshimiwa Waziri tukubali maeneo mengine ya kuweka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho Mheshimiwa Waziri ambalo niliseme ni kuhusu mambo ya madini; na mimi kwenye madini ni seme kidogo ili na mie niweke kumbukumbu sahihi. Usalama wa Taifa wako wapi? Mali zote hizo zilizoibiwa siku zote Usalama wa Taifa wako wapi? Na nini jukumu la usalama wa Taifa katika nchi? Ikiwa Usalama wa Taifa wameacha mambo yote haya yameharibika kiasi hiki, hata sisi pia siwanaweza kutuuza?

Kwa hiyo, nafikiri usalama wa Taifa wajitathimini wasitake kumbebesha mtu mwingine msalaba wakati wao wana *access* ya kujua mambo mengi yanayotendeka katika nchi. Kwa hiyo jukumu la usalama wa Taifa, Mheshimiwa Rais kimsingi tunakubaliana naye katika mambo ya kupambana na watu ambao wanafanya tofauti lakini hakikisha Kitengo/ Taasisi cha Usalama wa Taifa inarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru asante sana.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngwali, tunaendelea na Mheshimiwa Rita Kabati na badae Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mada iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwa Rais alipokuwa anapokea ile ripoti ya makinikia ya pili aliomba sisi Watanzania tumuombe, hasa na mimi nikaona nitayarisha vifungu ni nukuu kidogo hapa katika Bunge letu ili wale ambao wanakuwa hawasomi Biblia waweze kusoma na naomba nisome Timotheo wa Pili Mlango wa Kwanza mpaka wa Tatu; “Basi kabla ya mambo yote wataka dua sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya Wafalme na wote wenye mamlaka ili tuishi maisha ya utulivu na amani.”

Lakini ukisoma Waibrania 13 mpaka 17 inasema; “Watiini viongozi wenu na kuwa wanyenyekevu maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu kama watu watakaotoa hesabu ili kwamba wafanye kazi yao kwa furaha na kwa manufaa yenu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magufuli ni zawadi kwa Watanzania ni Mussa wa Watanzania kwa vile Mungu alivyosikia kilio cha watu wa Taifa la Israel kuwakomboa toka utumwani na kuwapeleka Kanani vivyo hiyo Mungu amesikia kilio cha Watanzania wanyonge amemleta Rais Magufuli ili awe mkombozi wa kututoa katika utumwa, umaskini na kutupeleka katika neema kwa kudhibiti wizi wa madini na rasilimali za nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitumie fursa hii sasa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika nchi

yetu na niombe Watanzania bila kujali itikadi zetu tuunge mkono kwa yote anayo yafanya kwa ajili ya Taifa letu. Nawapongeza Watanzania wote waliomuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu na hatua wanazozichukua kukabiliana na upotevu wa mapato ya Serikali katika sekta ya madini, nawapongeza Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa azimio lao ambalo walilitoa juzi kuunga mkono juhudi hizi za Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri katika Ofisi yake Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wake Mheshimiwa Mavunde kwa kuaamua kuupatia heshima Mkoa wetu wa Iringa kuja kuzindua mafunzo ya ufundi kwa vijana wetu katika Chuo cha Don Bosco; mafunzo ambayo yatawanufaisha vijana karibu 3,440 na yataendelea kwa nchi nzima tena bure kabisa. Vijana 1,000 Mwanza, vijana 1,000 Morogoro, vijana 2,000 Dar es Salaam na vijana 4,000 ambao wamekuwa wakifanyakazi bila kupata mafunzo watapata vyeti vyao. Kwa hiyo, ni jambo jema ambalo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inatakiwa iungwe mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeza sasa katika madaa nimpongeze Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango, Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kijaji na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yake ya bajeti nzuri na yenye mashiko, na ambayo imejali watu wote wakulima, wafanyakazi, wote imewajali kwa kweli. Lakini naomba kabla sijaanza kuchangia kabisa na mimi ni nukuu katika hotuba ya msemaji wa Kambi ya Upinzani ukurasa wa tatu maneno ya hayati Nelson Mandela *“No easy walk to freedom.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie wenzangu Wapinzani kuwa nchi hii ilikwisha pata uhuru kwa njia ya amani na utulivu. Sasa sijui wenzetu wanapigania uhuru wa nchi gani maana nchi yetu ilikwisha kombolewa kutoka kwa wakoloni kwa jitihada za TANU na sasa hivi ndio CCM na hao hao NAC tuliwasaidia Watanzania kupata uhuru kutoka kwa makaburu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali katika bajeti hii kwa kuwatambua rasmi wafanyabishara wadogo wadogo wasio rasmi na wanafanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi kama mama lishe, wauza mitumba wadogo wadogo, wauza mazao ya kilimo kwa kuwapatia vitambulisho maalum kazi wanazozifanya. Lakini nilitaka kujua je kuhusiana na vijana wa bodaboda na wenyewe wako maana yake kwenye kitabu kile hawajasema maanake nao wamekuwa wakitoa kodi naomba na wenyewe labda watakapokuwa wanajibu watuambie kama na bodaboda na wenyewe wapo.

Pia nilikuwa naomba Halmashauri zetu ziandae sasa mazingira rafiki kwa hawa wafanyabiashara waweke miundombinu rafiki, kuwepo na maji, kuwepo na umeme na waangalie sehemu ambazo hawa wanaweza wakafanya biashara zao na wakapata faida. Kwa sababu utakuta Halmashauri zetu zimekuwa zikitenga maeneo ambayo sio rafiki na biashara na kuwasababisha vijana wetu kushindwa kufanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi pia niungane na wote waliochangia kuhusiana na tozo ile ya shilingi 40 katika mafuta mimi nilikuwa naomba kweli ipelekwe moja kwa moja katika mradi wa maji. Kwa sababu maji vijijini ili dhamira ya kumtua ndoo kichwani mwanamke iweze kutimia kwa sababu ukiangalia katika Mkoa wetu utakuta miradi hii ya maji mingi sana imekwama, visima vingi vimechimbwa lakini havitoi maji na vilevile unakuta kuna vyanzo vya maji vingine ambavyo bado sio salama, kwa hiyo, kuna maziwa na mito mingi lakini bado hatujaweza kupatiwa maji vizuri katika Mkoa wa Iringa maji vijijini ni tatizo kubwa sana. kwa hiyo nilikuwa naomba ile tozo iende moja kwa moja kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuchangia kuhusiana na hoja hii nafikili tunaelekea katika uchumi wa viwanda lakini bila kutoa kipaumbele katika barabara zetu za kiuchumi bado tunapatashida sana, kwa sababu ndizo ambazo zenye malighagfi, utakuta katika Mkoa wetu wa Iringa barabara nyingi sana za kiuchumi hazina lami. Kwa

hiyo, utaona kwamba zile malighafi wakati wa mvua malori yanakuwa yanakwama ukienda kule Mufindi, Kilolo unakuta kwamba yale malori yanakwama kule kwa hiyo mimi nilikuwa naomba Serikali itoe kipaumbele ihakikishe kwamba barabara zote za kiuchumi zinawekewa lami ili kusaidia hata kukuza uchumi huu wa viwanda kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia mara ya kwanza nilichangia kuhusiana na Benki ya Wanawake; kwa kweli hii Benki ya Wanawake sisi kwa Wanawake ni mkombozi na nilisema kwamba imeshafungua baadhi ya madirisha katika baadhi ya Mikoa ambayo sio mingi, ningeomba Serikali kwa kweli iangalie kwa karibu ili iweze kuipatia ile pesa ambayo ruzuku ambayo ilikuwa Serikali imeamua kuwapatia ili Wanawake wote wafaidike kwa sababu Wanawake wengi sana walikuwa wanaaibishwa, ndoa nyingi sana zimevunjika kwa sababu wanaenda kuchukua kwenye taasisi za fedha nyingine ambazo zinawafanya wanawake wanadhaliika wanawake ndoa zimevunjika, wanauziwa mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naamini kwamba kwa sababu Serikali na tulikaa kwa pamoja na tukaamua kwamba Benki ya Wanawake iwanufaishe Wanawake wote basi Serikali iweze kutoa pesa ambayo ruzuku ilikuwa imeahidi kwamba ingeweza kuwa inatoa kila bajeti ili madirisha mengi sana yaweze kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kinu chetu cha Iringa pale *National Milling*, nililisema siku ile kwenye swali, kile kinu tuna imani kwamba *NSSF* walisema kwamba wangetusaidia ili kile kinu kiweze kusaidia wakulima wa Iringa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kweli hili nalo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba makinikia yetu sisi Iringa ni vinyungu, utaona Wabunge wengi sana wamechangia hapa wakizungumzia kuhusu vinyungu. Vinyungu ndio mkombozi wa wana Iringa sasa nisipozungumza sasa hivi wanawake wote wanashindwa, maana yake ilikuwa mwaka mzima unalima, mwaka mzima

unafanya biashara kupitia vinyungu vile, hata mimi mwenyewe nimesomeshwa kwa vinyungu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iangalie upya hili suala la vinyungu maana yake hata kwa Wasukuma kule wanaita majaruba maana mimi nimeolewa na Wasukuma wanaita majaruba kwa hiyo kila nchi wanaita kwa majina yao, kwa hiyo ningepomba hivi viangaliwe upya ili wananchi waendeleo kutumia maana yake naona Wabunge wengi wa Iringa pia wamezungumzia kwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza haya kwa kweli kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na niseme kwamba Waziri wa Fedha kanyaga twende, fanya kazi, tunajua kwamba tunakuamini, wewe ni Waziri ambaye umekuwa ukitusaidia sana, kwa hiyo, endelea na Naibu wako, fanyeni kazi leteni bajeti na niombe sasa pesa zifike kwa wakati kwenye Halmashauri zetu ili ile miradi ya muda mrefu iweze kumalizika kwa wakati kwa sababu tumekuwa na miradi mingi ya muda mrefu ambayo sasa mkichelewesha pesa gharama inakuwa inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia 150. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati, tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Zedi baadaye Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Richard Mbogo, ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupata nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia bajeti hii ambayo mimi naiita ni bajeti sikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa dhati kabisa wametoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa

Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua za dhati anazochukua kulinda raslimali za Nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ujasiri na uthubutu wa Dkt. John Pombe Magufuli haupo tu ndani ya Tanzania bali umevuka mipaka ya Tanzania. Mimi mlinipa heshima mlinichagua kuwa Mbunge kuwakilisha Tanzania kwenye Bunge la nchi za SADC mara zote hivi karibuni nilipokuwa nikienda kwenye vikao vya Bunge la SADC, Wabunge wote wa nchi za SADC ambazo ni nchi kama 14 wakiwemo na Maspika wa nchi zao, tunapokutana, tulikuwa South Africa, tulikuwa Namibia, kila unapojitambulisha kama ni Mbunge umetoka Tanzania baada ya salamu tu, suala linalofuatia ni kuuliza *how is Magufuli doing?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana shauku ya kujua wengine wanauliza huyu mtu kabla hajawa Rais alikuwa nani, wanataka kujua ni kwa sababu ya uthubutu na ujasiri ambao kwa kweli umevuka kiwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo naipongeza bajeti hii kwa sababu ni bajeti sikivu kwa maana ya kwamba imezingatia maoni ambayo kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiyatoa na tumekuwa tukitaka yatekelezwe, sasa yamekubalika na ndiyo maana naiita bajeti sikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba ukiacha Madini eneo lingine ambalo kuna *potential* kubwa ya kupata mapato ni eneo la gesi asili. Ushauri wangu hapa ni kwamba Bunge lililopita Bunge la Kumi, mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini tuliunda Kamati Ndogo ambayo tulipitia mikataba ya gesi na kuona *loophole* na mianya ambayo inaleta upotevu wa fedha kwenye sekta ya gesi asilia. Nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Mipango atafute *report* ya Kamati Ndogo ya Nishati na Madini iliyoshughulika na gesi ya mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo mengi na ushauri ambao tumetoa ya namna ambayo Serikali inaweza kupata mapato mengi tu ya kutosha kutoka kwenye sekta asilia ya gesi, pamoja na kwamba gesi kubwa ambayo tumevumbua sasa hivi haijaanza kuzalishwa, lakini hiyo hiyo ya Songosongo kuna *potential* kubwa sana ya kupata mapato ambayo sasa hivi hatuyapati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tafuta hiyo *report* upitile mapendekezo na ushauri nina uhakika utapata mambo mazuri tu hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa sababu Jimboni kwangu kuna kero nyingi ambazo nataka zitatuliwe na mambo yote tunayoyahitaji, tunasema watu wetu wanahitaji umeme, wanahitaji maji, wanahitaji barabara, haya yote hayawezekani bila kupata rasilimali fedha na bajeti hii kwa kiwango kikubwa imekuwa *very smart*, imeainisha namna ambavyo wananchi watalipa kodi na watalipa kodi bila maumivu makubwa jambo ambalo litafanya tupate fedha za kutosha ili tuweze kushughulikia matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu kuna mradi mkubwa wa *REA Phase III* ambao zaidi ya vijiji 40 kwa mara ya kwanza haijawahi kutokea vinakwenda kupata umeme, lakini kuna vijiji ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vikisubiri umeme vijiji vya Mwamala, Igusule, Lububu, Kasela, Kayombo, Karitu na Isagehe kwa kipindi kirefu mno, kila ninapokwenda kule kero yao ni nishati muhimu ya umeme na sasa hili linakwenda kutokea kwa vitendo. Kwa hiyo, ninaipongeza sana bajeti hii kwa kuzingatia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalonifanya kifua mbele kabisa kupongeza bajeti hii ni namna ambavyo bajeti hii imepunguza ushuru wa mazao. Jimbo langu la Bukene asilimia 90 ni vijiji na shughuli kubwa ya wananchi kule ni kilimo cha mpunga, kilimo cha mahindi na hii hii mpunga na mahindi ni mazao ambayo kwetu sisi ni ya biashara, lakini hayo hayo pia ni mazao ya chakula. Kwa hiyo, wananchi wengi wamekuwa wakisafirisha mazao yao kwa

ajili ya kuuza, lakini kulikuwa na kero hiyo ya kwamba hata gunia tano/sita chini ya gunia kumi watu walikuwa wanatozwa kwenye vivuko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bajeti imezingatia hilo na kuanzia sasa chini ya tani moja ambayo kama ni magunia ya kilo mia mia magunia kumi hayataozwa chochote kwenye mageti kwa hiyo nia jambo ambalo wapiga kura wangu wamekuwa wakinipigia simu wakifurahia na kusema kweli kwamba hii Serikali ya Awamu ya Tano kweli ni Serikali kwa ajili ya wanyonge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kodi ya majengo na tunafahamu *Urban Authority Rating Act* inazipa Halmashauri uwezo wa kutoza kodi za majengo, lakini ushauri wangu hapa ni kwamba namna ya utekelezaji ambao unafanyika huko ngazi za chini na niseme hapa kwamba ninafahamu dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano siyo kuwanyanyasa au kuwasumbua wananchi na sisi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kwenye ngazi za Halmashauri ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba Wakurugenzi na wataalam hawakiuki au hawatekelezi jambo hili kwa namna ambayo inaleta madhara, ninafahamu maeneo mengine kwa mfano Nzega, tumeanza kuweka alama kwenye nyumba kwa ajili ya maandalizi ya kwenda kwenye zoezi hilo, lakini maeneo mengine Watendaji wamekuwa wanakwenda kinyume wanaweka alama kwa ajili ya kutoza hadi kwenye nyumba ambazo zimezekwa kwa nyasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ambazo zimejengwa kwa matope ambazo sio nyumba za kudumu, na tunajua utaratibu na muongozo ni kwamba kodi ya majengo ilipwe kwenye nyumba za kudumu na nyumba ya kudumu ni nyumba ambayo imejengwa kwa matofali ya saruji au matofari kuchomwa na imezekwa kwa bati. Lakini sasa maeneo mengine kwa makosa ambayo haya ni makosa ya Watendaji, siyo sera, siyo sheria, ni watendaji maeneo mengine ambako unakuta hata nyumba za nyasi, nyumba

za matope ambazo sio za kudumu nazo wanazitosa kodi ya majengo. *(Makofi)*

Lakini hili ni jambo la sisi hatuwezi kutegemea Mheshimiwa Mpango aende kijijini kwangu kule Semembela akaseme hii nyumba inafaa ni sisi sasa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kwenye ngazi za Halmashauri tusimamie hilo ili kodi hii isiwe kero kwa wananchi. Lakin nishauri Halmashauri pia zianzishe mfumo wa kuzitambua hizi nyumba, ili uwe na uhalali wa kuitoa nyumba ushuru wa majengo ni lazima uitambue. Kwa hiyo maeneo ambayo nyumba zimeishajengwa na hauwezi kutoa hati basi angalua mfumo wa kutoa leseni za makazi, kama ambavyo Halmashauri nyingine zinafanya basi ufanyike ili nyumba itambulike na baada ya hapo ikionekana ina sifa za kuanza kutozwa kodi iweze kutozwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nipongeze Serikali kwa uamuzi wa kufanya majadiriano na kukubaliana na Serikali ya Uganda ili bomba la mafuta lipite kwetu, kutoka Uganda mpaka Tanga na hili bomba Jimboni kwangu litapita kwenye Kata kama tano; Kata ya Igusule, Kata ya Mwamala, Kata ya Kasela na Kata Mwangoye. Ushauri wangu yule Mkandarasi Mkuu atakayepewa kazi ya kujenga bomba, basi kazi ndogo ndogo atoe, agawe kwa wakandarasi wa ndani lakini maeneo ambayo bomba la mafuta litapita wale vibarua ambao wanatakiwa kufanya kazi zisizohitaji ufundi basi watoke maeneo hayo hayo ya vijiji, ambalo bomba linaweza kupita ili angalau wananchi waweze kunufaika na bomba hilo kupita kwenye maeneo yao. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Fatma Toufiq, baadae Mheshimiwa Richard Mbogo, halafu Mheshimiwa Rose Tweve na baadae atafuatia Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami nichangie mada iliyoko mbele yetu. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana

Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuandaa na kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja moja kwa moja. Katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 47 mpaka 48 Mheshimiwa Waziri amebainisha jinsi Serikali inavyojitahidi kudhibiti mapato kwa kuweka mashine za EFD na pia kuwa na mfumo wa kieletroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote za Serikali bado kuna baadhi ya wafanya biashara ambao sio waaminifu hawatoi risiti na kuna baadhi ya wananchi wengi bado hawaombi risiti. Hivyo basi, mapato mengi hayaingii katika mfumo ambao tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana baadhi ya wafanya biashara na wananchi hawafahamu umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya Taifa. Nilikuwa napenda kuishauri Serikali yangu sikivu pamoja na Wizara ni budi kwamba hii elimu ya mlipa kodi bado inahitajika sana katika jamii yetu na ikiwezekana iwe ni ajenda ya kuduma na hata ikiwezekana ianzie katika shule za msingi ili wanafunzi wetu waweze kuipata elimu hii ili mwisho wa siku watakapokuwa watu wazima na wao wasiweze kukwepa kodi kwani watafahamu faida ya kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa pia ninaomba niongelee kuhusu sekta ya utalii, nidhahiri kwamba sekta ya utalii imekuwa ikiingizia Taifa letu fedha za kigeni na ni sekta ya pili kwa kuingizia Taifa letu fedha za kigeni. Lakini kwa masikitiko makubwa sana katika bajeti hii, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri halikutiliwa mkazo hili jambo kuhusiana na hii sekta ya utalii. Sambamba na hilo katika hotuba ya Kamati ukurasa wa 40 imebainisha kwamba bado sekta ya utalii inakabiliwa na changamoto za Kisheria pamoja na za kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba utalii ambao uko hapa nchini kwetu ni ule ambao ni *high profile tourism* ambapo watalii wengi wanaokua hapa nchini wanatumia matumizi yao makubwa zaidi ni pamoja na mahoteli na usafiri. Katika malazi mahoteli mengi sana yanamilikiwa na wageni, hivyo basi pesa nyingi za kigeni haziingii hapa nchini badala yake zinawanufaisha wale wageni katika nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa tu naomba niishauri Serikali yangu kwamba hebu ingeweka mkakati wa uhakiki wa kuona ni jinsi gani wazawa wanawezeshwa ili kusudi waweze kumiliki haya mahoteli ili mwisho wa siku, pesa hizi ziweze kubakia hapa hapa nchini na sisi tuweze kufaidika na pesa hizo. Kwa sababu kwa taarifa iliyopo pesa inayobaki kwenye utalii ni pesa kidogo sana ambayo ni *hotel levy*, pamoja na ile pesa ambayo inatokana na kwenye mishahara ya *pay as you earn*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo jambo jingine ambalo katika utalii ni suala zima la usafiri. Usafiri unachukua asilimia 50 ya mapato katika suala zima la utalii, hivyo basi nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua kuleta ndege na kulifufua Shirika la Ndege, pamoja na dhamira ya dhati ya kuona kwamba ndege zaidi zinaweza kupatikana, kwa sababu upatikanaji wa ndege hizo utasaidia sana utalii katika nchi hii kwa hiyo kwa vyovyote vile pato la Taifa litaweza kuongezeka kutokana na utalii. Kwa sababu kwa takwimu zilizopo ni kwamba, zaidi ya dola 1.5 bilioni ambazo zimelipa kwenye sekta ya utalii, zimekwenda kwenye usafiri na kwenye usafiri huo waliofaidika zaidi ni mashirika ya ndege ya nje kwa mfano kama *Qatar Airways, Emirates* na mengine ambayo pia sikuyabainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba hebu Serikali naendelea kumuomba Mheshimiwa Rais aendeleo kufanya kazi kwa bidii sana pamoja na longolongo zote hizi zilizopo, pamoja na maneno ambayo baadhi ya wananchi wanamkatisha tamaa, wenzetu wa upinzani lakini

ukweli ni kwamba mwisho wa siku watajua nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais kwa sababu ana nia nzuri sana kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba niungane mkono pamoja na wenzangu wote ambao wamenzungumzia kuhusu hii tozo ya shilingi 40 katika mafuta na mimi pia niungane na wenzangu kwamba hebu Serikali ione ni jinsi gani tozo hii sehemu yake ipelekwe katika sekta ya maji ili kusudi tuweze kumtua mwanamke maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la sekta isiyo rasimi napongeza Serikali kwa yote, lakini mimi ushauri wangu ulikuwa ni kwamba ili kusudi tuweze kujua idadi ya watu walioko katika sekta isiyo rasimi, ni vizuri ukafanyika utaratibu wa sensa katika kila Wilaya, katika kila Halmashauri, katika kila Mji au Jiji ili kubaini hao watu wako wangapi, lakini mwisho wa siku ufanyike utaratibu wa watu walioko katika sekta isiyo rasmi waweze kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja na ninashukuru sana kwa kunipa fursa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Fatma Toufiq, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Rose Tweve ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwanza naomba nimshukuru Mungu kwa nafasi ambayo anatupatia na pili kwanza niunge mkono hoja ya bajeti hii ambayo Waziri amewasalisha nawapongeza kwa uwasilishaji mzuri, na pia kwa Waziri kuwa *flexible* na *comments* za Wabunge pamona na wadau mbalimbali ambao umeweka ndani ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitakuwa sina furaha kama nisipompongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ya pekee ambavyo amekuwa na jitihada katika kuendeleza Nchi hii, tumeona katika hotuba kuna maeneo

ambayo yamepewa msukumo wa kipekee ambao ni msukumo tunasema wa Mheshimiwa Rais. Tukianza na ujenzi wa reli ya *standard gage*, ni msukumo wa Rais, ufufuaji wa Shirika la Ndege la *Air Tanzania* nimeshangaa sana kuona baadhi ya Wabunge na hasa rafiki zangu kule wanakandya juu ya kufufua *Air Tanzania*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani nchi yoyote ambayo inataka kukuza utalii lazima usafiri wa ndani uimarishwe, Ethiopia kuanzia mwaka 1963 waliweza kuanzisha Shirika la Ndege na wamelisimamia mpaka leo limekua na Addis Ababa ndiyo *hub* ya dunia nzima na wanaweza kukuza uchumi wao na sasa hivi wameongezea maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona juhudi za Rais pia kwenye Mchuchuma na Liganga. Tunaomba Serikali muangalie huyu mwekezaji ambaye yuko tayari kutoa huu mtaji tuharakishe aweke fidia kwa wananchi kazi ianze. Tukipata chuma pamoja na umeme tutapunguza gharama ya uendeshaji wa Shirika la *TANESCO* maana sehemu nyingine ambako hakuna gridi ya Taifa wanatumia majenereta na uendeshaji wa mafuta ni mgumu ndiyo maana kila siku tunataka bei zipande na inakuwa ni gharama kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya uwekezaji na pia kwenye gesi ya kimiminika ambako Serikali imewekea mkazo yote ni maeneo ambayo ya msukumo wa kipekee ambayo bajeti hii imewapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nizungumzie kuhusu tozo ya shilingi 40 ambayo tumeweka kwenye mafuta. Mheshimiwa Waziri kama itakupendeza tubadilishe tu jina, hii tuite tu tozo kwa ajili ya Mfuko wa Maji Vijijini. Kwa nini nasema hivyo? Mwaka jana tulikulilia sana kuhusu Mfuko wa Maji Vijijini, lakini ukasema tusingeze kwenye mafuta kwa mwaka jana wa fedha ambao tulikuwa tunaujadili 2016/17. Basi mwaka huu hii shilingi 40 iwe *ring fenced* kwenda kwenye maji ili makusanyo ya fedha hizi moja kwa moja tuwe na *cash flow* inayotosha kwa ajili ya maji vijijini

na ile bajeti ambayo tumeikubali mliyoishusha ya Wizara ya Maji kutoka shilingi bilioni 900 mpaka shilingi bilioni 600 lakini kwa Wabunge wote tulisema kwamba bajeti hii ikamilike kwa asilimia 100. Sasa ili iweze kukamilika kwa asilimia 100 bajeti ya shilingi milioni 600 lazima tuwe na chanzo cha uhakika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba kwenye mabadiliko ya Sheria yako kwenye *Finance Bill* ambayo utaiteta hii tuiwekee *amendment* na mimi nitakusaidia *ku-lodge schedule of amendment* ili fedha hii iwe *ring fenced* kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nije kwenye tozo ambazo zinahusu Halmashauri. Tunajua nia kabisa ya Serikali ni kuondoa mzigo kwa wakulima, lakini naomba tu nikumbushe Bunge lako ni kwamba Halmashauri zilianzishwa kwa mujibu wa Katiba, Ibara 145 na 146 ni kwa ajili ya kushughulikia wananchi wetu huku chini. Sasa zimeathirika kwa namna tatu, namna ya kwanza kwa kubadilisha Sheria namba 290 ambapo tozo ya mazao inashusha kutoka asilimia tano mpaka tatu na mbili kwa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya pili ambayo Halmashauri zinaathirika ni kutokana na baadhi ya makusanyo kuchukuliwa na *TRA* ambapo ni mabango na *property tax*. Aina ya tatu, Halmashauri zinaathirika kwa mapato yao ya ndani ni kutokana na namna ya ujazo ambapo umeweka kwamba chini ya tani moja mtu asiweze kutozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikianza kwenye tozo. Mfano Halmashauri yangu ya Nsimbo asilimia 50 ya makusanyo tunapata kutoka kwenye zao la tumbaku. Kwenye bajeti hii 2017/2018 kwenye tumbaku tunatarajia kupata milioni 440 ambapo fedha hii tulikuwa tunatarajia kwamba iingie kwenye miradi ya maendeleo. Sheria mnaajua kabisa, makusanyo ya ndani na asilimia 60 inapelekwa kwenye miradi ya maendeleo na ndani ya asilimia 60 kuna ile asilimia tano ya vijana na akina mama. Kwa hiyo, kwa

kupunguza haya makusanyo ya Halmashauri na kwenye bajeti yetu hapa Halmashauri zetu ni shilingi bilioni 687 matokeo yake hizi zinaenda kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutaomba Waziri atuambie *compensation* ya hizi Halmashauri kutokana na kuathirika kwa mabadiliko ya sheria namna ya kutoza wana-*compensate* kiasi gani. Mimi nitaomba Mheshimiwa Waziri, kabla hatujaenda kwenye *schedule of amendment* na tukakubaliana kukubali mabadiliko yako au kuyakataa, tutaomba *comfort* yako ni jinsi gani Serikali inaenda kufidia Halmashauri zetu ambazo zinaathirika. Halmashauri nyingi hasa za vijijini wanategemea hizi tozo. Kwa mfano ukienda hapa Gairo ni mazao tu, hamna dhahabu hamna nini, wanategemea mazao haya. Ukienda Vwawa – Mbozi wanakusanya karibuni bilioni tatu, ni kwenye mazao, ukienda Nsimbo na Halmashauri nyingi. Sasa hapa Serikali naomba mjiandae, bila *comfort* kwakweli tutakutana kwenye *schedule of amendment*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu kilimo, Serikali ina nia nzuri kabisa. Tumeona tozo mbalimbali zimepunguzwa kwenye aina mbalimbali za mazao lakini kwenye mbegu Mheshimiwa Waziri hatujaona! Hujafuta VAT ili mbegu inayozalishwa humu ndani nchini iweze kushindana na ile ambayo inatoka nje ya nchi. Vile vile kwenye kilimo Mheshimiwa Waziri bado Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo hujaiongezea mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utalii; bajeti yako na tunajua nia kabisa ya Serikali ku-*promote* utalii lakini pia bado tunahitaji tuone juhudi zaidi ili utalii wetu uweze kufidia suala la mapato ndani ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu madini. Nashukuru sana umeongeza baadhi ya tozo kwenye madini, lakini watu wenye leseni za madini *primary license, mining license they are always doing false declaration on their revenue*. Hawasemi ukweli juu ya mapato, kwa hiyo Serikali ione namna gani ili soko liwe huru

watu waje pale wauze kwa uhuru na Serikali iweze kupata mapato. Leo hii muulize mtu hata mwenye leseni sehemu zote za madini au leseni ndogo *PML* au *ML*, waulize kwa mwaka wanaingiza ngapi? Hawakuambii ukweli lakini tunaona maisha yao yanavyokwenda na Serikali tupate mapato. Mimi tu Halmashauri ya Nsimbo *service levy* hatupati! Wananunua, wanauza kimya kimya/kisiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe tena kuzungumzia kuhusu Benki Kuu ya Tanzania. Benki Kuu ya Tanzania inatanua huduma kanda mbalimbali. Tunaomba Kanda ya Magharibi Benki Kuu ijengwe tawi pale Katavi. Ukiangali Katavi pale kiusalama ni mbali na Ziwa Tanganyika na nchi zinazotuzunguka za majirani. Kwa hiyo, tawi la Benki Kuu lije lijengwe pale Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kodi kwenye mafuta ya ndege. Umeongeza kodi kwenye mafuta ya ndege ne tunajua kila ndege ina *maximum takeover weight* kwa hiyo tutawafanya kwamba wasiweke mafuta mengi hapa kwetu wanaenda kujaza sehemu nyingine hasa ndege za *transit* kwa hiyo tunaomba kodi hii Waziri aisimamisha kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa upande wa Serikali yetu, bajeti yetu ya trilioni 31 kodi ni trilioni 17. Nimuombe Waziri, hapa *TRA* wamejifunga kitanzi. Ongezeko la mpaka Juni tunatarajia mtakusanya trilioni 14.2; lakini kwenye bajeti 2017/18 makusanyo ya kodi ni trilioni 17. Sasa mnaenda kufanyaje ili ongezeko la trilioni mbili na ushee liweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika. Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kabla sijaanza naomba ninukuu maneno ya busara kabisa ya baba wetu wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwenye kitabu chake cha *Freedom and Socialism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 32 anasema; *for too long we in Africa and Tanzania as part of Africa we have slept and allowed the rest of the world to walk around and over us*. Kwa tafsiri isiyo rasmi anasema; sisi Bara la Afrika na Tanzania tukiwa sehemu ya Afrika tumelala kwa kipindi kirefu wakati wenzetu wakitembea na wengine wakitembea hadi kwenye migongo yetu. Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa Amiri Jeshi Mkuu wanchi hii ambaye hajalala na anaendelea kutuamsha Watanzania wote kuhakikisha hatupotezi rasilimali za Taifa hili. *I know some people are still in denial*, lakini kwa yaliyotokea juzi *I am sure a lot of people are catching up*. Najua tutafika, Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba nichukue fursa hii nikupongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baba yangu Mheshimiwa Mpango na dada yangu Mheshimiwa Ashatu kwa kutoa bajeti ambayo imetatua changamoto nyingi zilizokuwa zinawasumbua Watanzania. Nikupongeze kwakutoa tozo la kwenye mazao. Hii imewasaidia sana *especially* wanawake ambao ndiyo nguvukazi kubwa wanaojishirikisha na shughuli za kilimo. Kwa hilo nawapongezeni sana.

Vilevile nikupongeze kwa kuongeza hii tozo ya shilingi 40, lakini nakusihi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ili wananchi wasisikie uchungu wa tozo hii, tunaomba zitakapokusanywa tuhakikishe tunaenda kutatua zile kero ambazo zimekuwa zikiwasumbua muda mrefu *especially* issue ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Iringa bado tuna changamoto kubwa ya maji. Maeneo ya kilolo kule Ilula bado ni changamoto kubwa, Mufindi, Mafinga bado ni changamoto kubwa, pale mjini kidogo wamejitahidi na Iringa Vijijini bado tuna changamoto ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna jambo lingine ambalo ningependa niliongelee. Kwa mujibu wa Sheria ya *Finance Bill* ya 2016, tulitaka hawa *operators* wote wa simu walete hisa zao sokoni maana ya *Dar es Salaam Stock Exchange*. Lengo lilikuwa ni kuongeza *transparency* ili tujue ni nini kinaendelea kwenye haya makampuni.

Pili, tulitaka kuwapa fursa Watanzania ili waweze kushiriki moja kwa moja katika kumiliki uchumi wa nchi yao, haya ndiyo yalikuwa matarajio yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Vodacom walikwenda sokoni ili kutekeleza takwa hili la kisheria. Nikiuliza hapa Wabunge wangapi wamenunua hisa hizi *they will be very few*. Sasa kama muitikio huu umekuwa mdogo kwa Waheshimiwa Wabunge, *imagine* kwa mwananchi wa kawaida kule kijijini ambaye hajapewa elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ifuatavyo; wakati haya makampuni mengine yanajipanga kwenda sokoni sasa sisi ingebidi tuhakikishe tunatoa elimu kwa wananchi. Elimu ya kutosha na tusiwaachie makampuni ya simu peke yao. Sisi kama Serikali tuna taasisi nyingi ambazo ziko jirani na hawa wananchi zitaweza kutoa elimu juu ya umuhimu wa kumiliki hisa hizi. Sasa kwa sababu muitikio umekuwa mdogo basi tupunguze kutoka kwenye hii asilimia 25 tuanze asilimia 10 mpaka 15 *then* baade hali ikikaa vizuri tutarudi *back to* asilimia 25. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tushirikishe hata wenzetu kuna hawa *East African Community, SADC* na baadae hata iende dunia nzima kama wenzetu wa *TBL* na *TCC* walivyofanya. Nina uhakika hili jambo linawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri utakapokuja kumaliza hapa ulipatie kidogo ufafanuzi. Wenzetu wa Kenya, Serikali ya Kenya imefanya *non tax barrier* kwa wasambazaji na wasindikaji wa gesi ambayo inatumika nyumbani. Sasa hivi hawa wasambazaji kutoka Tanzania hawaruhusiwi kupeleka gesi hii nchini Kenya. Hii ni kinyume kabisa na matakwa ya *East African Community*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kama Wakenya wataendelea na msimamo huu na sisi tuzuie bidhaa zao kuingia nchini Tanzania. Ni nani haelewi ni kiasi gani Wakenya wame-*benefit* kutoka kwenye nchi hii? Leo *Blue Band* tunazotumia nyingi zinatoka Kenya, tukija kwenye maziwa, robo tatu ya maziwa ambayo yanaingia Tanzania yanatoka Kenya, madawa, sabuni zinatoka Kenya. Hii sio sahihi, natambua ushindani wa kiuchumi lazima uwepo na mimi hapa nilishauri lazima tu-*send statement* uwezo wa kuzalisha maziwa nchi hii tunao! Tuna ng'ombe wa kutosha, tuna viwanda vizuri vya kisasa. Iringa pale tuna kiwanda kikubwa cha Asas, nilisema *last time* kina uwezo wa ku-*process* lita laki moja kwa siku. Na pale Iringa kuna wananchi ambao maziwa yanaozea ndani. Nimekuwa naongea, tuwatengenezee miundombinu, *collecton centres* tuwape hawa wakusanye maziwa yaende kwa yule mwenye kiwanda pale. Tu-*send statement* kwa hawa Wakenya kuwa tuna uwezo wa kuendesha viwanda vya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na tukiikubali hii habari ya gesi moja tutapoteza ajira, pili tutapoteza mapato. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba hili jambo tulitolee ufafanuzi wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naendelea kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nawatakia heri katika utekelezaji wa bajeti hii. Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rose Tweve, tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa baadae

Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Rashid Shangazi wajiandae. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema lakini vile vile nichukue nafasi hii kuweza kumshukuru sana Rais wangu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana ambayo ameendelea kuifanya kwa ajili ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu tu kugusia mambo machache katika hotuba ya Bajeti ya Serikali. Kabla sijaanza, niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais amejitahidi sana kufanya mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu na baadhi ya mambo ambayo ameyafanya ambayo lazima tumshukuru na tuendeleo kumuunga mkono ni mambo yafuatayo:-

Kwanza, suala la kuhamia Dodoma halikuwa jambo dogo kwa hiyo kwa nia hiyo njema ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Serikali yanahamia Dodoma na kufanikisha zoezi hilo baada ya miaka zaidi ya 40 ni jambo la kumshukuru sana na kumpongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ni masuala ya usafirishaji. Zoezi hili la kuunda reli kwa kiwango cha *standard gauge* ni jambo ambalo lazima tuishukuru Serikali na tuendeleo kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi ambazo wanaendelea kufanya kwa sababu ninaamini kabisa kama reli hii itakamilika ina maana uchumi wa nchi yetu utaboreshwa zaidi na hatimaye tunaweza tukapata mafanikio makubwa katika siku chache zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile amejitahidi sana kuhakikisha kwamba masuala ya watumishi hewa, wanafunzi hewa, manunuzi ya ndege, meli mbili lakini vile

vile amerudisha nidhamu katika masuala mazima ya kazi. Haya ni mambo ambayo tulikuwa tukiyatamani na tumempata sasa kiongozi au Rais ambaye ameweza kweli kufanya mabadiliko makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo moja ambalo limetokea kipindi kifupi kilichopita nalo ni kuhusu masuala la madini, masuala ambayo ni muhimu sana katika ujenzi wa Taifa letu. Suala la makinikia ni suala ambalo kweli ni la muhimu sana katika ujenzi wa Taifa letu. Tukiangalia kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais amejitahidi kulifuatilia na kulifanyia kazi suala hili na hatimae leo hii tunaenda kuunda sasa utaratibu mpya wa kuleta ule Muswada katika Bunge hili ili tuweze kuweka sheria ambayo itaweza kuhakikisha kwamba tatizo la madini katika nchi yetu linakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili sio jambo dogo, ni kweli kwamba katika nchi/mataifa mbalimbali mbalimbali wamejitahidi sana kufanya utaratibu wa kuja katika nchi maskini, kunyonya nchi maskini, kuchukua rasilimali zetu, kuondoka nazo na kutuachia na umaskini katika nchi yetu. Lakini tumempata Rais ambaye ameenda kufanya mabadiliko, amelichukua hili kama jambo lake, amelichukua hili kama jambo la Serikali na hatimae sasa kuwafanya Watanzania waanze kuanza maisha mapya kwa kuwa na imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba jambo kama hili ni jambo ambalo linahitaji kwa ujumla wetu bila kujali upinzani, bila kujali Chama Tawala kuhakikisha kwamba tunamuunga mkono Rais katika kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba kwenye Bajeti ya Serikali, bajeti ya mwaka jana ilieleza kwa undani zaidi ikasema kwamba kuna zile dola milioni 500 ambazo zilikuwa zinatakiwa kutoka katika Serikali ya India ambazo zilikuwa zinalenga uboreshaji wa miundombinu ya maji katika nchi yetu. Lakini mpaka leo fedha hizo hazijatoka.

Ningependa kuishauri Serikali na kuendelea kuwashauri wadau ambao wako nje katika nchi ya India, wafanye kazi ya ziada, Serikali iendeele kusukuma, kutoa msukumo wa hali ya juu ili tuweze kupata fedha hizi ziweze kusambaa katika maeneo mbalimbali ya Taifa letu ili tatizo la maji sasa liweze kupungua. Tukiweza kufanya hivi tutapunguza adha ya maji katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna akina mama ambao wako vijijini, kuna watoto ambao wako vijijini, kuna shule na taasisi mbalimbali ambazo hazijafikiwa na huduma hii ya maji. Tukipata fedha hizi inakuwa inaleta sababu moja au maana moja kwamba tutapunguza adha ya maji katika maeneo mbalimbali hasa katika yale maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba Taifa letu linapita katika wakati mgumu sana, wakati ambapo katika vijiji vyetu kila kona utakayoenda tatizo la maji litakuwa ndilo tatizo la kwanza kuzungumzwa. Lakini lazima tuendeele kuiwekea mkazo hii ya kwamba fedha ambazo zimewekwa katika Wizara au zimeombwa na Wizara husika Serikali iweze kupeleka fedha zile ili maji yaweze kutatuliwa kama changamoto kubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ongezeko la Deni la Taifa limekua. Lakini ni lazima tuangalie, je, ongezeko hili tunaweza tukalihimili au hatuwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kitu kimoja, nchi mbalimbali katika dunia hii bado wanaendelea kukopa, wala isiwe shida kwamba Tanzania deni la nchi au Deni la Taifa limeendelea kuongezeka. Tuangalie nchi kama Marekani, tuangalie nchi zingine kama Kenya, tuangalie nchi zingine za Bara la Afrika, je, zinaendelea kukopa au haziendelea kukopa na je, katika suala la ukopaji tunakopa kwa ajili gani, hauwezi ukopoa bila kuwa na sababu maalum, na sisi tunavyoendelea kukopa isimaanishe kwamba Watanzania labda ni maskini, isimaanishe kwamba Watanzania hatuna mikakati ya namna gani tunaweza

kukamilisha changamoto zetu za kimaendeleo, tunakopa kwa sababu tunataka tukamilishe miradi mbalimbali ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata fedha hizi ina maana ni moja kwa moja tunaenda kuhudumia miradi mbalimbali katika vijiji vyetu katika miji yetu na kuhakikisha kwamba miundombinu ambayo tunaiona kwa mfano *fly over* tunaziona Dar es Salaam, hii ni sababu mojawapo kwamba tunavyoendelea kukopa ina maana tunaboresha miundombinu yetu, kama tunatengeneza reli, barabara na miundombinu mingine yoyote ambayo tunaweza kuitamka, kama tutatumia fedha hizi kwa uangalifu na tukakopa kwa uangalifu basi wala isiwe shida kwa sababu deni hili ni *sustainable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mengi ya kuongea nijaribu kugusia tatizo moja la benki ya *FBME* ambayo miezi kama miwili iliyopita ilisimamishiwa leseni yake, niseme tu kwamba benki hii ni muhimu kwa wananchi, na kuna wateja ambao waliweka fedha zao katika benki ile. Imefika sasa wakati kwamba Serikali iweze kutoa tamko la moja kwa moja kwamba ni lini sasa fedha hizi ambazo wananchi au wateja ambao wapo katika benki hii wataenda sasa kuzipata, kwa sababu mpaka sasa hivi imekuwa kama ni *dilemma*, haieleweki kama Je, Serikali itatoa lini tamko kwamba leseni hii baada ya kufungiwa sasa wateja waende wapi kuchukua fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi yoyote na hasa uchumi katika mataifa madogo kama Tanzania ambayo yanategemea ukuaji wa mabenki, ambayo yanategemea ukuaji wa fedha ambazo zinakuwa *deposited* katika mabenki mbalimbali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo ilikuwa kengele ya kwanza ni kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa hiyo.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja, nakushukuru sana Mungu akubariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa, tunaendelea na Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae na Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya pili ya Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ambayo mwaka jana wakati tunachangia bajeti humu ndani ilijinasibu sana na tukawa tunaambiwa Waheshimiwa Wabunge tulieni bajeti ni ya kwanza.

Mimi jinsi ninavyoamini kati ya awamu zote zilizopita na zinazoendelea naweza nikasema kuwa, awamu itakayofanya vibaya na Watanzania watakuja kulia sana ni Serikali hii ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnawaahidi Watanzania mnaacha kutekeleza mliyoyaahidi mnakuja mnatekeleza mambo tofauti na vile mliyoyaahidi, yaani mnaimba kama malaika mnakuja kucheza kama mashetani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mliwaahidi Watanzania kuwajengea barabara....

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjulisha Msemaji anayeendelea amesema kwamba, Serikali ya Awamu hii wananchi watajutia kuliko Serikali zote. Nataka nimuambie kwamba wananchi wa Tanzania walipiga goti na kuomba Mungu awalettee kiongozi atakayetawala nchi hii, sasa kama anataka kuwa tofauti na Watanzania naomba atuambie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na atambue tu kwamba Watanzania hawakupiga goti, bali John Pombe Magufuli ndiye aliyepiga pushapu kuomba Watanzania wampe kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu uzilinde.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo sasa jamani taarifa tupunguze jamani nawaombeni.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti afute neno mashetani sisi sio mashetani! Anasema sisi ni mashetani naona kama anasumbua Taifa, afute neno mashetani hakuna shetani hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti naomba uendelee jamani, tunaomba tutulie.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kuweza kuniruhusu niweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, wakati wagombea wakijinadi na vyama mbalimbali vikijinadi kwa Watanzania, vilikuwa vinanadi mambo mbalimbali ama shughuli mbalimbali za kijamii ambazo vyama hivyo

vitatekeleza kama vitapewa ridhaa. Mliwaahidi Watanzania kuwajengea barabara ili ziweze kupitika kwa mwaka mzima kipindi cha masika na kipindi cha kiangazi, hamjajenga barabara hata moja, mnawapelekea Watanzania waende wakawalipie *motor vehicle*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hujajenga barabara unaenda unampelekea mwananchi wa kijijini akakulipie *motor vehicle* na Wabunge mko humu ndani mnapiga makofi, wananchi wenu kule vijijini barabara zisizopitika kipindi cha masika waende wakalipe hii *motor vehicle* hii siyo sawa, kwenye Ilani ipi ya Chama cha Mapinduzi mstari upi, ukurasa gani uliandika kwamba mtaenda kuwalipisha Watanzania *motor vehicle*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *motor vehicle* mmeamua kwenda kuwapelekea Watanzania kwa kupandisha mafuta ya taa, *diesel* na *petrol* yaani leo Watanzania wa nchi hii, umeme ni anasa, walibakia na mafuta ya taa, nayo mafuta ya taa yanaenda kuwa anasa kwa Watanzania. Mnaturudisha enzi za huko nyuma zama za kale za kwenda kuanza kutembea na vijinga kwenye vyumba kwa nini tunawafanyia Watanzania vitu vya namna hii ninyi? Hivi kwa nini hamna moyo wa huruma! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kupandisha mafuta ya taa wakati umeme umeshindwa kuwafikishia Watanzania unakwenda kuendeleza kumdhoofisha Mtanzania maskini aendelee kuwa maskini mpaka siku yake ya kufa, hii inajidhihirisha kuwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Ilani yenu inajidhihirisha kuwa hamjawahi kuwa na dhamira ya dhati ya kwenda kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini na ndio maana mnachokiadi hamtekelezi na mnajua mkitekeleza watu hawa wakiwa na uwezo wakawa na uchumi wao kwa *story* zenu hawatawachagua, kwa hiyo, mnabakia kila siku mnaahidi hiki mnaenda kutekeleza kitu kingine ili baada ya miaka mitano ikiisha mrudi tena kwenda kuahidi namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la

kwenda kuhamisha *motor vehicle* kuwapelekea Watanzania waende wakalipe si sawa, si sawa kuwahamisha yaani *motor vehicle* ya Kunti nimpelooke mtu mwingine kule kijijini aende akanilipie *motor vehicle*, kila mmoja aende atimize wajibu na majukumu yake, Watanzania wale hawajatutuma sisi tununue magari, ni Watanzania wangapi wenye magari? Watu wengi waliopo vijijini hawana magari kwa hili suala nadhani halikai sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Wabunge mnasema kwamba eti ile shilingi 40 iende kwenye maji, unakumbuka tulipendekeza hapa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji tulisema tutoe shilingi 50 iende kwenye maji, leo mnasema 40 iende kwenye maji, aliyewaambie inaenda kwenye nani? Nani aliyewaambieni inaenda kwenye maji? Hii inapelekwa badala ya *motor vehicle*, *motor vehicle* itakatwa kule tukinunua mafuta ndio umelipa *motor vehicle*, kwa hiyo, hili suala si sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kodi ya majengo, Watanzania hawa wanajenga kwa shida kweli, lakini kitu cha kwanza Mtanzania huyu analipa kodi ya ardhi, Mtanzania huyu analipa kodi kwenye *cement*, kwenye nondo, kwenye bati, kwenye kila kitu mpaka mchanga anaochota ardhini ukisombwa pale anaulipia kodi, leo tena hivi vijumba vyao ambavyo wamejijengea kwa shida mnaenda tena kuwanyonya hawa Watanzania waende wakawalipieni tena kodi, tena mnaenda kuwapandishia kutoka shilingi 3,000 mpaka shilingi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawataka nini hawa Watanzania wa watu *yallai toba maulana*, wametukosea nini Watanzania? Hivi kuwapa ridhaa ya kuongoza nchi hii ndio imekuwa adhabu kwao? Waoneeni huruma hawa Watanzania, mlienda kuwapigia pushapu mpaka misamba ya suruali ikachanika, kwa hiyo, waoneni kwamba ile huruma waliowapeni basi hebu itumieni kuweni na moyo wa huruma kwa binadamu wenzenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kodi ya majengo si

sawa, mngekuja mimi nilikua najua hapa mngekuja mkasema kwamba kama mnataka kodi ya majengo basi vifaa vya ujenzi vipinguzwe kodi ama viondolewe kabisa, ili muweze kuchukua hiyo kodi ya majengo, hamtoi vifaa vya ujenzi vinapanda kwa kupandisha mafuta vifaa vya ujenzi vitapanda. Lakini pili mnawapandishia hivyo vifaa vya ujenzi mnakwenda tena mnawatoza na kodi za majengo huko waliko, jamani mnawakamua kiasi hiki wamewakosea kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shilingi milioni 50, ni suala lile lile tunaimba kama malaika tunacheza kama mashetani, mliahidi hapa na mwaka jana tulisema, hili suala la milioni 50.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Kunti, atoe angalau shukrani, maana kutoka hapa Dodoma kwenda mpaka Jimboni kwake Chemba ni lami, shaaaa! anafika kwa haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mariam nimsamehe bure tu, Jimbo lenyewe la Chemba halijui huyu, hiyo barabara imepita wala wananchi wa Chemba hawanufaiki na chochote kwenye lile Jimbo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipaza sauti kuashiria kutokukubaliana na mzungumzaji)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Chemba, tulieni ninyi nini mnachozomea kitu gani? Tulieni hiyo, vitulizeni taratibu *crisapen* iingie, vitulizeni visiwashe saa hizi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika zangu tatu zimebaki naomba unilindie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shilingi milioni 50, mliwaahidi Watanzania kila kijiji kuwapatia shilingi milioni 50, tunataka tujue shilingi milioni 50 ni lini au ni deni watakuja kuwadai waanzie wapi kudai shilingi milioni 50, hatujaziona kwenye kitabu cha Waziri humu shilingi milioni 50 ziko wapi? Mlijinasibu na shilingi milioni 50 leo mwaka wa pili, bajeti ya pili hii kitabu kinapita *empty*, hata dalili wala harufu wala sisikii Mbunge wa CCM akiongelea suala la shilingi milioni 50, ni lini hizo shilingi milioni 50 mtazitoe?

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa inasema hivi shilingi milioni 50 iko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano, kwa miaka mitano tutatoa shilingi milioni 50 sio kila mwaka itatoka. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti malizia.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahisi Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hawanielewi. Nimesema hivi jamani mlichokiahidi sicho mnachokitekeleza ni miaka miwili sasa, mliahidi shilingi milioni 50, mliahidi barabara, matokeo yake *mmeahidi barabara mnaenda kuleta Bombardier ambazo zinaanguka hovyoy bila utaratibu*. **[Maneno haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeahidi shilingi milioni 50 mmeenda kujenga uwanja wa Chato wa ndege! Hivyo ndiyo vitu shilingi milioni 50 mtaitoa lini? Siyo suala kwamba miaka Mitano, hivi vingine havikuwepo hata kwenye Ilani yenu, vimepatikanaje? Halafu unakuja unaniletea *story* hapa eti Ilani ya Chama cha Mapinduzi inanihusu nini mimi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Waziri akija hapa atuambie, shilingi milioni 50 ni lini zinaanza kutolewa kwa Watanzania wetu, ukidai ujue na kulipa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti naomba, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti....

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Mheshimiwa Kunti, kuna Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuzungumza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa sasa kwa Kanuni ya 68(1) pamoja na 64(1)(a) Msemaji anayesema sasa anasema uongo kuhusiana na kwamba kuna ndege zinaanguka. Naomba athibitisha, vinginevyo afute kauli yake, kwa sababu mimi kama Naibu Waziri mwenye dhamana, hakuna ndege iliyoanguka. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Naibu Waziri amethibitisha kwamba hakuna ndege iliyoanguka naomba ufute kauli yako ikiwa kama una uthibitisho ulete.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ndege ilishindwa kuruka *mummy*, jamani, kazi yetu ni kuwaambieni ukweli ili muweze kufanya haya mambo sasa kama kila kitu mnakataa mnachotaka nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti upo tayari kuthibitisha kwa hilo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege ilishindwa kuruka Kigoma, ndicho nilichokisema

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanguka na kushindwa kuruka ni tofauti.

**MWENYEKITI:** Ndege ilishindwa kuruka ama ndege ilianguka?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba tuelewane kwanza tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshatoa uthibitisho kwamba hakuna ndege iliyoanguka, Mheshimiwa Kunti anasema kwamba ndege ilishindwa kuruka ni tofauti na alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Kunti naomba ufute kauli yako uliyozungumza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba tutulie, Mheshimiwa Kunti kwanza tumalizane na unafuta kauli kuhusiana na hilo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi, labda nirudie na *Hansard* ziende zikachukuliwe, nimesema hivi mnacho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti naomba unisikilize, aidha ufute kauli au ulete uthibitisho.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie maneno yangu. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Naomba tuelewane, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshazungumza na ametoa uthibitisho kwamba hakuna ndege iliyoanguka na wewe ulizungumza ilianguka sasa naomba ufute kauli ama ulete uthibitisho kama kuna ndege amabyo imeanguka. (*Makofi*)

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema naomba unisikilize au *Hansard* ziende zikaletwe nilichokisema, mnachokiahidi sicho mnachokitekeleza, mliahidi shilingi milioni 50 mmeenda kununua Bombardier ambazo ni mbovu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, naomba yale

ambayo umeyazungumza kuhusiana na kuanguka kwa ndege tu tuwe hapo kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mmeenda kununua Bombardier ambazo ni mbovu, nikiwa namaanisha kwamba ni ndege iliyoshindwa kuruka Mkoani Kigoma.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti unaenda kinyume na yale ambayo umezungumza mwanzo, tumemaliza Mheshimiwa naomba ukae tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa ni muhimu sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti dakika zangu bado.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti kwanza tumalizane, unafuta kauli ama?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, amefuta kauli, tuendeleo.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda taarifa ya mwisho.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mimi ni Mbunge wa Viti Maalum kutokea Mkoa wa Kigoma na nina uhakika kwamba Ndege ya *Air Tanzania* ilidondoka.

**MWENYEKITI:** Naomba tuelewane, Mheshimiwa Sungura umepewa na nani nafasi ya kuzungumza? Malizia Mheshimiwa Mapunda.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anayesema analiongopea Bunge, anasema katika Ilani ya CCM haikusema ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege, naomba ninukuu na inasema hivi "Katika kipindi cha miaka mitano Ilani ya Uchaguzi ya CCM Serikali itaboresha huduma ya usafiri wa anga ikiwepo na ujenzi wa viwanja vya ndege." (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Muda umekwenda mwingi Mheshimiwa naomba umalize kwa dakika moja.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na sio dakika moja zilikuwa zimebaki tatu nimeweka *stop watch* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Dakika moja naomba kwa sasabau muda umepoteza maneno unaongea mengi ambayo hayakubaliki.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wenyewe ndio wanaleta michecheto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo, nilikuwa naangalia hapa vipaumbele vya mwaka huu 2017/2018, ukuzaji wa ujenzi wa misitu na uchumi wa viwanda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, basi naomba ukae muda umekwenda mwingi.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu bado.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti naomba ukae muda umeenda mwingi sana. Tunaendelea hapa hakuna kuyumba, tunataka ukweli na uwazi, mnaongea maneno mengine ambayo hayako katika ukweli. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi na baadaye Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba kabla sijaendelea niwaambie wenzangu Waheshimiwa Wabunge waende katika Kitabu cha Maendeleo Fungu Namba 21 Hazina wataona pale kuna shilingi bilioni 60 kwa ajili ya *Village Empowerment* hapa ndio kwenye zile shilingi milioni 50 kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijaribu tu kumsahauri Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hili ni agizo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi na humu ndani tuko vyama vingi ni vema hizi shilingi bilioni 60 ungeanza katika Majimbo yale ya Chama cha Mapinduzi ambao kimsingi ndio wameahidi kwenye Ilani yao, hizi Ilani nyingine ambazo hatujawahi kuziona ungeweka pembeni kwanza, kwa hiyo shilingi bilioni 60 ambayo iko kwenye Fungu Namba 21 Kitabu cha Maendeleo hiki hapa wote msome *Village Empowerment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii adhimu kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, kazi hii ya kuzuia makinikia, ni kazi ambayo ni ya ujasiri mno haijawahi kufanywa na kiongozi yeyote wa Taifa hili tangu Awamu ya Pili, ya Tatu na ya Nne. Kama tunasema zimeundwa tume lakini zimeishia kuwa ni Tume ambazo labda zimeweka makabrasha pembeni lakini huyu amechukua hatua ya kwenda hata kuzuia.

Kwa hiyo, ni jitihada za kijasiri sana ambazo zinapaswa kuungwa mkono na kila mzalendo wa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshauri na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria yuko hapa kwamba kuna watu wanatutisha kwamba tutashitakiwa. Lakini kwa bahati nzuri Mwenyekiti wa Barrick ameshakuja kuonesha kwamba anahitaji maridhiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kwa sababu siyo jinai ni madai, madai yanaanza kwanza kuzungumza ninyi wenyewe, inaposhindikana ningeshauri kwamba tusiogope tuende kwenye Mahakama ya Kimataifa (*International Court of Justice - ICJ*), kule tunapelekana baada ya kushindwa kuelewana. Kwa hiyo hii ni mahakama huru kabisa tunakwenda kule tunashitaki na tunaweza tukapata haki zetu stahiki, kwa sababu kuna *dispute* imefanyika ndani ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niseme hata kwenye Mahakama zetu, kuna ile *alternative dispute resolution* ambayo kabla hamjaamua kushtakiana mnaweza kwanza mkakaa ili kutafuta *amicable way* ya ku-solve matatizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri najua wewe huna makeke ni mtulivu na ni mwanasheria ambaye umebobea, kwa hiyo hili naamini litakwenda vizuri.

## T A A R I F A

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba kama tulivyomfahamu wengi, Mheshimiwa Rais Mtukufu alieleza wale mabwana tayari wamekubali kulipa. Sasa haya

masuala unayosema ya mahakamani ya nini tena, wameshakubali kulipa hiyo ndio kauli ya Amri Jeshi Mkuu wa nchi hii, nakupa taarifa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii kwa kuwa amesema ndugu yangu Khatib kwamba naye anaelewa kwamba mwelekeo ni kulipa basi naipokea, safi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo kwenye tozo ya shilingi 40 kwenye mafuta, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapozungumza hii tozo, kwanza inaanza kutozwa kwenye ushuru, yale makampuni yanayoingiza mafuta ndio kwanza wanawekewa hii tozo. Mafuta yakishalipiwa ushuru yakishatoka, yakishaingia kwenye usambazaji hakuna tena kodi pale, mafuta hayana VAT ndio maana EWURA wako pale kwa ajili ya kuweka bei kikomo. Sasa hivi kwa sababu tunaingiza mafuta kwa njia ya *bulk procurement* maana yake ni kwamba hata EWURA wataangalia *competitive price* na kwenye *price stabilization* ya mafuta REA ipo, reli ipo, kwa nini tushangae mafuta leo? Hata hiyo shilingi 50 ya maji ipo, mbona gharama hazikuongezeka? Kwa hiyo hili ni suala la kitaalam. Mambo haya ya mafuta niwaambie hata hayo mafuta ya taa sasa hivi tunaagiza kiasi kidogo sana, yako makampuni 23 yanayoingiza mafuta hapa nchini, lakini hayazidi matano yanayoingiza mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ya taa yanatumika kwa kiasi kidogo sana sasa hivi, tusidanganye, ni lazima Watanzania tutanue wigo wa walipa kodi. Walipa kodi walikuwa ni wachache sana ndio maana hao hao kila siku wanakamuliwa, lakini tunavyotanua wigo wa walipa kodi maana yake ni kwamba hata huyu mtu mdogo ambaye anatomia lita mbili atuchangie shilingi 80. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii niseme kwa dada yangu Mheshimiwa Majala, wewe ni Muislam na katika uislam kuna

*Zakatul - Mal* (zaka ya mali) kila shilingi 100 unatakiwa ulipie japo shilingi mbili na nusu, hii haikwepeki. Hata katika Wakristo fungu la kumi lipo, kodi haijawahi kumpendeza yeyote. Tunasema hapa lazima watu walipe ushuru, lazima walipe kodi, kama ambavyo kanisani watu wanatoa sadaka na kama ambavyo kanisani watu wanatoa fungu la kumi na kule misikitini watoza *Zakatul- Mal* na hata huu mwezi wa Ramadhan wewe unatakiwa utoe *Zakatul- Fitr* kabla ya kuswali sala ya Idd. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mamlaka hii ya Magufuli ni mamlaka inayotoka kwa Mungu na haya ndio maagizo kwa mujibu wa vitabu. Kwa hiyo, lazima tutanue wigo wa ulipaji kodi, kodi inapolipwa na watu wengi kwanza inakuwa ni rahisi kulipika, inapungua, pia tunaongeza katika mfuko wetu tunapata kodi nyingi zaidi. Nani aliyewaambia kodi ya *road licence* ilikuwa inaenda kununua maandazi ya wafanyakazi wa *TRA*? Ilikuwa inaenda kwenye huduma. Kwa hiyo, hata hii ya tozo ya mafuta inakwenda kwenye huduma, hivyo tsubiri mwakani kama utekelezaji haupo, tuwaambie mmechukua shilingi 40 kwenye kila lita utekelezaji wake uko vipi, lakini suala la kodi halikwepeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la viwanda. Kule Tanga viwanda vyetu vingi vimefungwa kwa sababu ya mambo ya kodi pia wengine ni kwa sababu ya ushindani wa kibiashara. Naomba nitoe rai Kiwanda cha *Afritex* cha nguo kimefungwa, nimeshazungumza sana Mheshimiwa Waziri, pia wenzetu wale wa *Tanga Fresh* wanapewa deni ambalo haliwahusu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri ulisimamie deni hili ili wawekezaji hawa waweze kuona *comfort* ya kufanya biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kiwanda cha Chai cha Mponde, umeshazungumza kwamba wawekezaji kupitia Mfuko wa *LAPF* watakwenda kuwekeza pale, lakini sasa ni mwaka wa tatu bado tunaona mambo hayaendi. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba katika Halmashauri ya Bumbuli, Jimbo la Bumbuli, Kata 14 zinalima chai, kwa hiyo, kufungwa kwa kiwanda hiki ni msiba

mkubwa wale wananchi kwa kweli tumewakosea sana, wanashindwa kuzalisha mali na wanashindwa kuongeza pato la Taifa kupitia uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni usambazaji wa umeme vijijini. Ninashukuru kwamba Wizara ya Nishati na Madini imetoa vijiji 146 katika Mkoa wa Tanga, ni vijiji vichache sana ukifananisha na Mikoa mingine. Nimuombe Waziri mwenye dhamana aliangalie hili kwa umakini sana, kwa sababu kama katika Halmashauri ya Lushoto na Halmashauri ya Handeni, Halmashauri pekee zina Majimbo mawili mawili...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shangazi malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Waziri mwenye dhamana tuangalie hili kwa kina sana kuhakikisha kwamba tunapata viwanda vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza hiyo?

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Martha Umbulla baadaye Mheshimiwa Ester Mmasi ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi nami nichangie hoja hii iliyoko mbele yetu.

Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mahali hapa kuchangia hii hoja, aidha niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri wa Fedha, Dkt. Philip Mpango, Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kutuletea bajeti ya kihistoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri, ni ya matumaini makubwa kwa wananchi na wananchi wameipokea pamoja na kebehi zote zinazotolewa na Wapinzani Wabunge wenzetu, lakini bado wananchi wameisifia na wanakwenda kuitekeleza kwa sababu ni bajeti shirikishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mawasilisho ya Kambi Rasmi ya Upinzani, wenzetu wameibeza bajeti hii katika misingi ya takwimu. Kutofautiana kwa vitabu *Volume One, Two, Three, Four* ni suala la takwimu tu ndugu zangu, haiwezi kuwa suala la kihistoria kwamba bajeti hii haifai. Kuna wachangiaji wachache wametuhumu sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kujenga kiwanja cha ndege kule Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni Rais wa Tanzania lakini ni Rais anayetambulika kimataifa, ni Rais anayetambulika na dunia nzima, ajenge kiwanja cha ndege mashuhuri, tena kikubwa sana kule Chato, watu wengi watapenda kwenda kuona amezaliwa wapi Rais Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ni wa kimataifa na watu wengi wanampenda, kujenga kiwanja cha ndege ni kitu kidogo sana na binadamu hana jema...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atakapomaliza muda watasema hajafanya kitu.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mzungumzaji anavyosema kwamba watu watapenda kwenda kuangalia alikozaliwa Mheshimiwa Rais. Tunajua kabisa kwamba Mwalimu Nyerere kule Butiama hakijajengwa kiwanja chochote, pia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Mkapu pia hakuna kiwanja kilichojengwa. Kwa hiyo, asijenge hoja kwa masuala ambayo kwa kweli hayana msingi kabisa. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu hafananishwi na mwenzake, kila mtu na mazaliwa yake, mapendo yake, juhudi zake na mambo yake tofauti, kwa hiyo siipokei hoja taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la ukusanyaji wa fedha *TRA*. Mwaka jana wakati tunapitisha Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) tulikubaliana *TRA* inaenda kukusanya kodi ya mapato kwa ajili ya mapango na kadhalika. Sheria hiyo ya Fedha, tuliipitisha hapa Bungeni wakiwemo Wapinzani ambao leo wanaikebehi. Sababu za *TRA* kukusanya kodi iko katika ukurasa wa 28 waende kusoma, kipengele cha 38. *TRA* imefanya ufanisi mkubwa sana katika ukusanyaji wa kodi na *TRA* ina mtandao mpana sana hapa nchini kulingana na Halmashauri zetu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho jamani sasa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba *TRA haina ufanisi wowote kwa viwango vyovyote vya kimungu na vya kishetani...* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

...kwa sababu kwa taarifa ya Waziri kodi ya mapato, hata kodi ya majengo Dar es Salaam, Manispaa ya Ilala kwa mwaka tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni 18, kwa taarifa yako Mkoa wa Dar es Salaam yote ni shilingi bilioni tisa tu. Kwa hiyo siyo kweli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara naomba ya mwanzo uifute ya kwamba kwa Mungu wala kwa shetani haijafanya kitu naomba uifute hiyo.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara naomba uifute ile kauli ya awali.

**MBUNGE FULANI:** Afute kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara naomba uifute kauli uliyosema kwamba *TRA* hawafanyi chochote kwa Mungu wala kwa shetani naomba uifute kauli hiyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unasema nifute nini?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hebu tulieni kwanza naongea na Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, kauli ambayo umezungumza kuhusiana na *TRA*.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusikiliza Mama.

**MWENYEKITI:** Kuhusiana na *TRA* umezungumza maneno ambayo hayafai ndani ya Bunge kwamba *TRA*.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah siyo mazuri na siyo ya Kibunge?

**MWENYEKITI:** Eeeh.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kwa heshima yako nimeyaondoa hayo.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wameazima watu hawana uwezo kukusanya fedha ya majengo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha naomba uendelee

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba nijielekeze kwenye kuchangia bajeti. Bajeti hii siyo tu imeanisha namna ya kukusanya mapato kwa ufanisi, bali pia imefafanua namna ya kupata, kutumia na kwa uwazi zaidi, ndio maana tunampongeza sana Dkt. Mpango pamoja na Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji. Kubwa zaidi ambalo limewapendeza wananchi ni kwamba bajeti hii imejielekeza kuwanufaisha wakulima wadogo na walalahoi wa vijijini kwa sababu inaenda kuboresha kilimo kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta pekee inayogusa wananchi walio wengi ili waweze kuendelea na kuondoa umaskini ni sekta ya kilimo. Kwa hiyo, bajeti hii inakwenda kuboresha kilimo na kuondoa umaskini katika nchi yetu na ndio maana wananchi wameipokea kwamba ni bajeti ya kihistoria na inaenda kuwanufaisha wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017. Bajeti hii imeanisha ufanisi,

pia imeainisha changamoto, bado kuna changamoto chache. Katika miradi ya maendeleo tumeona kwamba fedha zetu za miradi zilichelewa, tuna imani kwamba Waziri wetu anaenda kuangalia kwa umakini sana changamoto ya kuchelewesha fedha za miradi, vilevile kuhakikisha kwamba zinafika kwa wakati na zinakwenda jinsi bajeti hiyo ilivyokuwa imeidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna mikakati ya mipango tuliyojiwekea kwamba haijakaa vizuri na hiyo nayo ni eneo la kuliangalia kwa sababu haina maana mipango yetu tuiweke mizuri lakini haiendi kutekelezwa jinsi ambavyo tumeainisha kwenye kitabu cha mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba ili bajeti hii iwe shirikishi tuweze kuteua kamati itakayosaidiana na Baraza la Madiwani kuhakikisha kwamba Wenyeviti wa vijiji, Maafisa Watendaji, wazee wawili, viongozi wa dini, timu kamili iweze kuundwa kuhakikisha kama *watchdogs*, kuhakikisha kwamba fedha zinazokwenda kwenye miradi na fedha zinazotoka kwenye tozo mbalimbali zinazokwenda kwenye maji ziweze kuangaliwa, ziweze kunufaisha wananchi jinsi ambavyo Bunge limepitisha na kuhakikisha kwamba zimewanufaisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye kukuza uchumi. Tanzania tumebarikiwa, tunazo rasilimali nyingi, tuna rasilimali watu, Rais wetu alisema kwamba kwenye maeneo mbalimbali imesheheni maprofesa, madaktari, mainjinia lakini bado tuna tatizo la rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji na utekelezaji wa masuala mbalimbali bado uko nyuma kwa ajili ya utendaji usio wa uaminifu, wezi na mambo kama hayo. Naamini kwamba Waziri wetu Mheshimiwa Angellah Kairuki katika eneo hilo anahusika. Yeye ni Waziri makini, aende kuangalia ni namna gani atajengea uwezo watumishi wa umma ili waweze kuwa waaminifu kuhakikisha kwamba miradi yote ya maendeleo, mipango yote inayoelekezwa katika kuleta maendeleo, suala la rasilimali watu linapewa kipaumbele

kuacha hata rasilimali fedha. Kwa sababu Baba wa Taifa aliwahi kusema kwamba fedha siyo msingi bali watu ndio maendeleo zaidi na juhudi inaletwa na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye suala zima la vipaumbele katika nchi yetu. Katika utekelezaji wa bajeti ninashauri Serikali iangalie maeneo ya pembezoni. Naomba kutoa mfano mdogo, leo hii ukamchukua mwanamke wa Kihadzabe, ukamweka pale ukampa milo mitatu, ukampa mavazi, ukampa na mafuta ya kujipaka. Upande huu ukampa mwanamke wa Kiswahili, ukampa chakula milo mitatu, ukampa mavazi, ukampa na mafuta, yupi atakayeonesha *impact* haraka? Ni yule ambaye hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wetu wa Manyara tuko pembezoni sana, tuna makabila ambayo bado wako nyuma sana, tunaomba utekelezaji wa bajeti hii ilenge maeneo ya pembezoni, iweze kuwanufaisha wananchi wale wa chini sana ili na wao waweze kuona maana ya kuwa Tanzania, maana ya kuishi katika hali nzuri kuondokana na umaskini na kuondokana hali duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara tuligawanyika kutoka Mkoa wa Arusha mwaka 2002, lakini hadi leo *resources* nyingi bado ziko Arusha. Mkoa wetu unazalisha mazao mengi sana, mazao haya yanafaa kwa ajili ya kuanzishwa viwanda vidogovidogo. Tazama ng'ombe wengi wanatoka Mkoa wa Manyara, wanatoka Simanjiro, Kiteto, Hanang na Mbulu lakini kiwanda cha nyama kiko Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iangalie kwa umakini sana ni wapi inaenda kuanzia kwa kuweka kitu gani? Ni wapi inaenda kuanzia viwanda kwa ajili ya rasilimali zipi? Tunaomba Kiwanda cha Nyama kijengwe Babati ili tuweze kutengeneza ajira ya wananchi wetu na kuweza kunufaisha wananchi wa Manyara na wanufaika na rasilimali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie *potential* ya

kila mahali, Mkoa wa Manyara una *potential* katika michezo ya riadha. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda umemalizika naomba umalize sentensi ya mwisho.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sasa tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh na baadaye Mheshimiwa Raphael Japhary pamoja na Mheshimiwa Ester Mmasi atamalizia.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitaanza na makinikia ambayo kidogo yameelekea kama kutugawa huku ndani kiasi ambacho juzi Mheshimiwa Abdallah Ulega alisema kwamba sisi ni *UNITA* na kwa kwa sababu hakukatazwa na hakuna kiongozi yeyote aliyemwambia afute kauli hiyo nataka niulize maswali matatu/manne.

Nani *UNITA* zaidi au upande ule ambao wanafuta matokeo ya uchaguzi na wanaweka watu wasio halali? Nani *UNITA* zaidi wanaofuga mazombi ambao kila siku wanapiga raia? Nani *UNITA* zaidi ambao wanatunga sheria za kuzuia watu wasitoe maoni yao na wanafungia magazeti? Nani *UNITA* zaidi ambao wanaweka Masheikh kwa miaka minne hata bila kesi kufanyika? Hilo nimemaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nilitaka kusema kwamba hii makinikia imekuja ili kutupunguzia uwezo wa kuchangia katika bajeti yetu hapa. Mimi sioni kama ni bahati mbaya kitu ambacho kiko nje ya Bunge kimeletwa hapa ndani kimetupunguzia uwezo wetu wa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilihudhuria kwenye

kongamano moja ambalo linasema hapa Tanzania watoto 30.2 wenye uwezo wa kwenda shule hawaendi shule, hatujadili hapa tunaona kama kitu kidogo tu. Jana tumesikia kwamba, asilimia 34 ya watoto wa Kitanzania wana utapiamlo, tumeacha kulizungumzia hapa! Lakini pia, tumeacha kuzungumzia kwamba bajeti yenyewe imekuja na mashimo mengi ambayo yanapaswa yajazwe, pia bajeti yenyewe imekuja ikiwa imetekelezwa chini ya asilimia ndogo ya ile ya mwaka jana, imetutoa katika *mood* na tumeanza kuzungumza mambo mengine ambayo hayakuwa na umuhimu kuyazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mambo ya bajeti nina mambo mawili matatu, kwanza ni Deni la Taifa. Mimi siyo katika wanaoamini kwamba deni letu linanyumburika, sijui linafanya kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisema na kusema kweli *rate* ya mwaka jana imeongezeka mwaka huu kwa hivyo, bado nina maoni kwamba Deni la Taifa linapaswa likabiliwe inavyopaswa na sio kuona kwamba linahimilika kwa hivyo tuliachie liendeleo. Mwaka jana nilisema na mwaka huu narudia, ziko nchi zilikuwa zikisema hivyo hivyo kwamba deni linahimilika lakini zimesambaratika, Greece, Venezuela, Peru na wengine, hilo la pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mwaka jana nilisema na mwaka huu nasema tena. Bado sioni faida ya Serikali ya Muungano kwa Zanzibar katika mambo makubwa. Nilisema mwaka jana kwamba katika miradi kielelezo basi angalao mmoja uwepo Zanzibar. Hii nasema kwa sababu Zanzibar tuko watu 1,200,000 ukipeleka mradi ambao unaajiri watu elfu tano, elfu sita, maana yake umeajiri *work force* yote ya Zanzibar, lakini bado Serikali ya Muungano inaona kwamba bado haitaki kufanya wajibu, mimi nahisi ni wajibu, inaona haina wajibu kwa Zanzibar. Lakini Zanzibar itafanyaje mambo makubwa wakati uchumi wake unazuilika na upande huu? Kodi zake haziwezi kukusanywa kama inavyotakiwa? Lakini itakavyokuwa vyovyote vile uchumi wa Zanzibar ni uchumi mdogo hauwezi kufananishwa na uchumi wa Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachotaka kusema ni kile ambacho Mheshimiwa Ulega alisema siku mbili tatu nyuma, nampa *credit* yake. Alisema kwamba Rais Magufuli anafaa sasa aelekeze kwenye ku-*invest* kwenye mambo ya bahari, lakini hata leo Mheshimiwa Adadi alisema jambo hilo. Sisi tumezungukwa na nchi ambazo ni *land locked*, Rwanda, Zambia, sijui wapi, wote wale, tungekuwa tumejijenga kwenye bahari tuna meli za kutosha, tuna uwezo, tungelamba *cargo* zote za nchi hizo, sio tu wakati wa kuodoa, lakini hata wakati wa kuingiza, hilo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni suala la *aqua culture*. Wiki tatu nyuma nilisema katika Wizara ya Maliasili kwamba bado hatujatumia *blue economy* na kitu kimoja ambacho kina utajiri mkubwa sana, narudia tena ni bahari, kuanzia Bahari Kuu kule mpaka pembezoni humu. Kwa kuwa watu wengi wameshazungumzia Bahari Kuu, mimi nazungumzia hapa pembezoni; nilisema utajiri wa hapa pembezoni uko katika fukwe pale, kwa maana ya kufuga vitu kama kamba, kufuga vitu kama kaa, ambazo ni *billions of dollars*. Nchi kama Vietnam ambayo tuna urafiki nayo, nchi kama China, hawashibi kwa mazao ya bahari. Chochote utakachozalisha wewe wanaweza kukichukua kama vile ambavyo India ukizalisha chochote kile cha *beans* hizi, chochote kile watakichukua. Kwa hiyo, nasema tena Mheshimiwa Waziri, hilo tulifanye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lilizungumzwa leo suala la afya. Tungewekeza katika afya kiasi cha kutosha tukawa na hospitali ambazo ni kubwa ni za maana, watu wasingekuwa wanakwenda India. Tuna majirani zetu hapa chungu nzima wangukuwa hii ndio India yao wanakuja kwetu. Serikali najua hii haitafanya kazi muda huu, itandike misingi yakuwezesha hilo lifanyike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye suala la elimu. Suala la elimu wenzetu mfano *Northern Cyprus* moja katika kipato chao kikubwa ni kwenye elimu au nchi nyingine. Tumekuwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina *brand* moja nzuri sana kupita kiasi duniani, lakini kimeshindwa kukua

nje ya Tanzania kimebaki hapa hapa, wakati wenzetu kama Marekani utakuta *American University* iko Misri, iko Lebanon, iko wapi. Na sisi kama tungejipanga vizuri tungeweza kutumia eneo letu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Mama Rwakatare jana alisema hapa au juzi, kwamba kuna kodi nyingi kwenye elimu kiasi ambacho hatuvutii watu kutoka nje. Nchi kama Cyprus watu kutoka nje ni mataifa 144 wanakwenda kusoma Cyprus, wana wanafunzi zaidi ya laki mbili kutoka nje ambao wanasoma katika nchi yao. Tukifanya hii kama ni sehemu ya kipato, tukatengeneza vizuri, tukapunguza kodi, tukai-*streamline*, naamini inaweza kutusaidia sana kwenye mapato ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo linaweza kutusaidia ni kwenye *diaspora*. Mpaka sasa *diaspora* tunasema *in general terms* kwamba waje wawekeze. Je, tumeonesha maeneo gani wanaweza kuja kuwekeza? Tumetangaza wao kama *diaspora* watapata vivutio gani kuja kuwekeza? Kwa hiyo, ina maana kwamba kama tukijipanga vizuri tunaweza kutengeneza hiyo ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tunajenga reli. Reli kutoka inakotoka mpaka inakokwenda hapa katikati kungeweza kufanywa vitu vya kuweza kusaidia, ili *local content* iwe na maana, lakini kama tutajenga reli tu ili itoke mwanzo kama ilivyo sasa inatoka Dar es Salaam inakwenda mwisho wa reli Kigoma, hapa katikati hapana chochote kuwasaidia watu wafanye *local content* itakuwa haina maana yoyote. Kwa hiyo, nashauri kama tunajenga reli hii kubwa, tusilenge tu kwamba tutatoa makaa kutoka kule mpaka kuja huku, lakini pia katikati hapa kuwe na uwezekano wa kuwawezesha watu wafaidi kwa *local content*. Hali kadhalika katika hili bomba la mafuta linalotoka Uganda kuja Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumza Mheshimiwa Selemani Zedi hapa katikati watu wapate ajira. Sio ajira tu kwa maana ya vibarua, lakini *what after that?* Nashauri

kwamba kama tunataka tuwatengenezee watu fursa nzuri ya maisha, basi tuwatengenezee *local content* ili waweze kusaidia, lakini kama tukizubaa hapa chakula cha wafanyakazi wa reli watakaojenga, Waturuki kitatoka Uturuki badala ya kuwawezesha wananchi wetu hapa wakasaidia. Chakula cha wafanyakazi ambao wanajenga hilo bomba kitatoka kwingine, tujipange katika haya ili tuweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Tunaendelea na Mheshimiwa Raphael Japhary Michael na baadae Mheshimiwa Mmasi atamalizia.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba niunge mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hoja ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo napenda kulizungumza hapa ni ambalo limekuwa likinadiwa sana katika bajeti hii kwamba hii bajeti ni ya kihistoria. Na mimi nimepita kwenye hii bajeti kwa kadri ilivyowezekana nikitazama hiyo historia ya hii bajeti, bahati mbaya sijaweza kuona, labda Mheshimiwa Waziri atanishawishi wakati ana-*wind up* kunionesha jinsi hii bajeti ilivyo ya kihistoria kwa sababu mimi nilivyoiona hii bajeti ni tegemezi kama zilivyo bajeti nyingine zote ambazo zimepita katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inategemea kukusanya shilingi trilioni 19.9 mapato ya ndani, takribani na inategemea kutumia kutumia shilingi trilioni 19.7 mapato ya ndani kwa matumizi ya kawaida. Sasa najaribu kujjuliza tofauti yake na bajeti zingine ni nini kwa sababu bado asilimia 38 ya bajeti hii inategemea mikopo ama misaada kutika nje. Kwa hiyo, nilikuwa najaribu kutafuta huo uhistoria na mimi siuoni! Naomba sana kushawishiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shilingi trilioni 11 za maendeleo pesa yenye uhakika wa kupatikana katika bajeti hii ni mikopo ya ndani ya shilingi trilioni 6.1 mikopo ya shilingi

trilioni 5.56 tunategemea kutoka wa wahisani au washirika wa maendeleo ama mikopo kutoka nje. Katika kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba, mahusiano yetu na washirika wa maendeleo sio mazuri na ndio maana imeundwa timu ya pamoja ya kutoa ushirikiano wa namna gani tume huru inaweza ikasaidia namna ya kujenga mahusiano na washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini mahusiano yetu sio mazuri wakati yalikuwa mazuri wakati wa Mheshimiwa Mkapu mpaka tukafutiwa madeni? Ni kwa nini mahusiano yetu sio mazuri wakati wa Mheshimiwa Kikwete mpaka tulikuwa na *International PR*? Kwa nini kwa sasa hivi mahusiano yasiwe mazuri? Ni lazima Serikali ingetakiwa ijiangalie mmekosea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo mlilokosea ni la wazi kabisa, wanazungumza kila siku. Mmekiuka misingi ya demokrasia katika nchi hii, mmekiuka misingi ya utawala bora, mmezuiia uhuru wa vyombo vya habari, mmetengeneza sheria mbovu za mitandao, ni vitu vya wazi. Sasa mnatafuta kitu gani cha kuzungumza na hao mnaowaita mabeberu ambao angalau wana-*good governance* kuliko sisi Watanzania ambao sio mabeberu? Kwa hiyo, nilikuwa natamani nipate sababu ya kwa nini bajeti hii inaitwa bajeti ya kihistoria, ambayo ni bajeti tegemezi kama zilivyo bajeti nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, bajeti hii haina uhalisia, sio *realistic*. Kwa sababu, najaribu kuangalia ni namna gani tutapata shilingi trilioni 17.1 kwenye mapato ya ndani wakati tunakwenda kukopa sisi, kama Serikali, kwenye benki za ndani zaidi ya shilingi trilioni sita. Kwa misingi hiyo tunazuia *private sector* kukopa, hiyo *private sector* inaposhindwa kukopa italipaje kodi kwa Serikali, ili tupate mapato ya shilingi trilioni 17.1? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini biashara zinafungwa, makampuni yanondoka kwenye biashara tunakuja kuambiana hapa kwamba, kuna makampuni 200,000

yameongezwa katika kujiandikisha kwenye biashara. Sasa najjuliza swali...

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ambayo inamtaka mchangiaji kusema maneno ambayo ni ya ukweli. Tumeshtuka kuona kwamba anasema taarifa inasema kwamba, Serikali haina mahusiano mazuri na wahisani, tunaomba athibitise.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raphael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa mujibu wa Kanuni, Serikali ndio ilitakiwa ithibitise kwamba ninayosema siyo ukweli, lakini naomba twende kwenye ukurasa wa 41 mpaka 42. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu, Mheshimiwa Waziri anasema; Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali itaendelea kupanua soko la fedha na mambo mengine, lakini 42 anasema; katika jitihada za Serikali kutaka kuimarisha ushirikiano kati yake na washirika wa maendeleo na kuhakikisha fedha zinazoahidiwa zinatolewa kwa wakati, Serikali na washirika wa maendeleo walitafuta washauri elekezi huru, timu hiyo iliongozwa na Dkt. Donald P. Kebaruka aliyekuwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Washauri Elekezi walipewa kazi ya kutathmini na kutoa mapendekezo ya kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo na muundo wa utoaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwa namna ya lugha yoyote itakayofaa kutumika, kama ni kuimarisha, *what*

so ever mimi sina ubishani katika hilo, hoja yangu ni kwa nini sasa nchi ambayo tumekuwa na uhusiano na hawa washirika siku zote mpaka madeni yakafutwa na *Paris Club* wakati wa Mheshimiwa Mkapa, mpaka tukawa na mahusiano makubwa ya kusifika wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne, kumeingia kitu gani Serikali ya Awamu ya Tano? Ndiyo hoja yangu ya msingi ninayotaka kuuliza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo hoja ina ukakasi, Serikali itabidi mniwie radhi, lakini ndicho kilichoandikwa hapa ndani. Kwa hiyo, Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raphael, kilichoandikwa humo siyo mahusiano mabaya baina ya Serikali ni kuimarisha uhusiano.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nimeshakuelewa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, naomba uondoshe ile kauli ya mwanzo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio mabaya, hayako vizuri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ndiyo hivyo ambavyo umesema. Uondoshe kwa sababu sivyo ilivyo kwenye kitabu. (*Makofi*)

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya siyo mabaya, lakini yanaimarishwa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo hivyo eeh, sawa.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka tu kujua kama yanaimarishwa, yanaimarishwa kwa sababu gani? Nilichokuwa najaribu kusema ni kwamba hata bajeti yenyewe kama nilivyosema sio ya uhalisia kwa sababu hiyo

ya kwanza niliyosema kwamba, haiwezekani Serikali mkope kwenye benki za ndani, halafu wafanyabiashara watakopa wapi? Mnajua kabisa kwamba Serikali ina uhakika wa *security* zake kukopeshwa kuliko wafanyabiashara, *private sector*. Kwa misingi hiyo kusinyaa kwa *private sector* haonekani kodi mtapatia wapi ya shilingi trilioni 17. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia biashara nyingi kama nilivyosema zimefungwa, lakini hata matumizi yenyewe ya mashine za *EFD* bado kabisa hatujaweza kuhamasisha kwa kiasi cha kutosha katika mikoa yote katika nchi hii. Inaonekana hizi mashine za *EFD* zinakuwa *so selective* kwa sababu ukienda Kilimanjaro hizi mashine zinatumiwa mno kuliko kawaida. Kiduka cha shilingi milioni 14 lazima kiwe na mashine ya *EFD*, lakini njoo katika maeneo mengine ya nchi hii, hazitumiki! Tena hao ndio wanalalamika sana kwamba, hawana maendeleo, lakini hawataki kutumia mashine za *EFD*. Kwa hiyo, ni lazima haya mambo yafanyiwe kazi kama tunataka kuhakikisha kwamba tunapata hiyo shilingi trilioni 17. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata wigo wa walipa kodi (*tax base*), Mheshimiwa Waziri hajaonesha hata kwamba, labda kwenye taarifa atuambie ni walipa kodi wangapi wa makampuni? Walipa kodi wangapi binafsi? Na walipa kodi wangapi ambao ni wa kawaida ili tufahamu kwamba hivi tunatengeneza *tax base* yetu kupitia wapi, ili tujue uwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Raphael, malizia sentensi ya mwisho hiyo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si hii ni kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo, naomba umalizie sentensi yako ya mwisho.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Makatibu ni ya pili eeh? Kengele ya pili naambiwa hapa.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Dakika moja, ungemalizia hiyo sentensi ya mwisho, unapoteza muda zaidi.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama imetoshwa, hayo niliyosema yanatosha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia dakika zilizobaki chache na Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwenye Kikao hiki cha Bunge. Ninapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri, hakika mmetutoa kimasomaso, hakika mmejibu kiu ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya yanayotendeka, kwa sakata zima la makinikia, Mkoa wa Kilimanjaro umeniagiza kwenye Bunge lako hili Tukufu kwamba, wao wamesimama na Mheshimiwa Rais kwa sababu nao ni wahanga hata kupitia machimbo ya *Tanzanite*. Kwa hiyo, wamenituma niseme kwenye Bunge lako hili Tukufu, ikitokea leo Mheshimiwa Rais anaomba kwenda Mkoa wa Kilimanjaro watahitaji miezi sita waweze kupanua ule uwanja uliompokea juzi kwenye Mei Mosi ili waweze kukaanae na kumpa hongera hizi. Kwa kweli Mheshimiwa Rais popote ulipo pokea pongezi za dhati kutoka kwa Mkoa wangu wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasita leo kujjuliza maswali mengi, nimemuangalia kaka yangu Mheshimiwa Januari

Makamba simuoni! Nilitaka nimuulize neno moja, hivi huu sio ule utabiri wa Mzee Makamba tulipokuwa pale kwenye ule Mkutano Mkuu ambapo walisema alisema huyu ajaye atatubatiza kwa moto, hivi huu sio moto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, imefika tunaongea hata tusiyoyajua. *Network* zimekata, *connection* hakuna, *links* hakuna chochote kinachoendelea katika Bunge hili. Wamekuja watu hapa wanatuambia kwamba makinikia ni suala la mtaani, limeletwa hapa kuja kutufunga midomo, kuja kuchafua Bunge, wapi na wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu pale, namheshimu sana Mheshimiwa Ally Saleh, tuko kikao kimoja kule *SADC*, michango yako naiheshimu sana, lakini kwa kweli leo umenifanya pengine hata nitakosa usingizi juu ya mchango wako juu ya leo. Mbona ilipaswa mpaka tunapokuja kuchangia tuwe tumesoma ripoti ya Profesa Mruma, lakini pia na ripoti ya Profesa Osoro, kwani hatufahamu...

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani hatufahamu ni shilingi trilioni tisa zimepotea kwa miaka 17 kwa Taifa hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Salleh, taarifa fupi.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema mimi ni kwamba, makinikia limekuja hapa kutugawa, sikusema hayo anayosema yeye. Kwa hiyo, namtaarifu kwamba, aseme kile ambacho nimesema mimi, kama ananiheshimu aendelee kuniheshimu tu. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tofauti ya kutugawa na migongano ya kifikra na kimaslahi. Ripoti imeeleza bayana tunapoteza shilingi trilioni tisa kwa mwaka mmoja kwa miaka 17, tumepoteza shilingi trilioni 108. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotambua uchungu wa wavuja jasho wa Taifa hili lazima tuliseme hapa. Kuna *direct link*, tunaona mahusiano ya moja kwa moja kwenye upotevu huu wa pesa pamoja na michango yetu katika Bunge lako hili Tukufu hususan kwa kupitia Wizara hii, Wizara hii na bajeti ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu, kama sio huu ubatizo wa moto, ninashangaa wengine wanasema hapa sisi tumekuja kuimba nyimbo za mashetani! Ngoja nikuulize rafiki yangu kijana wewe unayejiita kijana wa Dodoma hii, sikiliza, sisi hatuimbi nyimbo za mashetani, ndugu yangu tunaimba za kucheza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ninyi mlikaa kwenye Ilani yenu, mlihubiri kufufua wafu, akina Balali mliitambia mnataka kumfufua Balali, ni nani anayeimba nyimbo za mashetani humu ndani? Ni nani anayeongea lugha za kufufua mashetani humu ndani kama sio wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, wamejitahidi sana kutuvunja mioyo humu ndani. Walikuja wakatwambia kwamba, tutaenda kushtakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mmasi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, hapana.

**MBUNGE FULANI:** Muda bado.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mmasi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa dakika zangu.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Bora usingeniita saa hizi, bora usingenipa hii nafasi.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utovu wa nidhamu, Mwenyekiti kasimama, kaa chini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa ningetamani tuendelee, lakini kikanuni muda umemalizika kwa vile ni saa 12.00 jioni tayari.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lolote hapa mbele, lakini kwa vile nawaona wageni kwenye majukwaa yetu, basi naomba niwakaribishe tena katika Bunge letu, lakini mwisho kabisa napenda niwashukuru, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kutuweka salama na kumaliza kazi zetu, lakini ninawashukuru na ninyi pia, kwa namna ambavyo mmewajibika kwa siku ya leo. Naamini kwamba, mwenye kushukuru dogo ndiyo anapewa kubwa. Kwa hiyo, naamini kuna baadhi ya Wabunge ambao hawana tabia ya kuweza kushukuru kwa dogo, watajifunza na waweze kushukuru kwa dogo ili wapate kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Bunge hadi tarehe 19 Juni, Siku ya Jumatatu, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 19 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*